Sh 3000

# MIKAKATI NA MBINU ZA USIMILISHWAJI KATIKA FASIHI YA WATOTO

NA:

MUTHUBI FIDELIS M.

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

JUNI 2005



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

______________________

**MUTHUBI FIDELIS M.**

**(MTAHINIWA)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo hiki.

______________________

**DKT. NDUNGO C.M.**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**Na**

______________________

**BI. PAMELA M.Y.** NGUGI

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

# TABARUKU

Kwa mamangu, Mukami na babangu, Muthubi; mmekuwa mfano mwema kwangu.

Kwa ndugu zangu, Wangari, Mwaura na Njuguna; nawashukuru kwa kunitia ari na moyo wa kuendelea na masomo yangu.

# YALIYOMO


Mada ........ I

Ikirari ........ II

Tabaruku ........ III

Yaliyomo ........ IV

Shukurani ........ XIII

Ikisiri ........ XIV

Vifupisho ........ XVI

Ufafanuzi wa Dhana Muhimu ........ XVII

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI WA TASNIFU**

1.0 Utangulizi wa Tasnifu ........ 1

1.1 Mada ya Utafiti ........ 4

1.2 Malengo ya Utafiti ........ 6

1.3 Sababu za Kuchagua Mada ........ 7

1.4 Upeo na Mipaka ya Tasnifu ........ 8

1.5 Msingi wa Nadharia ........ 9

1.6 Udurusu wa Maandishi ........ 12

1.7 Mbinu za Utafiti ........ 14

1.7.1 Ukusanyaji wa Data ........ 14

1.7.2 Uchanganuzi wa Data ........15

**SURA YA PILI**

**MIKAKATI NA MBINU ZA USIMILISHWAJI WA KAZI ZA WATOTO**

2.0 Utangulizi ........16

2.1 Ploti ........19

2.2 Lugha ........24

2.3 Wahusika ........28

2.4 Maudhui ........33

2.5 Umbo la Kitabu ........33

2.5.1 Vielezo ........34

2.5.2 Jalada la Kitabu ........36

2.5.2.1 Anwani ya Kitabu ........37

2.5.2.2 Maandishi ya Chapa ........38

2.5.2.3 Umbo la Nje la Kitabu ........37

2.6 Hitimisho ........38

**SURA YA TATU**

**USIMILISHWAJI WA HADITHI KATIKA KITABU CHA *ALFU LELA ULELA***

3.0 Utangulizi ........40

3.1 Ploti ........42

3.1.1 Safari Saba za Sinbad Baharia ....................42
3.1.1.1 Safari ya Kwanza ....................42
3.1.1.2 Safari ya Pili ....................43
3.1.1.3 Safari ya Tatu ....................43
3.1.1.4 Safari ya Nne ....................44
3.1.1.5 Safari ya Tano ....................45
3.1.1.6 Safari ya Sita ....................45
3.1.1.7 Safari ya Saba ....................46
3.1.2 Kisa cha Mbilikimo Mwenye Kinundu ....................46
3.1.3 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Tano ....................47
3.1.4 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Sita ....................48
3.2 Lugha ....................49
3.2.1 Tashbiha ....................49
3.2.2 Tashihisi ....................51
3.2.3 Misemo ....................52
3.2.4 Chuku ....................53
3.2.5 Vihisishi ....................54
3.3 Msamiati ....................54
3.4 Usimulizi ....................55
3.5 Wahusika ....................56
3.5.1 Kisa cha Safari Saba za Sindbad ....................56

3.5.2 Kisa cha Mbilikimo Mwenye Kinundu ........ 57
3.4.3 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Tano ........ 57
3.5.4 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Sita ........ 57
3.6 Maudhui ........ 58
3.6.1 Ukarimu ........ 58
3.6.2 Wema ........ 59
3.6.3 Haki ........ 59
3.6.4 Uvivu ........ 59
3.7 Umbo la Kitabu ........ 60
3.7.1 Jalada na Anwani ya Kitabu ........ 60
3.7.2 Michoro iliyojumuishwa Katika Matini ........ 60
3.7.3 Maandishi ya Chapa ........ 61
3.8 Hitimisho ........ 61

**SURA YA NNE**

**USIMILISHWAJI WA RIWAYA YA *MASHIMO YA MFALME SULEMANI***

4.0 Utangulizi ........ 63
4.1 Ploti ........ 65
4.1.1 Matayarisho ya Safari ........ 65
4.1.2 Safari Yenyewe ........ 66
4.1.3 Nchi ya Wakukuana ........ 67

4.1.4 Safari ya Kurudi Nyumbani ....................68

4.2 Lugha ....................70

4.2.1 Tashbiha ....................70

4.2.2 Misemo ....................72

4.2.3 Vihisishi ....................72

4.2.4 Tanakali za Sauti ....................74

4.2.5 Taswira ....................75

4.2.6 Taharuki ....................77

4.2.7 Ucheshi ....................77

4.2.8 Nyimbo ....................78

4.2.9 Tafsida ....................79

4.3 Usimulizi ....................80

4.4 Wahusika ....................80

4.4.1 Bw. Quatermain ....................81

4.4.2 Mfalme Twala ....................81

4.3.3 Gagula ....................82

4.4.4 Bw. Good ....................82

4.4.5 Umbopa ....................83

4.4.6 Bw. Henry ....................83

4.5 Maudhui ....................86

4.5.1 Ushujaa ....................87

4.5.1.1 Ushujaa wa Safari ....87
4.5.1.2 Ushujaa wa Kugundua Mambo ....87
4.5.1.3 Ushujaa wa Ulengaji Shabaha ....88
4.5.2 Maadili ....88
4.5.3 Upendo ....88
4.5.4 Fadhila ....89
4.5.5 Umoja ....90
4.5.6 Haki ....91
4.5.7 Ukatili ....91
4.6 Umbo la kitabu ....92
4.6.1 Michoro ....92
4.6.1.1 Mchoro wa Jalada ....92
4.6.1.2 Michoro iliyojumuishwa Katika Matini ....93
4.6.2 Umbo la Nje la Kitabu ....94
4.6.3 Aina ya Chapa ....94
4.7 Hitimisho ....95

**SURA YA TANO**

**USIMILISHWAJI WA RIWAYA YA *MKASA WA SHUJAA LIYONGO***

5.0 Utangulizi ....96
5.1 Ploti ....99

5.2 Lugha ........ 103

5.2.1 Tanakali za Sauti ........ 104

5.2.2 Methali ........ 105

5.2.3 Tashbiha ........ 105

5.2.4 Misemo ........ 106

5.2.5 Taswira ........ 107

5.2.6 Wimbo ........ 108

5.2.7 Chuku ........ 108

5.2.8 Ucheshi ........ 109

5.3 Usimulizi ........ 109

5.4 Wahusika ........ 110

5.4.1 Liyongo ........ 110

5.4.2 Mfalme Mringwari ........ 111

5.4.3 Moni ........ 111

5.4.4 Shida ........ 112

5.4.5 Sada ........ 112

5.4.6 Mbwasho ........ 113

5.4.7 Halali ........ 113

5.4.8 Jaji na Wazee ........ 114

5.5 Maudhui ........ 115

5.5.1 Ushujaa ........ 115

5.5.2 Tamaa ........ 115

5.5.3 Ufisadi ........ 115

5.5.4 Usaliti ........ 116

5.5.5 Udhaifu ........ 117

5.6 Umbo la Kitabu ........ 117

5.6.1 Vielezo ........ 117

5.6.1.1 Mchoro na Anwani ya Jalada ........ 117

5.6.1.2 Vielezo vilivyojumuishwa Katika Matini ........ 118

5.7 Hitimisho ........ 119

**SURA YA SITA**

**ULINGANISHI NA ULINGANUZI WA USIMILISHWAJI KATIKA: *ALFU LELA ULELA, MASHIMO YA MFALME, SULEMANI* NA *MKASA WA SHUJAA LIYONGO***

6.0 Utangulizi ........ 121

6.1 Ploti ........ 121

6.2 Lugha ........ 122

6.3 Maudhui ........ 123

6.4 Wahusika ........ 125

6.5 Umbo la kitabu ........ 126

6.6 Hitimisho ........ 126



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**SURA YA SABA**

**HITIMISHO**

7.0 Utangulizi ....128

7.1 Muhtasari ....128

7.2 Matokeo ya Utafiti ....137

7.3 Kiishio ....140

7.4 Matatizo ....141

7.5 Mapendekezo ....142

**MAREJELEO** ....143

VIAMBATISHO

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa neema, nguvu na uwezo wa kuiandika kazi hii. Sifa na utukufu ni kwake daima.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wa kazi hii, Dkt. C. Ndungo na Bi. P. Ngugi waliochukua muda wao kuniongoza kwa busara, ukakamavu na kujitolea. Ushauri wao uliniwezesha kuithibiti kazi.

Shukrani kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunitia moyo katika masomo yangu.

Natoa shukrani za kipekee kwa Dkt. E. Alembi, Idara ya Fasihi (Kiingereza), kwa msaada na ushauri alionipa. Pia, shukrani ni kwa ndugu yangu Njuguna aliyenipa msaada palipohitajika.

Aidha shukrani zangu na mkono wa kheri ni kwa Mtume Ziwa aliyenipa matumaini makubwa katika masomo yangu, Mercy na Elizabeth kwa msaada wao wa hali na mali na wanafunzi wenzangu hasa Mary, Nelly na Jacinta kwa ushirikiano wao ambao umechangia pakubwa katika kufaulu kwangu. Asante kwa wale wote wameshirikiana nami katika maombi. Mungu azidi kuwabariki.

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia usimilishwaji wa kazi za watoto katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Lengo la utafiti huu ni kuainisha na kufafanua mikakati na mbinu zinazotumika katika kusimilisha kazi za watoto. Kadhalika utafiti huu umetumia mbinu hizi kuvihakiki vitabu vifuatavyo: *Alfu lela ulela, Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo.*

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya Elimumitindo. Nadharia hii huzingatia lugha na matumizi yake katika kazi za fasihi. Aidha nadharia hii huchunguza mtindo wa mwandishi kama unavyojitokeza katika kazi zake.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura saba. Sura ya kwanza imeshughulikia mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti pamoja na sababu za kuchagua mada hii. Kadhalika, udurusu wa maandishi yanayohusu mada ya utafiti pamoja na msingi wa nadharia iliyoongoza utafiti huu ni baadhi ya mambo ambayo yameshughulikiwa.

Sura ya pili inahusu mikakati na mbinu zinazozingatiwa wakati mwandishi anaisimilisha kazi yake. Mbinu hizi zimeainishwa na kufafanuliwa. Maelezo haya ni muhimu kwani ndiyo yametumiwa kama msingi wa kuchanganua kazi zilizoteuliwa.

Sura ya tatu imekihakiki kitabu cha *Alfu Lela Ulela*. Uhakiki huu unabainisha jinsi usimilishwaji wa ngano (za fasihi simulizi) ambazo zilitambwa na watu wazima kwa hadhira ya watu wazima zinasimilishwa kuwa kazi zinazoilenga hadhira ya watoto.

Sura ya nne imeihakiki riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani*. Uhakiki huu ni muhimu kwani unabainisha jinsi kitabu kinachoilenga hadhira ya watu wazima kinasimilishwa na kuilenga hadhira ya watoto.

Sura ya tano imeihakiki riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Uhakiki huu unatupa picha kamili ya jinsi tenzi zinasimilishwa kuwa hadithi za kusomwa na watoto.

Sura ya sita inahusu ulinganishi na ulinganuzi wa vitabu vyote vitatu vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu ili kuwa na picha kamili ya mwelekeo wa usimilishwaji wa kazi za watoto.

Sura ya saba ni hitimisho la tasnifu hii. Mambo ambayo yamezingatiwa ni pamoja na muhtasari, matokeo, matatizo na mapendekezo ya mtafiti.

**Vifupisho Ambavyo Vimetumika Katika Matini**

Uk. - Ukurasa

Taz. - Tazama

Kbt - Kiambatisho

Vbt. - Viambatisho

Khj - Kama hapo juu

Rej. – Rejelea

## Ufafanuzi wa Dhana Muhimu

### 1 Mtoto

Dhana 'mtoto' inafasiriwa kwa njia mbalimbali kulingana na malengo ya mtafiti. Kwa mujibu wa Mkataba wa Muungano wa Haki na Ulinzi wa Watoto nchini Kenya (2002), mtoto ni mtu au binadamu yeyote aliye na umri chini ya miaka kumi na minane. Mkataba huu unaendelea kufafanua dhana 'mtoto' kisheria ambapo mtoto kulingana na sheria ya ajira ni mtu aliye na umri usiozidi miaka kumi na sita. Sheria ya masuala ya ndoa inamtambua mtoto wa kiume kama aliye chini ya miaka kumi na sita na mtoto wa kike kuwa aliye chini ya miaka kumi na mitatu. Akitumia kigezo cha Piaget, Hunt (1994), anamfafanua mtoto kama msomi chipukizi na ambaye hajazama katika uwanja wa usomaji wa fasihi. Akiungama haya, Tucker (1981) anasema kuwa, mtoto ni kiumbe aliye kati ya kipindi cha kujiunga na shule na kipindi cha kubaleghe. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtoto ni kiumbe aliye kati ya umri wa miaka kumi na miaka kumi na mitano. Huyu ni mtoto ambaye kulingana na Tucker (khj) ana uwezo wa kuisoma hadithi iliyochangamano kidogo na ana uwezo wa kufikiria kidhahania na kufikia uamuzi wa kimantiki.

### 2 Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ni ile iliyoandikiwa hadhira ya watoto. Aidha, fasihi ya watoto ni ile ambayo inawavutia na kusomwa nao hata ingawa haikuandikwa huku

ikiwalenga. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika fasihi ya watoto ambayo hapo awali iliandikiwa hadhira ya watu wazima kisha ikasimilishwa kwa kuandikwa na kusanifiwa upya ili iwafae na isomwe na watoto.

### 3 Usimilishwaji

Usimilishwaji ni ile hali ya kuifanya upya matini chasili kwa kuifanyia marekebisho kama vile kuiandika upya, kuisanifu upya, kuifupisha au kuirefusha na/au kuitafsiri ili iwafae wasomaji wanaolengwa tofauti na wale waliokuwa wamelengwa na hiyo matini. Marekebisho haya hufanywa kwa uangalifu ili kiini cha hadithi kisije kikaathirika.

### 4 Ufupishaji

Ni ile hali ya kuondoa baadhi ya sehemu za hadithi kutoka kwa hadithi yenyewe ili kuifanya iwe fupi. Kwa mujibu wa utafiti huu, ufupishaji una maana ya kuondoa baadhi ya sehemu za hadithi zinazowalenga watu wazima na ambazo ni ndefu kiasi cha kumchosha mtoto anapozisoma ili kuibuka na hadithi ambayo urefu wake utawafaa watoto wanaolengwa.

### 5 Tafsiri

Ni ile hali ya kuhamisha sambamba maandishi kutoka kwa lugha chasili hadi lugha pokezi, yaani, tafsiri sisisi. Katika utafiti huu, dhana 'tafsiri' ina maana ya

tafsiri mawasiliano ambapo matini chasili imeingiliwa na kufanyiwa mabadiliko ambayo yanalenga kumfaa mtoto atakayeisoma matini lengwa. Ni tafsiri ambayo imefanywa bila ya mtafsiri kuwa mwaminifu kwa matini chasili.

**6 Matini Chasili**

Kazi ya awali na ambayo ndiyo hufanyiwa marekebisho na kuandikwa upya, yaani, ile kazi inayosimilishwa.

**7 Matini Lengwa**

Kazi mpya inayotokana na ile ya awali.

**8 Mwandishi/Mtafsiri**

Maneno haya yanarejelea mtu aliyehusika na usimilishwaji wa vitabu ambavyo vimeshughulikiwa katika utafiti huu.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA TASNIFU

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya watoto ina historia ndefu nchini Kenya. Kwa mujibu wa Akoleit (1990) na Mpesha (1995), fasihi ya watoto ya awali ilikuwa fasihi simulizi na ambayo iliendelezwa kabla ya majilio ya Wazungu. Hii ni fasihi ambayo ilipitishwa kwa njia ya masimulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuhifadhiwa katika kumbukizi za wanajamii. Fasihi hii ilijumuisha nyimbo, mashairi, methali, vitendawili na ngano miongoni mwa masuala mengine. Kupitia kwa fasihi hii, watoto walifunzwa mambo mengi kama vile: maadili ya jamii, miiko na makatazo ya jamii na kuwa wenye bidii na watiifu.

Baada ya majilio ya Wakoloni, nafasi ya fasihi simulizi ilichukuliwa na 'Fasihi ya Wakoloni', yaani, fasihi iliyoandikwa na Wazungu kwa minajili ya kusomwa na Wazungu wenyewe. Hii ndiyo fasihi ya mwanzo kabisa kuwahi kusimilishwa nchini Kenya ili isomwe na watoto. Kwa mujibu wa Odaga (1985), fasihi hii ilimsuta Mwafrika na kumtukuza Mzungu. Fasihi hii iliendelea kushika mizizi na kusomwa na watoto nchini hata baada ya uhuru.

Baada ya nchi ya Kenya kujinyakulia uhuru, fasihi ya watoto haikukuzwa, iliendelea kubaki nyuma huku ikidunishwa tu. Kulingana na Akoleit (1990), fasihi hii ilichapishwa pale tu wachapishaji walikuwa na uhakika kuwa vitabu vyenyewe

vingenunuliwa. Jambo hili liliwavunja waandishi wengi moyo na badala yake, wakajitoma katika uwanja wa fasihi ya watu wazima. Kule kutoikuza fasihi ya watoto kuliwafanya watoto waendelee kuvisoma vitabu vya Wazungu vilivyokuwa vimesimilishwa. Hata hivyo, fasihi ya watoto imeanza kupanuka huku kukiwa na waandishi wengi ambao wameanza kuiandikia hadhira ya watoto. Pia, wakuza mitaala nchini Kenya (K.I.E) wakishirikiana na Wizara ya Elimu wamependekeza kuwa, fasihi ya watoto ijumuishwe katika masomo ya shule za msingi. Hii ni hatua muhimu ambayo inachangia katika kukua na kuendelea kwa fasihi ya watoto nchini Kenya.

Fasihi ya watoto huwa na tanzu mbili; fasihi andishi na fasihi simulizi. Katika fasihi andishi msanii anaweza kuibuni hadithi na kuiandika moja kwa moja au anaweza kuibuni kazi yake kutoka kwa kazi ya msanii mwingine kwa njia ya kuisimilisha. Utafiti huu umejishughulisha na fasihi ya watoto iliyosimilishwa.

Usimilishwaji una historia ndefu nchini Kenya. Kulingana na Odaga (1985) na Mpesha (1995), asili ya usimilishwaji wa kazi za watoto nchini Kenya ni Wazungu wenyewe katika kipindi cha ukoloni. Wakiyaungama haya, Gachukia na Akivaga (1978) wanasema kuwa, ukosefu wa vitabu ambavyo vingetumiwa shuleni na watoto kuliwafanya Wazungu wavisimilishe vitabu ambavyo walikuwa wameviandika ili visomwe na Wazungu wenyewe. Naye Oyoo (2003) anasema kuwa, vingi vya vitabu hivi vilivyosimilishwa ni vile ambavyo vilikuwa vimeilenga

hadhira ya watu wazima lakini vikaweza kuwavutia watoto ambao waliweza kuvisoma.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), baadhi ya vitabu hivi ni pamoja na: *Alfu Lela Ulela, Mashimo ya Mfalme Sulemani, Hadithi ya Robinson Kruso, Safari za Guliva, Kisiwa chenye Hazina* na *Elisi Katika Nchi ya Ajabu.* Wanaendelea kusema kuwa, vitabu hivi ndivyo vilikuwa msingi wa riwaya nchini. Usimilishwaji huu uliipenyeza fasihi ya kikoloni nchini Kenya ambapo hata baada ya kazi hizi kusimilishwa, bado ziliendelea kumdunisha Mwafrika huku zikimtukuza Mzungu.

Kutokana na ustawi wa haraka wa kazi za watoto hivi karibuni, waandishi wengi wameanza kusimilisha kazi za watoto katika viwango mbali mbali kwa kutumia aidha lugha ya Kiingereza au lugha ya Kiswahili. Ushairi umesimilishwa na kuwa hadithi fupi au hata riwaya. Kwa mfano, *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001) na *Mwana Kupona: A Poetess from Lamu* (King'ei, 2000). Pia ushairi umesimilishwa na kuwa tamthilia. Kwa mfano, *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001). Hadithi na ngano za watu wazima zimesimilishwa na kuwa za watoto. Kwa mfano, *Alfu Lela Ulela* (Brenn, 1962). Vitabu vilivyowalenga watu wazima vimesimilishwa na kuwa vya watoto. Kwa mfano, *The Gods Are Not To Blame* (Rotimi, 1995), *The Cry of a Goat* (Alembi, 1997), *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Johnson, 1981) na *Chaka The Zulu* (Watkins, 1971). Kazi ambazo zimeilenga hadhira ya watoto zimesimilishwa ili kuifaa hadhira ya watoto katika mazingira

tofauti tofauti. Kulingana na Arbuthnot & Sutherland (1972), kazi ya *Cinderella* imesimilishwa ili iwafae watoto katika nchi mbali mbali.

Ingawa kuna kazi nyingi zilizosimilishwa kwa minajili ya watoto, nyingi zake zimesimilishwa bila kuzingatia mahitaji ya mtoto ambaye ndiye msomaji lengwa. Baadhi ya kazi hizi zilisimilishwa kwa njia isiyofaa kwa kukosa kuzingatia vipengele kama vile lugha na matumizi yake, wahusika, maudhui, ploti, sentensi na mpangilio wake, rangi na michoro miongoni mwa vipengele vingine. Vipengele hivi ni muhimu sana katika kufanikisha marekebisho ambayo yatafanyiwa matini chasili ili kuibuka na matini lengwa itakayowafaa watoto wanaolengwa.

Utafiti huu basi umelenga kuchanganua mbinu za usimilishwaji na kuhakiki baadhi ya vitabu vilivyosimilishwa ili kuchunguza kama mbinu hizi za usimilishwaji zilizingatiwa katika usimilishwaji wa vitabu hivi.

### 1.1 Mada ya Utafiti

Mwandishi yeyote yule hana budi kuzingatia mbinu zifaazo za usimilishwaji iwapo anatarajia kuibuka na kazi ya kiwango cha juu na iliyofanikiwa katika kuwafaa waliolengwa. Mbinu hizi ndizo uti wa mgongo wa kufanikisha usimilishwaji wowote ule. Utafiti huu umehakiki mikakati na mbinu muhimu za usimilishwaji ambazo zimeweza kuwapa waandishi mwaga zaidi wanaposimilisha kazi kwa minajili ya watoto. Ili kufikia lengo hili, utafiti huu umehakiki vitabu vitatu vya

watoto vilivyosimilishwa ili kuchunguza kama mbinu hizi za usimilishwaji zilitiliwa maanani wakati wa kuvisimilisha vitabu hivyo. Pia, utafiti huu umeonyesha ni kwa kiwango kipi hizi mbinu ziliweza kufaulisha usimilishwaji wa vitabu hivi. Vitabu hivi ni: *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001), *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Johnson, 1981) na *Alfu Lela Ulela* (kitabu cha pili) (Brenn, 1962). Kuna vitabu vinne vya hadithi za *Alfu Lela Ulela*. Mtafiti amekichagua kitabu cha pili kwa sababu kina upekee wake. Kitabu hiki kimeisimulia hadithi ya *'Sindbad Baharia'* na iliyochangamano kwa ukamilifu kikilinganishwa na vitabu vingine vitatu ambavyo havisimulii hadithi zilizochangamano kwa ukamilifu kama huu. Mtafiti amevitumia vitabu vifuatavyo kama matini chasili: Utendi wa Fumo Liyongo katika Kusanyiko la Mashairi (Jahadhmy, 1975), King Solomon's Mine (Haggard, 1885) na Arabian Nights' Entertainment (Stanley, 1937). Vitabu hivi vimechaguliwa kwa sababu vinaonyesha uwiano wa kiwango cha juu na matini lengwa.

Kulingana na Tucker (1981), watoto wa kuazia umri wa miaka kumi kuendelea hufurahia kusoma hadithi za kijasiri na zilizochangamano kidogo kwani zitawapa changamoto ya kuzisoma na kuzielewa. Kwa hivyo, kule kusimulia hadithi ya *'Sindbad Baharia'* ambayo inavimelea vya hadithi saba ndani yake kwa ukamilifu kumeifanya kuwa changamano kidogo. Imekuwa ni hadithi ndani ya hadithi na kwa hivyo kuwapa watoto changamoto ya kuhusisha matukio ya kila hadithi ndogo na hadithi kuu. Pia hadithi hii imejaa matukio ya kijasiri yenye kuvutia na kupendeza sana, jambo ambalo limepelekea mtafiti kukichagua kitabu cha pili

cha *Alfu Lela Ulela.* Pia kitabu cha *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Johnson, 1981) kilichosimilishwa kutoka kwa *King Solomon's Mines* (Haggard, 1885) kimeshughulikiwa. Vitabu hivi vimechaguliwa kwa sababu vimejikita katika sehemu tatu muhimu katika fasihi ya watoto na ambazo ndizo zimefanyiwa usimilishwaji kwa upana zaidi. Hizi sehemu ni ushairi (Matundura, 2001), hadithi hasa ngano za kubuni (Brenn, 1962) na riwaya (Johnson, 1981). Aidha, Kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001) na *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Johnson, 1981) ni baadhi ya vitabu ambavyo vimependekezwa kusomwa katika shule za msingi na wakuza mitaala wa K.I.E. Wamependekeza vitabu hivi visomwe na watoto wa darasa la saba na la nane.

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

1 Je, usimilishwaji huongozwa na mbinu gani?

2 Je, mbinu hizi zilifuatwa katika usimilishwaji wa kazi zilizoteuliwa?

3 Ikiwa mbinu hizi zilifuatwa, ziliweza kufanikisha kazi hizi au la?

4 Ikiwa mbinu hizi hazikufuatwa, kazi hizi zilipungukiwa vipi?

## 1.2 Malengo ya Utafiti

1 Kuainisha na kuchanganua mbinu za usimilishwaji katika kazi za watoto.

2 Kuchunguza kama mbinu za usimilishwaji huzingatiwa wakati kazi za Watoto zinaposimilishwa.

3 Kuchunguza mafanikio na udhaifu wa usimilishwaji wa kazi zilizoteuliwa.

## 1.3 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti mwingi umefanywa kuhusu fasihi ya watoto hasa katika lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na fasihi ya watoto katika lugha ya Kiswahili. Utafiti juu ya ukuaji na ueneaji wa fasihi ya watoto umefanywa na baadhi ya wasomi kama vile Mpesha (1995). Baadhi ya wasomi wengine kama vile Akoleit (1990) na Weche (2000) wamefanya utafiti juu ya vitabu vinavyosomwa na watoto kwa jumla. Wengine kama Alembi (1991) na Okhoba (1995) wameshughulikia ushairi wa watoto. Licha ya kwamba kazi za usimilishwaji zina historia ndefu (rej. uk.13) na zinazidi kuongezeka na kuchukua nafasi kubwa katika fasihi ya watoto, kwa ujuzi wa mtafiti hakuna utafiti wowote ambao umefanywa kuhusu swala la usimilishwaji. Utafiti huu unanuia kuuziba huu mwanya kwa kushughulikia swala la usimilishwaji katika fasihi ya watoto.

Aidha, usimilishwaji kama sehemu mojawapo ya fasihi ya watoto hukua na huathiriwa na wakati. Kama wanavyopendekeza Mwanzi (1982) na Akoleit (1990), utafiti wa fasihi ya watoto (ukiwemo usimilishwaji) unapaswa kuendelezwa ili kutambua mabadiliko yanayojitokeza katika fasihi hii na ambayo hutokana na mapisi ya wakati. Vitabu vilivyoteuliwa vilisimilishwa katika vipindi tofauti vya kihistoria na kwa hivyo vitafaa hasa katika kuonyesha picha kamili ya mabadiliko na pia mwelekeo wa usimilishwaji wa fasihi ya watoto unaotokana na mapisi ya wakati.

Kadhalika, usimilishwaji ni muhimu katika fasihi ya watoto kwani unachangia katika kurutubisha fasihi ya watoto kwa kuwapa watoto fursa ya kuzisoma kazi za fasihi za nchi zingine ambazo zimesimilishwa. Kwa hivyo, utafiti huu ni muhimu kwani utawawezesha washikadau wa fasihi ya watoto kukagua ufaafu wa kazi za kigeni zilizosimilishwa kwa watoto wanaolengwa.

Utafiti huu ni muhimu kwa sababu utawapa mwanga zaidi waandishi wanaosimilisha kazi za watoto ili waweze kuboresha kazi zao. Pia utawafaa wakufunzi vyuoni na wanazuoni ambao watashughulikia fasihi ya watoto na kwa hivyo utaweza kuwapa mshawasha wa kuendelea kufanya utafiti kuhusu usimilishwaji wa kazi za watoto. Kwa jumla utafiti huu utachangia katika taaluma ya fasihi ya watoto hasa katika uwanja wa usimiliswaji.

## 1.4 Upeo na Mipaka ya Tasnifu

Ijapo uwanja wa fasihi ya watoto ni mpana mno na umejaa rutuba nyingi ya kufanikisha utafiti huu, utafiti huu utajikita katika sehemu moja ya fasihi hii; usimilishwaji. Hii ni kwa sababu usimilishwaji ni muhimu sana katika fasihi ya watoto na huchangia katika kukuza na kuendeleza fasihi ya watoto. Kwa hivyo ni uwanja unaostahili kufanyiwa utafiti kama ilivyo katika nyanja zingine za fasihi ya watoto. Vile vile, kule kushughulikia usimilishwaji kama sehemu mojawapo ya fasihi ya watoto kutamwezesha mtafiti kuufanya utafiti wa kina zaidi iwezekanavyo.

Utafiti huu umejikita katika viwango vitatu vya usimilishwaji yaani usimilishwaji wa ushairi kuwa riwaya katika *Mkasa wa Shujaa Liyongo.* Usimilishwaji wa hadithi za watu wazima kuwa za watoto katika hadithi za *Alfu Lela Ulela* (kitabu cha pili). Usimilishwaji wa riwaya ya watu wazima kuwa ya watoto katika *Mashimo ya Mfalme Sulemani.* Kwa hivyo, vinampa mtafiti nafasi ya kuangalia viwango vitatu vya usimilishwaji ambavyo ndivyo vimejitokeza sana katika fasihi ya watoto. Matini chasili ya vitabu vyote vitatu haikuwalenga watoto na ili matini hii iwalenge watoto, kuna marekebisho yaliyofanywa kwa minajili ya kuifanya matini lengwa kutimiza mahitaji ya hadhira ya watoto na kuwafaa. Hii ni pamoja na kutafsiriwa na kufupishwa kwa matini chasili, kutumia lugha nyepesi na iliyorahisi kueleweka na watoto na kutumia rangi na michoro katika matini lengwa.

## 1.5 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Elimumitindo (Leech & Short, 1981; Ngara, 1982). Kulingana na Leech na Short (ibid), fasihi haiwezi kuchunguzwa kwa undani bila kuzingatia matumizi ya lugha. Akiungama haya, Mohamed (1995) anasema kuwa nadharia ya Elimumitindo hushughulikia fasihi katika upeo wa lugha kama chombo chake cha kuiundia. Aidha, Bright (1992) na Barnouw (1989) wana maoni sawa kuwa lugha ni chombo muhimu cha kuwasilisha mawazo ya mwandishi kwa msomaji. Msanii hivyo basi hana budi kutumia lugha ambayo itamfaa msomaji anayemlenga hasa anaposimilisha kazi yake.

Kulingana na Ngara (khj), kufaulu kwa mwandishi katika kazi yake hutegemea matumizi yake ya lugha. Kazi yoyote ile ya msanii huwa na vipengele kama vile ploti, maudhui, na wahusika ambavyo hufanikishwa na hupewa umbo lake na lugha. Msanii basi lazima atumie mbinu na sifa za lugha kwa njia ifaayo. Kulingana na Holman (1977), mbinu na sifa hizi huhusisha namna msanii huteua na kutumia maneno, muundo wa sentensi, matumizi ya tamathali za usemi, matumizi ya wizani na urudiaji pamoja na ploti ya kazi yenyewe. Akiendeleza haya Oyoo (2003) anasema kuwa, baadhi ya vipengele kama vile uteuzi wa maneno na matumizi ya tamathali za usemi ni muhimu sana katika kuhakiki mtindo katika vitabu vya watoto kwa sababu vinafanikisha mawasiliano baina ya msanii na msomaji.

Nadharia ya Elimumitindo imetumiwa katika utafiti huu ili kuchunguza jinsi waandishi wa kazi zilizoteuliwa wametumia lugha na kaida zake ili kufanikisha usimilishwaji wa kazi hizi. Uteuzi wa lugha kitamathali huwa na kaida na masharti ya kufuata kama vile umri, uana na kiwango cha elimu cha wanaolengwa. Utafiti huu umetumia mwongozo huu ili kuonyesha namna ufundi huu unavyodhihirika katika usimilishwaji wa kazi zilizoteuliwa.

Ili kuweza kuelewa fasihi vilivyo, msomaji hana budi kwanza kuelewa lugha na hali ya utendakazi wa lugha hii. Katika nadharia ya Elimumitindo, Ngara (1982) ana maoni kuwa, fasihi hutumia lugha ili kumwezesha msanii na msomaji kuwasiliana. Kwa hivyo nadharia ya Elimumitindo huichukulia lugha kama

chombo maalum cha kutoa uamuzi kuhusu kufaulu au kutofaulu kwa kazi ya kifasihi.

Ili kuchanganua kazi ya fasihi kwa kutumia nadharia ya Elimumitindo, sifa za kiisimu za lugha huchanganuliwa huku zikihusishwa na ujumi wa kazi yenyewe. Ujumi wa kazi zilizosimilishwa hujitokeza pale ambapo lugha imetumiwa kwa ufundi ili kuwasilisha ujumbe kwa msomaji. Utafiti huu kwa hivyo utatumia nadharia ya kimtindo ili kuhakiki jinsi lugha imetumiwa ili kufanikisha usimilishwaji wa kazi zilizoteuliwa. Utafiti huu umeongozwa na mihimili ifuatayo;

1 Lugha hufafanuliwa katika kiwango cha sarufi ambapo mtafiti amechunguza aina za sentensi na uhusiano kati ya maana na muundo.

2 Lugha hufafanuliwa katika kiwango cha msamiati. Katika kiwango hiki fani za lugha kama vile tashbihi, istiara, jazanda, na taswira miongoni mwa zingine zimechanganuliwa.

3 Lugha inayotumika iweze kuifaa hadithi yenyewe na yaliyomo katika hadithi hiyo yaweze kueleweka kwa urahisi. Lugha tata huyafanya yaliyomo kutoeleweka kwa urahisi jambo ambalo huenda likamfanya msomaji kupoteza hamu ya kuendelea kukisoma kitabu. Utafiti huu umeshughulikia jinsi lugha imetumiwa ili kuwasilisha yaliyomo (maudhui) katika hadithi kwa njia inayofaa kwa mtoto anayelengwa.

4 Aidha, utafiti huu umeshughulikia kiwango cha maandishi ambapo mambo kama vile chapa, rangi, michoro na umbo la kitabu kwa jumla

yameshughulikiwa kama njia moja ya kuchangia ujumi wa kazi zilizosimilishwa.

## 1.6 Udurusu wa Maandishi

Kwa ujuzi wa mtafiti, hakuna mengi yaliyoandikwa kuhusu swala la usimilishwaji wa fasihi ya watoto. Hata hivyo, kuna baadhi ya waandishi ambao wameligusia jambo hili bila kulijadili kwa kina. Miongoni mwao ni Holindale (1974) na Haviland (1973) ambao wametaja tu baadhi ya vitabu vilivyoandikiwa watu wazima kisha vikawavutia watoto ambao walivisoma hivi vitabu jambo ambalo lilipelekea kusimilishwa kwa vitabu hivyo. Baadhi ya vitabu hivi ni *Robinson Crusoe* na *Gulliver's Travels.* Hata hivyo hawakushughulika kuonyesha namna hivi vitabu vilisimilishwa.

Gachukia na Akivaga (1978) na Odaga (1985) wameangalia kwa jumla fasihi ya watoto nchini Kenya. Wamelizungumzia swala la usimilishwaji kwa njia finyu tu. Ingawa kazi zao zinalenga kuonyesha jinsi kazi za Wazungu zilimwathiri Mwafrika kimawazo, mawazo yao yameufaa utafiti huu kuhusu asili ya usimilishwaji wa kazi za watoto. Utafiti huu umetofautiana na wao kwa sababu hawakujishughulisha na kazi zilizosimilishwa wala mbinu zilizotumiwa kusimilisha kazi hizi, jambo linaloshugulikiwa na mtafiti.

Odaga (1985) ameshugulikia hadithi za kubuni za watoto nchini Kenya. Aliangalia vipindi vitatu vya historia ya fasihi ya watoto; kipindi kabla ya ukoloni, kipindi cha

ukoloni na kipindi cha baada ya ukoloni. Utafiti wake umeufaa utafiti huu kwa sababu amezungumzia masuala mengi kuhusu kazi zilizosimilishwa na wakoloni kama vile *Mashimo ya Mfalme Suleimani* na *Hadithi ya Robinson Kruso*. Hata hivyo, amelizungumzia swala la usimilishwaji kwa njia finyu tu na hakujishughulisha na kazi zilizosimilishwa wala kushughulika na mbinu zilizotumiwa kuzisimilisha kazi hizi. Utafiti huu unatofautiana na wake kwa sababu umeshugulikia mbinu za usimilishwaji na umetumia mbinu hizi kuvihakiki vitabu vilivyosimilishwa, jambo ambalo Odaga (khj) hakushugulikia.

Utafiti kuhusu vitabu vinavyosomwa na watoto umefanywa na Akoleit (1990) na Weche (2000). Weche amevihakiki vitabu vya Alembi. Utafiti wake unahusu jinsi fasihi ya watoto inaweza kuwa kioo cha mtoto cha kumwongoza kitabia. Akoleit amevihakiki vitabu vya Barbara Kimenye ambapo ameshughulikia upokezi wa fasihi ya watoto. Ingawa Weche (khj) na Akoleit (khj) hawakushugulikia vitabu vilivyosimilishwa, tafiti zao zitaufaa utafiti huu hasa katika upande wa nadharia ya kimtindo ambayo wameitumia katika kazi zao.

Utafiti wa Mpesha (1995) ulioshughulikia ukuaji wa fasihi ya watoto nchini Tanzania umeufaa utafiti huu kwa kuwa umetoa mwelekeo wa jinsi fasihi ya watoto huathiriwa na mapisi ya wakati ikiwemo fasihi iliyosimilishwa. Hata ingawa yeye pia alishughulikia baadhi ya vitabu vilivyosimilishwa na ambavyo husomwa na watoto nchini Tanzania, hakushughulikia swala la usimilishwaji kwa kina kama linavyoshughulikiwa na utafiti huu.

Baadhi ya wasomi wengine ambao kazi zao zimeufaa utafiti huu ni pamoja na Alembi (1991) na Okhoba (1995) ambao wameshughulikia fasihi simulizi ya watoto, utanzu wa ushairi kwa kutumia nadharia ya Elimumitindo. Kazi zao zimeufaa utafiti huu katika upande wa nadharia.

## 1.7 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu umejikita katika njia moja kuu ya utafiti ambayo ni ya maktabani. Mtafiti ameweza kudurusu maandishi yanayohusiana na swala la usimilishwaji na ameweza kuainisha na kufafanua mikakati na mbinu za usimilishwaji. Aidha, mtafiti amesoma kwa undani kazi za matini chasili na zile za matini lengwa kama zilivyoteuliwa na kuzichambua ili aweze kufahamu kwa kina marekebisho ambayo yalifanyiwa matini chasili wakati wa kuisimilisha na ambayo yanadhihirika katika matini lengwa. Pia mtafiti ametalii kazi zingine zinazohusiana na mada ya utafiti huu.

### 1.7.1 Ukusanyaji wa Data

Data ilitolewa katika matini chasili, yaani, *Arabian Nights' Entertainment* (1937), *Utendi wa Fumo Liyongo* (1975) na *King Solomon's Mines* (1885) na pia matini lengwa, yaani, *Alfu Lela Ulela* (1962), *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) na *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (1981). Katika kusoma vitabu vya matini zote mbili; chasili na lengwa, mtafiti ameweza kubainisha marekebisho ambayo yamefanyiwa matini chasili na ambayo yanajitokeza katika matini lengwa. Baadhi

ya mabadiliko haya yamedhihirika katika lugha, wahusika, maudhui, ploti na umbo la kitabu.

### 1.7.2 Uchanganuzi wa Data.

Mikakati na mbinu za usimilishwaji zimeainishwa na kufafanuliwa. Data kutoka katika matini chasili na matini lengwa zimechambuliwa kulingana na maswala ya utafiti. Kadhalika, mbinu hizi zimetumika kuhakiki kazi zilizoteuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Elimumitindo ili kuafiki malengo ya utafiti. Uhakiki huu umefanywa katika kiwango cha ploti ya hadithi, lugha na matumizi yake, wahusika, maudhui na umbo la kitabu. Utafiti huu umelinganisha na kulinganua usimilishwaji wa kazi zote tatu.

# SURA YA PILI

## MIKAKATI NA MBINU ZA USIMILISHWAJI WA KAZI ZA WATOTO

### 2.0 Utangulizi

Sura inayotangulia imeshughulikia utangulizi wa tasnifu ambapo swala na lengo la utafiti huu limezingatiwa. Sura hii inalenga kuainisha na kuchanganua mikakati na mbinu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto. Mikakati na mbinu za usimilishwaji ni sifa ambazo zinahusishwa na usimilishwaji na ni nguzo kuu za kufanikisha usimilishwaji wa kazi zilizolenga hadhira ya watoto. Baadhi ya mikakati na mbinu ambazo zimejadiliwa katika sura hii ni pamoja na lugha na matumizi yake, ploti ya hadithi, wahusika, maudhui na umbo la kitabu.

Usimilishwaji katika fasihi ya watoto ni ile hali ya kuifanyia matini chasili marekebisho yanayofaa ili kuweza kuibuka na matini lengwa ambayo itaifaa hadhira ya watoto ambao wamelengwa tofauti na wasomaji waliolengwa na matini chasili. Wakiungama haya, Oyoo (2003), Colwell (1980), Haviland (1973), Arbuthnot na Sutherland (1972) wanasema kuwa usimilishwaji wa kazi za watoto ni ile hali ya kuiandika upya na kuisanifu upya kazi ya fasihi kwa kuifanyia marekebisho mapya ili kuifanya isomwe na iwafae watoto wanaolengwa. Kulingana na Collinson (1976), vitabu vya watoto vinastahili kuwa kioo wazi cha maisha. Mwandishi anatakiwa basi kukiangalia kitabu cha watoto kwa jicho au

mtazamo wa mtoto. Yaani, hadithi iwe fupi na iwe na ploti ya moja kwa moja ambayo haitamkanganya mtoto anapoisoma. Hadithi yenyewe iwe na matukio na utendaji mwingi unaowahusisha wahusika na iwe na wahusika ambao mtoto anaweza kujitambulisha nao. Aidha umbo la kitabu liweze kumvutia mtoto hata kabla ya kukisoma kile kitabu. Kadhalika, lugha iwe sahili na yenye kufahamika na kueleweka na mtoto. Hivyo basi, mabadiliko yoyote yatakayofanyiwa matini chasili yanastahili kuwa yenye mtazamo sawa na ule wa mtoto.

Vitabu vingi vilivyosimilishwa mwanzoni ni vile ambavyo viliandikwa na Wazungu kwa minajili ya kusomwa na Wazungu wenyewe. Hata hivyo baadhi ya matukio katika vitabu hivi yaliweza kuwavutia watoto wao, jambo ambalo lilipelekea kusimilishwa kwa baadhi ya vitabu hivi kama vile *Mashimo ya Mfalme Sulemani.* Hivi ndivyo baadhi ya vitabu vilivyosimilishwa na Wazungu ili viwalenge na visomwe na watoto wa Kiafrika.

Mwandishi hata hivyo ana uhuru wa kukichagua na kukisimilisha kitabu hata kama hakikusomwa na watoto wenyewe mradi tu kiwe na matukio na mafunzo ambayo yanaweza kuwavutia na kuwafaa watoto. Jambo hili hutokea pale ambapo kitabu chenyewe ni kigumu kwa mtoto kukisoma na kukielewa. Kwa mfano, si rahisi mtoto kuzisoma na kuzielewa tendi kama vile *Utendi wa Mwanakupona* na *Utendi wa Fumo Liyongo* kwa sababu ya ile lugha ambayo imetumika. Mwandishi basi ana uhuru wa kuzisimilisha tendi hizi hata kama hazikusomwa na watoto mradi tu ziwafae watoto wanaolengwa kama vile



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

walivyofanya King'ei (2000) ambaye ameusimilisha *Utenzi wa Mwanakupona* na Matundura (2001) ambaye ameusimilisha *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Usimilishwaji wa kazi za watoto hutilia maanani umri na kiwango cha uelewa na upokezi wa watoto wanaolengwa kwani watoto wa umri tofauti tofauti huipokea fasihi yao kwa njia zilizotofautiana. Utafiti huu unashugulikia watoto walio na umri kati ya miaka kumi na kumi na mitano. Hawa ni watoto ambao kwa mujibu wa Tucker (1981) wana uwezo wa kufikiria kidhahania, wanafikiri na kufikia uamuzi wa kimantiki na wana uwezo wa kuisoma hadithi iliyo na ploti changamano kidogo. Vile vile, uwezo wao wa kumakinika ni wa kiwango cha juu ukilinganishwa na ule wa watoto walio na umri wa chini ya miaka kumi. Kwa mujibu wa Oyoo (2003), watoto hawa wana uwezo wa kuzisoma hadithi zilizo na urefu wa takribani maneno elfu mbili.

Ili mwandishi aweze kufaulu katika kazi yake ya kusimilisha, itambidi afanyie marekebisho vipengele kama vile wahusika, maandishi ya chapa, mtindo, ploti, maudhui miongoni mwa vipengele vingine. Kwa mujibu wa nadharia ya Elimumitindo lugha na matumizi yake hutiliwa maanani katika kazi yoyote ile ya fasihi kwani lugha kama chombo cha mawasiliano ndiyo hufanikisha uelewa wa kazi ya fasihi. Hata hivyo, lugha pekee haiwezi kutumika kufanikisha usimilishwaji katika fasihi ya watoto. Matumizi ya lugha hujitokeza katika vipengele vingine kama vile wahusika, ploti, maudhui na mtindo. Uwiano mzuri wa lugha na vipengele hivi pamoja na umbo la kitabu hufanikisha usimilishwaji wa hadithi

inayompendeza na kumvutia msomaji. Sura hii imeonyesha namna kila kipengele kinaweza kufanyiwa marekebisho ili kufanikisha usimilishwaji katika kazi za watoto.

## 2.1 Ploti

Huu ni mfululizo wa matukio katika hadithi. Kwa mujibu wa Kahigi (1995), ploti nzuri huwa na mpangilio mzuri wa mawazo ambapo sentensi zinatiririka vizuri katika aya, aya zinatiririka vizuri katika matini na kutoka aya ya kwanza hadi ya mwisho kunakuwa na mkufu na utangamano wa mawazo katika matini. Pasipo na mpangilio mzuri wa ploti, mawazo hayasomeki kwa urahisi na hukosa mvuto. Mfululizo huu lazima uwe na mantiki ili mtoto anayelengwa aielewe hadithi kwa urahisi. Kwa mujibu wa Huck (1979), ploti ambayo inahusu sababu na matokeo ni mwafaka zaidi kwa watoto. Anaendelea kusema kuwa, ploti huamua umbo na mtindo wa matukio katika hadithi na bila ploti nzuri, hadithi hupoteza nguvu zake za kumburundisha anayelengwa.

Kunazo aina nyingi za ploti katika fasihi ya watoto. Ploti ya hadithi inayoelezea tukio fulani la kijasiri. Katika hali hii, mhusika mkuu huchukua hatua ya kijasiri kulifanya jambo fulani ambapo anajipata hatarini na mwishowe anaweza kujinasua. Kwa mfano, hadithi za *'Sindbad Baharia'* katika kitabu cha *Alfu Lela Ulela* (1962) ni za kijasiri.

Kuna ploti ya hadithi inayotimiza kusudi fulani. Hadithi za aina hii zinahusu mhusika mkuu ambaye ana lengo fulani analoazimia kulitimiza na jinsi ambavyo mhusika huyu anafaulu kulifikia lengo lake. Mfano wa hadithi kama hii ni *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (1981) ambapo Bw. Henry na wenzake wanaazimia kwenda kumtafuta ndugu yake aliyekuwa amepotea na mwishowe wanampata baada ya kusafiri safari yao ndefu na yenye matatizo mengi.

Kuna ploti za hadithi zinazohusu mtu kujitambua na kujirekebisha. Kwa mfano, mhusika mvivu anaweza kutambua kuwa uvivu wake umemletea hasara nyingi na hivyo basi akaamua kubadilisha tabia yake na kuwa mtu mwenye bidii maishani.

Kuna ploti ya hadithi inayohusu kufanya uamuzi ambapo mhusika mkuu anakabiliwa na mambo mawili yanayokinzana na inambidi afanye uamuzi wa kuchagua kati ya mambo hayo mawili. Kwa mfano, mhusika Moni katika kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (2001) ambaye alikuwa afanye uamuzi kati ya kumuua babake na apate mali nyingi au asimuue babake naye aikose ile mali aliyokuwa ameahidiwa.

Mwandishi ana uhuru wa kubadilisha ploti ya matini chasili na kutumia ploti yoyote ile ambayo itakuwa ya ufaafu zaidi kwa watoto anaowalenga. Kulingana na McDowell (1976), fasihi ya watoto huwa na ploti yenye vipengele maalum ambavyo kwa kiasi fulani hutofautiana na ploti ya fasihi ya watu wazima.

Anasema kuwa ploti katika fasihi ya watoto inahitaji kuwa fupi, ya moja kwa moja na izue mgogoro ambao lazima usuluhishwe mwishoni mwa hadithi. Kwa mujibu wa Tucker (1981), ploti za kazi za watoto zanitakiwa kuwa fupi na wazi kwa sababu uwezo wa mtoto wa kumakinika na kuwaza kimantiki ni finyu. Hii hutokana na sababu kuwa mtoto angali anakua kiakili.

Wakati mwingine ploti inaweza kuwa na vimelea vya ploti ambavyo hata vikiwepo, havitakwamiza mtiririko wa ploti. Akiyaungama haya, Weche (2000) anasema kuwa ploti katika fasihi ya watoto huwa na mpangilio bayana wa moja kwa moja ikilinganishwa na ile ya fasihi ya watu wazima ambayo huwa ni tata kuifuata kwa sababu ya matumizi ya mbinu rejeshi ambayo inaifanya hadithi isiwe na mfululizo wa moja kwa moja wa matukio.

Katika kuzisimilisha kazi za waoto, mwandishi anafaa aisimilishe ploti ya hadithi kwa njia ambayo itaifanya ile ploti kuwa sahili na ya moja kwa moja ambapo visa vinapangwa kimoja baada ya kingine tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Ploti inafaa ianzie kwa utangulizi ukifuatwa na kiini cha hadithi kisha mwisho wa hadithi. Matukio yawe na mfululizo jambo ambalo linamfanya mtoto aweze kufuata matukio ya hadithi tangu mwanzo hadi mwisho.

Utangulizi wa hadithi ni jambo muhimu kwani ndio huamua kama mtoto ataendelea kuisoma hadithi hiyo au la. Watoto watafurahia hadithi ambazo zina utangulizi mfupi na unaovutia na kupendeza. Vile vile, mwisho wa hadithi ni

muhimu sana kwa mtoto. Akimnukuu Piaget, Oyoo (2003) anaelezea kuwa watoto hutazama ulimwengu wao kama unaofuata sheria fulani za uadilifu hivi kwamba matendo mazuri hutuzwa ilhali yale mabaya huadhibiwa ili kuyatosheleza matamanio ya mtoto. Ni jukumu la mwandishi kupangua ploti ya matini chasili na kuipanga upya ili kuondoa utata wowote unaoweza kumtatiza mtoto anayelengwa. Iwapo mbinu rejeshi imetumika katika ploti ya matini chasili, mwandishi anafaa azipange upya sura hizo ili matukio ya hadithi yafuatane vizuri bila matumizi ya mbinu rejeshi. Vile vile mwandishi aisimilishe kazi yake kwa kuipa utangulizi na mwisho unaofaa kwa hadhira ya watoto anayoilenga. Ni wajibu wa mwandishi kuusuluhisha mgogoro aliouzua katika hadithi kwa njia ambayo itatosheleza matumaini ya mtoto pale ambapo wema unatuzwa na uovu unaadhibiwa.

Mwandishi ana uhuru wa kuondoa baadhi ya sura ambazo ni changamano na si rahisi kueleweka na mtoto anayelengwa na ambazo ukosefu wake hautakuwa na madhara yoyote katika kiini na ploti ya matini lengwa. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), udondoshi wa matukio ni sifa mojawapo ya msuko ambapo baadhi ya sehemu fulani za hadithi ambazo sio muhimu huachwa. Anaendelea kusema kuwa, mwandishi ana uhuru wa kuyaacha baadhi ya matukio ambayo kuwepo kwake hakuna mchango mkubwa katika msuko wa kazi yenyewe. Udondoshi huu hufanywa ili kufupisha ploti ya hadithi na hivyo kutomchosha mtoto na kumfanya akifuatilize kisa. Ploti katika fasihi ya watoto huwa fupi na iliyojaa matukio ambayo yataweza kumvutia mtoto kwa kuijenga taharuki. Matumizi ya taharuki

katika fasihi ya watoto ni muhimu kwani humpa mtoto motisha wa kukisoma na kumakinikia kile kitabu tangu mwanzo hadi mwisho bila kuchoshwa na hadithi.

Kwa hivyo, mwandishi anaposimilisha kazi yake, anatakiwa kufupisha matini chasili ili ahakikishe kuwa urefu wa ploti ya matini lengwa unamfaa mtoto anayelengwa na pia ahakikishe kuwa hakuinyima ile ploti matukio ya kutosha na yanayojenga taharuki kwa mtoto. Mwandishi anafaa kuzua mgogoro katika matini lengwa na hatimaye aonyeshe jinsi mgogoro huo unavyosuluhishwa kufikia mwishoni wa kitabu. Vile vile ahakikishe kuwa yale marekebisho ambayo ameyafanyia ploti yangali yanaiacha ploti ikiwa na uwiano wa karibu na wahusika kwa sababu ploti na wahusika haziwezi kutenganishwa. Wahusika huathiri matukio ya ploti na kwa upande mwingine, wahusika huathiriwa na matukio ya ploti. Mwandishi anaweza kuzua vimelea vya ploti katika hadithi yake kutegemea umri na kiwango cha uelewa wa mtoto anayelengwa. Kilele cha ploti kinafaa kuwa cha juu ili kutimiza matarajio ya mtoto.

Kwa mujibu wa Mpesha (1995), mwandishi ana uhuru wa kuirutubisha ploti ya hadithi kwa kutumia mbinu kama vile mazungumzo baina ya wahusika na kutoa maelezo ya kina kuhusu tukio fulani. Maelezo haya humsaidia mtoto kuwa na taswira akilini kuhusu jambo linaloelezewa na hivyo kuielewa hadithi anayoisoma.

## 2.2 Lugha

Njia mojawapo ya kuweza kuteka akili za watoto katika maandishi ni kule kutumia lugha ambayo ni sahili na ambayo inaeleweka na mtoto mwenyewe. Kwa mujibu wa nadharia ya Elimumitindo, lugha ni chombo muhimu ambacho kinaleta uhusiano wa karibu baina ya mwandishi na hadhira lengwa. Lengo moja kuu la usimilishwaji wa kazi za watoto ni kuirahisisha lugha ya matini chasili kwa niaba ya kuwawezesha watoto kuisoma na kuielewa matini hiyo. Lugha atakayoitumia mwandishi ndiyo inaamua ama kazi yake itasomwa na mtoto anayemlenga au la.

Mwandishi ana uhuru wa kuiumbua na kuiumba upya lugha ya matini chasili ili iweze kumfaa msomaji anayelengwa. Aidha mwandishi anatakiwa atumie lugha ambayo ni sahili na inayoeleweka vizuri. Hii ndiyo sababu inayompelekea mwandishi kutafsiri vitabu anavyovisimilisha kama njia mojawapo ya kuitumia lugha ambayo itaeleweka na mtoto kama ilivyo katika vitabu kama vile *Mashimo Ya Mfalme Suleimani* (1981) na *Mazungumzo Ya Alfu Lela Ulela* (1962).

Kwa mujibu wa Kahigi (1995), lugha ifaayo katika kazi za watoto ni ile iliyolingana na uelewa wa mtoto anayelengwa kiakili na kielimu. Katika kiwango cha msamiati, mtoto aliye na umri wa kati ya miaka kumi na miaka kumi na mitano huwa tayari anaweza kuufahamu msamiati wa kidhahania. Ni muhimu msamiati huu uhusishwe na watu, matendo na hali inayofahamika na inayomzingira mtoto ili mwandishi ajiepushe na msamiati mzito ulio na dhana

zisizoeleweka kwa urahisi. Kadhalika, ni wajibu wa mwandishi kutumia Kiswahili ambacho kitaeleweka na mtoto na asitumie lahaja ambayo huenda ikakwamiza uelewa wa mtoto.

Katika kiwango cha sarufi, mwandishi anapaswa kujiepusha na sentensi zisizo sahihi kisarufi. Ni wajibu wa mwandishi kurekebisha sentensi ambazo zimeendelezwa vibaya kisarufi katika matini chasili. Mwandishi anayesimilisha kazi za watoto anatakiwa awe mweledi wa sarufi ya lugha ya Kiswahili ili kuifanikisha shughuli ya usimilishaji. Fauka ya haya, mwandishi anatakiwa ajiepushe na sentensi ndefu na ambazo huwa ngumu kueleweka na watoto. Badala yake, anatakiwa atumie sentensi fupi na ambazo kulingana na Njogu na Chimerah (1999) huisukuma hadithi mbele huku zikimpa msomaji hamu ya kutaka kusoma ili aweze kufahamu yatakayotokea. Kulingana na wakuza mitaala wa K.I.E. (1992), sentensi fupi husomeka kwa urahisi, hueleweka na mtoto na hujenga taharuki ya msomaji.

Matumizi zaidi ya lugha hujitokeza katika matumizi ya tamathali za usemi za lugha. Kwa mujibu wa Kahigi (khj), tamathali kama vile: tashhisi, tashbiha, tanakali za sauti na chuku zinaweza kutumiwa katika fasihi ya watoto kwani zinasaidia katika kukuza ubunifu wa mtoto. Hata hivyo, mtoto ataelewa tashbiha na tashhisi iwapo anafahamu kinachozungumziwa na kifananishi chake. Akiungama haya, Mpesha (1995) anasema kuwa tamathali kama vile matumizi ya mbinu za uashiriaji zinaweza kutumiwa katika usimilishwaji. Kwa mfano,

mawingu meusi huashiria mvua ilhali giza huashiria usiku. Mbinu hii huwapendeza zaidi watoto wa umri wa miaka kumi na zaidi kuliko wale walio na umri chini ya huu.

Mbinu ya maelezo ambapo mwandishi anatoa maelezo yanayohusu jambo au tukio fulani kwa kutumia lugha inayoeleweka inaweza kutumiwa. Maelezo yanayojitokeza vizuri humsaidia mtoto kuwa na picha akilini mwake kuhusu kinachoelezewa.

Mwandishi anaweza akatumia mbinu ya nyimbo kuondoa uchovu wa kuisoma hadithi mfululizo na pia kuendeleza hadithi yenyewe. Kwa kutumia lugha inayovutia, nyimbo humpendeza mtoto na humpa hamu ya kutaka kuendelea kuisoma ile hadithi. Aidha, nyimbo kwa mujibu wa Alembi (1991), huwashirikisha watoto katika kuziimba huku wakati mwingine wakiziambatanisha na vitendo na miondoko maalum. Jambo hili huwapendeza watoto mno na pia, huinua kiwango cha ubunifu wao.

Kwa mujibu wa Kahigi (1995), mbinu ya urudufishaji ikitumiwa katika kazi za watoto humwezesha mtoto kumakinikia hadithi. Mbinu hii humwezesha mwandishi kuunda neno ambalo ni maradufu ya lile la kwanza na lililo na maana tofauti na lile la kwanza kwa kurudia neno au shina la neno. Mwandishi ana uhuru wa kutumia tamathali za usemi mradi tu zinaambatana na uelewa wa mtoto anayelengwa.

Mwandishi anaposimilisha kazi yake hana budi kutilia maanani ukweli kuwa lugha hukua na hubadilika kutokana na mapisi ya wakati. Kwa maoni yao Williams na Gannon (1991), kukua na kubadilika kwa lugha ndiko kumeifanya lugha ya Shakespear kuwa ngumu kueleweka na msomaji wa kisasa. Baadhi ya msamiati alioutumia Shakespear hautumiki siku hizi au kama unatumika, una maana tofauti kabisa. Hii ndiyo maana Williams na Gannon (1991) walikisimilisha kitabu cha *Romeo and Juliet* wakiwa na nia ya kuirahisisha lugha aliyoitumia Shakespear. Hivi ndivyo ilivyo katika lugha ya Kiswahili ambayo hukua na hubadilika kutokana na mapisi ya wakati. Hapo awali, maandishi mengi yalihifadhiwa katika lahaja ya Kiamu. Baada ya kuundwa kwa chama cha *Inter-Territorial Swahili Committee* ambacho kilikabidhiwa jukumu la kuisanifisha lahaja moja ili itumiwe kama lahaja rasmi kiusomi, lahaja ya Kiunguja iliteuliwa, ikasanifishwa na mpaka sasa ndiyo inatumika katika shughuli za kiusomi.

Mwandishi basi ana wajibu wa kuisimilisha lugha katika matini lengwa ili iambatane na lugha pokezi inayotumika kwa wakati wake. Si hayo tu, ni muhimu lugha inayotumika na mwandishi iwe wazi na yenye ukweli wa kuaminika na mtoto. Akisisitiza umuhimu wa jambo hili, Collinson (1976:37) anasema,

> Mwandishi atilie maanani kuwa watoto wako katika hali yao ya kukua kihisia, kimawazo na kilugha na kwa hivyo atumie lugha ambayo itaweza kukirimu mambo haya. (Tafsiri yangu)

Kwa mujibu wa Fox (1976), sifa moja kuu ya lugha ni kuwa na uwezo wa kuvutia msomaji. Mwandishi hivyo basi hana budi kuitumia lugha kwa ustadi ili iweze

kueleweka na kumvutia mtoto anayelenga. Lugha kama hii itaweza kumpa mtoto azma ya kuisoma hadithi ilhali lugha isiyoeleweka hutinga ile hamu ya kutaka kuendelea kuisoma ile hadithi.

Mwandishi kwa hivyo ana uhuru wa kuifanyia marekebisho ile lugha iliyotumika katika matini chasili kwa kuitafsiri na kuifanya iambatane na lugha pokezi, kuirahisisha na pia kutumia tamathali za usemi zinazofaa ili kuifanya iwe faafu na yenye kuvutia mtoto anayelengwa.

## 2.3 Wahusika

Wahusika ni viumbe ambao mwandishi hutumia ili kuifanikisha kazi yake. Wanaweza kuwa ni viumbe wanyama au binadamu. Usimilishwaji wa wahusika kwa minajili ya kuwafaa watoto ni jambo muhimu sana. Hii ni kwa sababu kazi zinazowalenga watu wazima hutumia wahusika ambao ni watu wazima na ambao wanaweza kuwa na sifa na tabia ambazo si rahisi mtoto kuzielewa. Pia wahusika hawa huenda wakawa wamepewa majukumu ambayo si rahisi kueleweka na kuaminika na mtoto. Sifa moja kuu ya fasihi ya watoto kulingana na McDowell (1976) ni kule kutumia wahusika ambao ni watoto, huku mhusika mkuu akiwa ni mtoto.

Watoto mara nyingi hufurahia wahusika ambao wanaweza kuwaamini, kujitambulisha na kujinasibisha nao. Kwa hivyo, vitabu vya watoto vinafaa kuwa na wahusika ambao ni watoto. Kulingana na Mpesha (1995), watoto wana uwezo

wa kujinasibisha na wahusika ambao ni watoto na ambao wanapitia tajriba mbalimbali za maisha kama vile furaha, huzuni, mateso na hata mafanikio. Watoto wanafurahia hadithi ambayo mhusika mkuu ni mtoto. Akiyaungama haya, Tucker (1976) anasema kuwa, wazazi na watu wazima mara nyingi huondolewa katika hadithi za watoto kimakusudi ili kuwapa watoto nafasi ya kuifurahia hadithi yao isiyotawaliwa na watu wazima. Iwapo watajitokeza, ni kwa njia finyu tu kiasi kuwa sehemu kubwa ya hadithi huendelezwa na wahusika ambao ni watoto. Anaendelea kusema kuwa, watoto watafurahia kuisoma hadithi ambayo idadi kubwa ya wahusika ni watoto kuliko pale ambapo idadi kubwa ni ya watu wazima. Anasema (1976:181-182):

> Watoto hawafurahii kusoma kuhusu wazazi na watu wazima katika vitabu vyao. Hii labda ni kutokana na sababu kuwa kupitia ile hadithi ya kubuni ambapo wahusika ni watoto, mtoto anapata fursa ya kufurahia na kujifunza majukumu tofauti tofauti ambayo yamepewa mhusika ambaye ni mtoto na ambayo labda kama mhusika angekuwa mzazi au mtu mzima, mtoto angenyimwa nafasi ya kuyaendeleza.
> (Tafsiri yangu)

Hata hivyo, watoto wanaweza kuwafurahia wahusika ambao ni watu wazima katika kazi zao mradi tu mwandishi amewasawiri wahusika hawa kwa njia wanayoeleweka na kuaminika na mtoto. Kwa mfano, mwandishi anaweza kuwapa wahusika hawa majukumu yanayotengewa watu wazima na jamii. Baadhi ya majukumu haya ni, jukumu la kuwa kiongozi kama vile mfalme au kuibeba na kuilea mimba. Pia, watoto hawatasita kuwakubali wahusika ambao ni watu wazima iwapo wamepewa majukumu ambayo mtoto hangependa kuhusishwa nayo. Baadhi ya majukumu haya ni kama vile jukumu la kupunga

pepo analopewa mhusika mchawi katika hadithi. Ni muhimu kufahamu kuwa, iwapo mwandishi ataamua kuwatumia watu wazima kama wahusika katika kazi za watoto, basi inafaa ampe mhusika huyu sifa moja kuu ili mtoto aweze kumwelewa kwa urahisi. Hata hivyo, mwandishi ana uhuru wa kuwatumia au kutowatumia wahusika ambao ni watu wazima katika kazi yake. Akiwatumia, inafaa awafanyie marekebisho yatakayowafaa watoto wanaolengwa.

Mwandishi anatakiwa ajiepushe na wahusika chapwa wasio na uasili katika matini lengwa. Kwa mujibu wa Arbuthnot na Sutherland (1972), wahusika wanatakiwa wawe na msimamo thabiti na wawe wa kuaminika. Wawe na tabia za kuaminika na wakue kwa utaratibu kulingana na umri wao, jinsia , usuli, kabila na hata kiwango chao cha masomo. Siku hizi, watoto wamejikuta katika hali ngumu ya maisha hivi kwamba wanastahili kupewa fasihi ambayo itawapa matumaini na moyo wa kujiamini maishani. Wahusika katika fasihi hupewa sifa zinazowasaidia kutekeleza matendo na mienendo inayoendeleza maudhui ya kazi ya fasihi. Fasihi ya watoto huendeleza maudhui ya uadilifu. Kwa hivyo, wahusika wanaofaa kutumiwa katika kazi za watoto ni wale wenye sifa, tabia na mienendo inayoafiki maudhui haya. Mwandishi hana budi kusimilisha sifa, tabia na mienedo ya wahusika wa matini chasili iwapo tabia na mienendo yao inakinzana na sifa za uadilifu. Kadhalika, ana uhuru wa kuwaondoa kabisa wahusika kama hawa katika matini lengwa ili ajiepushe na ile hali ya kumkatisha tamaa mtoto anaposoma kuhusu wahusika ambao tabia zao haziwapi matumaini yoyote maishani. Baadhi

ya wahusika hawa ni kama vile walevi, wezi, wauaji, wanaharamu, mama wa kambo, au/na mbakaji wa watoto.

Fauka ya hayo, mwandishi anafaa asimilishe tabia tata na changamano za wahusika ili mtoto aweze kuwaelewa wahusika hawa kwa urahisi. Kwa mujibu wa Matti (2005), tabia za wahusika katika matini zinaweza kueleweka kwa urahisi na pia zinaweza zikawa tata na changamano na huhitaji uchambuzi na uchanganuzi wa msomaji. Kwa vile mtoto hana uwezo ule wa kiusomi wa kuchambua na kuchanganua wahusika, fasihi yao inahitaji kuwa na wahusika ambao ni rahisi kueleweka katika vifungu vya wahusika wabaya na wahusika wema. Vile vile, wanafaa kuwa wahusika wa mraba mmoja.

Ni jukumu la mwandishi kutumia idadi ya wahusika ambao watawafaa watoto anaowalenga katika matini lengwa. Wakati mwingine huenda ikawa wahusika waliotumiwa katika matini chasili ni wengi kiasi cha kuwakanganya watoto. Katika hali kama hii itambidi mwandishi apunguze idadi ya wahusika na ahakikishe kuwa, wale wahusika ambao atawaondoa hawataathiri kiini na ploti ya hadithi yenyewe. Mara nyingi wahusika wadogo na wajenzi ndio huondolewa kwani kuwepo au kutokuwepo kwao hakutaizuia hadithi kukamilika. Kwa upande mwingine, endapo wahusika waliotumiwa katika matini chasili ni wachache mno kiasi cha kutatiza mtiririko wa hadithi na ufaafu wa hadithi hiyo kwa watoto wanaolengwa, mwandishi basi hana budi kuongezea idadi ya wahusika katika

matini lengwa ili kuiwezesha ploti ya hadithi kutiririka na kueleweka na watoto wanaolengwa.

Mwandishi ana uhuru wa kuwapa wahusika katika matini lengwa majina mapya tofauti na yale ya matini chasili. Jambo hili hutokea pale ambapo wahusika wa matini chasili wamepewa majina magumu yasiyoambatana na sarufi ya lugha pokezi na yaliyo na utata kutamkika, kufahamika na kukumbukika. Kwa mfano, majina ya wahusika katika matini chasili ya riwaya ya *Animal Farm* iliyoandikwa na Orwell (1945) yanatatanisha yakilinganishwa na yale ya matini lengwa katika kitabu cha *Shamba la Wanyama* kilichotafsiriwa na Kawegere(1967) ambapo wahusika wamepewa majina ya kimajazi na ambayo yanaambatana na sarufi ya lugha pokezi.

Huku akinukuliwa na Tucker (1976), Piaget anasema kuwa, watoto hawapendi majina ya kidhahania ambayo si rahisi kwao kuyafahamu na kuyatambua. Hii ni kwa sababu watoto, kinyume na watu wazima hawana uwezo wa kufikiria kwa njia ya kuwaza na kuwazua. Kwa hivyo, watafurahia wahusika walio na majina wanayoyaelewa na kuyafahamu moja kwa moja. Hii ndiyo sababu kuwa mwandishi ana uhuru wa kuyasimilisha majina ya wahusika wa matini lengwa kwa sarufi ya lugha pokezi.

## 2.4 Maudhui

Maudhui hutegemea kile ambacho mwandishi alikusudia kukielezea katika hadithi yake. Kwa mujibu wa Huck (1979), maudhui katika fasihi ya watoto yafaa yaendeleze maadili ya kijamii. Maudhui katika fasihi ya watoto yanahitaji kusimilishwa kwa njia ambayo itamfunza mtoto anayelengwa maadili ya kijamii pindi anavyoendelea kukua. Maudhui haya yanaweze kumpa mtoto mwongozo mwema kuhusu mwenendo wa tabia ambao anatarajiwa kuwa nao katika jamii yake. Maudhui haya yanaweza kuwa juu ya jinsi ya kukabiliana na kuushinda woga au wivu, jinsi ya kuukubali ulemavu au mabadiliko ya kimaumbile kama vile kubaleghe na kadhalika. Kwa maoni yake Davies (1975), maudhui katika fasihi ya watoto yanatakiwa kuwa mepesi ili yaweze kueleweka na mtoto anayelengwa. Mwandishi anafaa atumie lugha sahili itakayomwezesha mtoto kuyaelewa maudhui haya. Mwandishi hana budi kuyaepuka maudhui mazito mazito ambayo huenda yakapatikana katika matini chasili. Badala yake, anafaa kuyasimilisha ili yaweze kuwafaa na kuwanufaisha watoto anaowalenga.

## 2.5 Umbo la Kitabu

Umbo la kitabu huegemea sana kwenye uchapishaji kuliko uandishi. Wakati mwingine, mwandishi hana uwezo wa kuamua michoro na rangi ianayostahili kutumika katika kitabu chake. Hata hivyo mchoraji na mchapishaji anafaa atumie rangi zenye kuvutia macho ya mtoto na pia zenye uwiano wa moja kwa moja na matini yenyewe.

KENYATTA UNIVERSITY

Umbo la kitabu ni mkusanyiko wa mambo mbalimbali kama vile vielezo (michoro), maandishi ya chapa na ukubwa wake, aina ya karatasi iliyotumiwa kupigia chapa, jalada la kitabu, rangi iliyotumika na ujalidi wa kitabu ambao ndio hukamilisha umbo la kitabu. Haya ni mambo muhimu sana katika fasihi ya watoto kwa sababu yanasaidia kuongezea ujumi wa lugha na matumizi yake. Ingawa lugha na matumizi yake ni muhimu sana katika fasihi kama ilivyojadiliwa katika nadharia ya Elimumitindo, lugha pekee haiwezi kuwavutia watoto bila kuongezewa uzuri wake na umbo la kitabu. Kwa hivyo utafiti huu umeshughulikia jinsi matumizi ya lugha hujitokeza katika umbo la kitabu. Umbo la kitabu ni muhimu hasa kwa wale watoto wanaopendezwa sana na rangi na michoro. Sura ya kitabu ina uwezo mkubwa sana wa kumvutia mtoto kukisoma kile kitabu au pia ikamfanya akichukie.

### 2.5.1 Vielezo (Michoro)

Michoro ni njia moja ambayo mwandishi hutumia kuwasiliana na wasomaji wake. Kulingana na Oyoo (2003), mwandishi hutumia michoro kama njia ya kuwasilisha maneno yake. Hata hivyo, mwandishi wakati mwingine hana uamuzi wa michoro na rangi ya michoro itakayotumiwa katika matini yake hasa pale ambapo mchoraji ni tofauti na mwandishi. Kwa kuwa michoro ni muhimu katika kazi za watoto kwa vile hutumika kufafanua matini yenyewe, mwandishi na mchoraji hawana budi kushirikiana ili kuibuka na michoro na rangi zinazofaa. Michoro huifanya kazi yenyewe iwavutie wasomaji wanaolengwa na pia huondoa ule ukinaifu wa maandishi ya chapa ambayo wakati mwingine huenda ikamchosha

mtoto anayelengwa. Kadhalika, michoro humsaidia mtoto kuikumbuka ile hadithi. Sababu ni kwamba, michoro hutumiwa kufafanua baadhi ya sehemu za hadithi.

Ni muhimu kujumuisha michoro katika kazi za watoto kwa sababu inawasaidia watoto walio na uelewa wa kiwango cha chini kuielewa hadithi inayohusika. Ikiwa mchoraji ataongezea michoro katika matini, michoro hiyo inafaa kuwa na uwiano wa moja kwa moja na hadithi yenyewe kwa sababu ule uwiano ukikosa, basi michoro hiyo huishia kumkanganya mtoto.

Kwa mujibu wa Cass (1967), michoro iliyotiwa rangi huwavutia watoto kuliko ile ambayo haijatiwa rangi. Cass (khj) anapendekeza matumizi ya rangi ambazo huwavutia watoto miongoni mwake pakiwemo rangi nyekundu, ya majano, ya samawati na kijani kibichi. Hata hivyo, Cass (khj) anaonya kuwa matumizi mabaya ya rangi hizi huenda yakawaudhi na kuwachukiza watoto. Mchoraji hivyo basi anafaa awe mwangalifu anapoitia michoro rangi. Ahakikishe kuwa ameitia ile rangi vizuri bila kuiachilia itapakae ovyo katika michoro yake. Iwapo michoro itakuwa na rangi zaidi ya moja, mchoraji anafaa azichanganye zile rangi kwa uangalifu sana ili matokeo yake yaweze kuyavutia macho. Aidha, ni muhimu rangi ya michoro iwe na uwiano na michoro yenyewe.

Akishadidi haya Cass (khj) anaelezea kuwa, watoto wana tabia ya kuhusisha rangi fulani na vitu fulani. Kwa mfano, damu inahusishwa na rangi nyekundu ilhali matunda yaliyoiva huhusishwa na rangi ya majano. Pasipo na uwiano wa

rangi na michoro, michoro hiyo huishia kumkanganya mtoto jambo ambalo lafaa liepukwe. Iwapo michoro imetumika katika matini chasili, mwandishi ana uhuru wa kuifanyia michoro hiyo marekebisho ya rangi katika matini lengwa. Pia, ana uhuru wa kuongezea au kupunguza idadi ya michoro katika matini lengwa.

Hata hivyo, Akoleit (1990) anasema kuwa, watoto walio kati ya umri wa miaka kumi hadi kumi na mitano hawatilii vielezo maanani sana wakilinganishwa na watoto wa umri wa chini ya miaka kumi. Kwao hadithi yenyewe huwavutia kuliko vielezo mradi hadithi yenyewe iwe na matukio ya kutosha na yanayosisimua. Hii ndiyo sababu vitabu vya kale kama vile *Alfu Lela Ulela* vimeendelea kuwavutia watoto hata ingawa vielezo vilivyotumika havina mvuto mkubwa kwa watoto.

### 2.5.2 Jalada la Kitabu

Jalada la kitabu linahusisha umbile la jalada lililotumiwa, mchoro na rangi ya mchoro wa jalada pamoja na anwani ya kitabu. Baadhi ya vitabu vya kale huwa na majalada yaliyochakaa na yaliyo na rangi isiyovutia macho ya msomaji. Ni rahisi kitabu kama hicho kukataliwa na watoto hata kikiwa kina hadithi inayovutia na lugha iliyorahisi kueleweka. Kwa hivyo mwadishi ana uhuru wa kubadilisha rangi ya jalada la kitabu ili aweze kutumia rangi inayovutia macho. Rangi ya jalada yatakiwa iwe angavu na mchoro wenyewe uweze kuonekana wazi wazi.

### 2.5.2.1 Anwani ya Kitabu

Anwani ya kitabu ni muhimu kwani inaweza kumvutia ama kumchukiza msomaji. Watoto hupendezwa na anwani ambayo inaeleweka vizuri bila kutatanisha. Anwani fupi ni mwafaka zaidi. Wakati mwingine, mwandishi anaweza akatumia anwani isiyo wazi. Iwapo ataamua kutumia anwani kama hii, basi anafaa aiandike kwa njia ambayo itajenga taharuki kwa mtoto ili awe na ile azma ya kukisoma kile kitabu na pia kuambatana na kiwango cha uelewa wa mtoto anayelengwa. Mwandishi ana uhuru wa kuiumbua anwani ya matini chasili na kuiandika upya kwa minajili ya kuifanya iwafae watoto wanaolengwa.

### 2.5.2.2 Maandishi ya Chapa

Maandishi ya chapa yanatakiwa kuwa makubwa na yanayosomeka bila kuyafanya macho ya mtoto yakazike. Yakiwa madogo sana, huenda yakamtatiza mtoto kuyasoma na hivyo kumchokesha kiasi kuwa huenda akakichukia kile kitabu. Mwandishi anafaa aache nafasi za kutosha katika pembe zote za ukurasa hasa upande ambao ujalidi wa kitabu utafanyiwa ili maandishi yasije yakaingiliwa na ujalidi wa kitabu na kumfanya mtoto atatizike kuyasoma.

### 2.5.2.3 Umbo la Nje la Kitabu

Mwandishi anaweza kukipa kitabu umbo jipya. Hili ni jambo ambalo halijazoeleka nchini mwetu kwa kuwa watoto wamezoea kuvisoma vitabu vilivyo na umbo la mstatili au mraba. Watoto hupendezwa na maumbo mbalimbali na huenda vitabu vilivyotofautiana kimaumbo vikawapendeza pia. Aidha, kitabu kizuri cha watoto



KENYATTA

kulingana na Cass (1967) ni kile ambacho kina jalada imara na lisilochakaa kwa haraka kutokana na kushikwashikwa na watoto wanapokisoma. Ujalidi wa kitabu pia watakiwa kuwa imara ili kukizuia kitabu kuharibika haraka kutokana na kukazika kwake kinaposomwa na watoto na wakati huo huo, ufanywe kwa njia ambayo utakiwezesha kitabu kufunguka wazi.

## 2.6 Hitimisho

Mwandishi huisimilisha kazi ili kuipa uwazi na uangavu utakaowafaa wasomaji wanaolengwa. Kulingana na Wamitila (2002), uwazi na uangavu wa kazi ya fasihi hutegemea maudhui ya kazi hiyo, uteuzi wa lugha, msamiati na msomaji wa kazi inayohusika. Ni muhimu mwandishi awe na uwezo wa kuisimilisha kazi yake kwa namna ambayo itawachangamsha watoto. Anapaswa kuwa na ubunifu wa kiwango cha juu ili aweze kuisimilisha kazi yake kwa njia inayofaa na bila kuharibu kiini cha hadithi ya matini chasili. Aidha ni muhimu mwandishi aweze kuyafahamu mahitaji ya watoto anaowalenga kwani watoto wa umri tofauti tofauti huwa na mahitaji yaliyotofautiana. Kwa kufahamu mahitaji ya hadhira yake, ataweza kujua ni mambo gani yanayoipendeza, kuivutia na kuifaa hadhira hiyo. Zaidi ya hayo, ataweza kujua jinsi atakavyosimilisha ploti, lugha, wahusika na maudhui ya matini lengwa. Ni wajibu wa mwandishi kuhakikisha kuwa ameibuka na matini lengwa yenye mvuto na ufaafu kwa watoto anaowalenga.

Sura hii imeainisha mikakati na mbinu ambazo zinatumiwa katika kusimilisha kazi za watoto. Imeelezea jinsi ploti ya hadithi inasimilishwa kwa kudondoa baadhi ya

sehemu za matini chasili na pia kuipangua ile ploti ya matini chasili na kuipanga upya katika matini lengwa ili kuipa mtiririko ulio sahili. Aidha, sura hii imeelezea baadhi ya tamathali za lugha ambazo zinaweza kutumiwa katika kazi za watoto na zile ambazo zinaweza kuepukwa. Kadhalika, msamiati unaofaa kutumiwa katika kazi za watoto umeshughulikiwa. Maudhui ya kazi za watoto yamejadiliwa. Maudhui husimilishwa ili yawe sahili na yamfundishe mtoto kuhusu maadili katika jamii. Sura hii pia imeonyesha wahusika ambao wanafaa kutumiwa katika kazi za watoto na wale ambao wanafaa kuondolewa. Umbo la kitabu vile vile limejadiliwa ambapo michoro na rangi ya michoro imejadiliwa. Pia, jalada la kitabu, anwani na mchoro wa jalada sawa na maandishi ya chapa yamejadiliwa.

Sura ifuatayo itahakiki kitabu cha *Alfu Lela Ulela* cha Brenn (1962) kwa kutumia mikakati na mbinu za usimilishwaji zilizoainishwa na kuchanganuliwa katika sura hii (ya pili).

# SURA YA TATU

## USIMILISHWAJI WA HADITHI ZA *ALFU LELA ULELA*

### 3.0 Utangulizi

Sura hii imehakiki usimilishwaji katika kitabu cha pili cha *Alfu Lela Ulela* ambacho kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Brenn (1928) na kupigwa chapa kwa mara ya kwanza mnamo 1962. Kwa mujibu wa Stanely (1937), anwani hii ina maana ya siku elfu moja na moja. Inaaminika kuwa hadithi hizi na zingine ambazo zimedondolewa zilitambwa kwa siku elfu moja na moja mfululizo ndipo zikaitwa '*Alfu Lela Ulela*'. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), kitabu hiki ni miongoni mwa vitabu vya ngano vilivyotafsiriwa na Wamishenari baada ya majilio ya Wakoloni na vikawa ndivyo msingi wa riwaya ya kisasa.

Ingawa wataalamu wengi wamekichukulia kitabu hiki kama tafsiri, pia kimesimilishwa huku tafsiri ikiwa ni mbinu mojawapo kukisimilisha kutoka lugha ya matini chasili hadi lugha pokezi. Kama kitabu hiki kingekuwa ni tafsiri tu, basi kingewalenga watu wazima wa lugha pokezi wala si watoto. Aidha, kingetafsiriwa kama kitabu kimoja kilicho na mfululizo wa hadithi hizi badala ya kuziandika hadithi hizi katika majuzuu manne mafupi mafupi.

Hadithi hizi kulingana na Wamitila (2002) zina asili yake katika hurafa na migani ya Uarabuni na ziliwalenga watu wazima. Hadithi hizi zinafanana kifani na zina dhamira ya kidini. Chanzo cha hadithi hizi ni bibi mmoja kwa jina Shahrazad bintiye Waziri aliyeolewa na Mfalme Shahriyar. Huyu mfalme alikuwa na tabia za

kuwauwa wake zake usiku wa kwanza baada ya wao kufunga ndoa. Katika juhudi za kuyaokoa maisha yake, Shahrazad alianza kumtambia Mfalme hadithi tangu usiku wa kwanza baada ya wao kufunga ndoa hadi siku ya elfu moja na moja. Kila siku Shahrazad hakumaliza hadithi yake, alimwacha Mfalme katika hali ya taharuki. Hali hii iliokoa maisha ya Shahrazad na ikabadilisha tabia ya mfalme ya kuwauwa wake zake.

Nchini Kenya hadithi hizi ziliweza kusimilishwa na kutafsiriwa na wazungu kwa minajili ya kusomwa na watoto shuleni. Usimilishwaji huu ulifanywa kwa utaratibu bila kupotosha kiini na dhana muhimu za hadithi. Usimilishwaji wa kimsingi kabisa uliofanyiwa hadithi hizi ni kuziingiza katika fasihi andishi ya Kiswahili. Ingawa Brenn (1962) hakuelezea matini chasili aliyoitumia katika kufasiri hadithi hizi, hadithi hizi zinashabihiana sana na za Henry (1937) ambazo zimenakiliwa kwa lugha ya Kiingereza. Utafiti huu umeitumia matini ya Henry (khj) kama matini chasili. Hata hivyo si hadithi zote za matini chasili zinapatikana katika matini lengwa, *Alfu Lela Ulela* (kitabu cha pili).

Kuna majuzuu manne ya *Alfu Lela Ulela*. Utafiti huu umeshughulikia kitabu cha pili cha *Alfu Lela Ulela* kati ya hivyo vinne (taz. uk.9 ambapo sababu za kukichagua kitabu cha pili zimejadiliwa). Kwa mujibu wa nadharia ya Elimumitindo, sura hii imehakiki jinsi mwandishi amefanikiwa au jinsi hakufanikiwa kutumia lugha ili kufanikisha usimilishwaji wa hadithi hizi kwa minajili ya kusomwa na watoto. Sura hii imejadili jinsi mwandishi alivyotumia

lugha ili kufanikisha usimilishwaji wa ploti, uumbaji wa wahusika, umbo la kitabu na pia kuwasilisha maudhui kwa watoto wanaolengwa.

## 3.1 Ploti

Huu ni msuko wa visa na matukio katika hadithi. Kwa mujibu wa nadharia ya kimtindo, mwandishi hutumia lugha kufuma, kuunda na kuunganisha tukio moja na lingine, wazo moja na lingine na sura moja na nyingine. Sehemu hii imehakiki kila hadithi katika matini lengwa.

### 3.1.1 Safari Saba za Sindbad Baharia.

Hii ni hadithi iliyo na hadithi saba ndani yake zinazohusu safari za Sindbad. Msimulizi ni Sindbad mwenyewe.

#### 3.1.1.1 Safari ya Kwanza

Sindbad na wengine wanaondoka kwenda kuchuma mali. Walitia nanga mgongoni mwa nyangumi aliyekuwa ameelea juu ya maji kule baharini huku wakidhani ni kisiwa. Walishuka na kuwasha moto ili wapike. Nyangumi alipohisi joto, alijizamisha majini ghafla. Baadhi ya mabaharia walizama baharini akiwemo Sindbad. Sindbad alichukuliwa na mawimbi hadi kisiwani ambapo alikutana na wachungaji farasi wa mfalme. Wachungaji hawa walimchukua mpaka kwa mfalme wao. Akiwa pale Sindbad alibahatika kukutana tena na wale mabaharia waliokuwa nao safarini. Alipata shehena lake na akauza kisha akarejea nyumbani akiwa na mali nyingi.

#### 3.1.1.2 Safari ya Pili

Sindbad na wenzake wanakwenda kuchuma mali. Walitia nanga katika kisiwa kimoja ili kuchota maji na kujiliwaza. Sindbad alijistarehesha kwa mvinyo kisha akasinzia. Jahazi lilipoondoka, Sindbad aliachwa akiwa amelala. Alipoamka alijipata yu pweke. Alizungukazunguka kule kisiwani bila kufanikiwa kumpata mtu yeyote. Alipiga kambi mahali palipokuwa na yai la ndege mmoja kwa jina Rok. Yule ndege aliporejea jioni hiyo, Sindbad alitumia kilemba chake kujifungia katika mguu wa Rok. Mapambazuko, yule ndege alimbeba Sindbad mpaka kisiwani ambacho kilikuwa na majoka wengi na mawe ya almasi. Sindbad alitumia kilemba chake tena kujifungia kwenye mnofu wa nyama. Tai alipouchukua ule mnofu, Sindbad alinyanyuliwa mpaka kiotani. Aliokolewa na mabaharia waliokuwa wakirusha ile minofu ya nyama. Aliwagawia baadhi ya mawe ya almasi aliyoyachukua kutoka kule kisiwani. Alifanikiwa kuyauza yale mawe ya almasi na kurejea nyumbani akiwa tajiri mkubwa.

#### 3.1.1.3 Safari ya Tatu.

Sindbad anaondoka Baghdadi kwenda kuuza bidhaa zake Basra. Mchafuko wa bahari uliwalazimisha watie nanga katika kisiwa kilichokuwa na vijitu na mazimu wakali waliokuwa wakiwala watu. Baadhi ya mabaharia walikufa maji na wengine wakaliwa na mazimwi. Sindbad na wenzake wawili waliweza kutoroka kutoka katika kisiwa hiki. Walikwenda katika kisiwa kingine ambapo walikutana na joka kubwa. Joka hili liliwala wenzake Sindbad. Sindbad aliponea chupuchupu na hatimaye akaokolewa na mabaharia ambao walikuwa wanaelekea Sahalat.

Kisadfa, mabaharia hawa walikuwa ni wale wenzake waliomwacha akiwa amelala. Hivyo basi, shehena lake lilikuwa lingali pale jahazini. Alilichukua na akauza bidhaa zake na akafanikiwa kuchuma mali nyingi kisha akarejea Baghdadi.

### 3.1.1.4 Safari ya Nne

Sindbad anaondoka kwenda nchi za Ajemi. Walikabiliwa na dhoruba kali iliyosababisha kuzama kwa jahazi lao. Wengi wa mabaharia walikufa maji lakini Sindbad na wenzake wachache walinusurika. Mawimbi yaliwachukua mpaka kisiwani ambacho kilikuwa na watu waliokuwa wanakula watu. Wenzake Sindbad waliliwa lakini yeye akatoroka mpaka pale alipokutana na Wazungu wakichuma pilipili. Wazungu hao walimchukua mpaka kwa mfalme wao. Mfalme alimwoza mwanamke mwenyeji wa kile kisiwa. Siku moja, huyu bibiye Sindbad aliugua na kuaga dunia. Kulingana na sheria za kile kisiwa Sindbad alizikwa akiwa hai pamoja na mkewe katika shimo la maiti, mahali watu walikuwa wakizikwa. Akiwa shimoni aliweza kugundua tundu ambalo lilikuwa limepita chini mpaka pwani ya bahari. Alilifuata lile tundu mpaka pwani akiwa amebeba vitu vya dhamani alivyovipata kutoka shimoni. Pale pwani alibahatika kuwaona mabaharia waliomchukua katika safari zao ambapo aliweza kuuza mali yake kisha akarejea nyumbani akiwa tajiri.

### 3.1.1.5 Safari ya Tano

Sindbad alianza safari pamoja na mabaharia wengine. Walitua katika kisiwa kimoja ambacho hakikuwa na watu. Wenzake waliliona yai la ndege anayeitwa Rok na wakalivunja. Kitendo hiki kiliwaudhi hawa ndege na kuwafanya walipize kisasi kwa kuwashambulia wale mabaharia na kuivunja jahazi yao. Mabaharia wote walizama baharini isipokuwa Sindbad aliyenusurika. Aliweza kuelea juu ya maji kwa kutumia kipande cha ubao hadi kisiwa kingine. Pale kisiwani alitekwa nyara na mzee wa bahari ambaye aliganda shingoni mwake. Kila siku Sindbad alimbeba yule mzee na kumzungusha mle kisiwani ili achume matunda. Siku moja Sindbad alitengeneza mvinyo wa sabibu na kumpa huyu mzee. Alipokunywa alilewa chakari. Hapo hapo, Sindbad alimuua na akaweza kutoroka. Kwa bahati nzuri alipata jahazi na akaliabiri mpaka mjini. Pale mjini Sindbad alinunua bidhaa ambazo aliuza akiwa safarini kurudi Baghdadi. Alirejea Baghdadi akiwa tajiri.

### 3.1.1.6 Safari ya Sita

Sindbad na wenzake walianza safari yao. Walipigwa na dhoruba kali kule baharini. Wenzake Sindbad walikufa kwa njaa huku Sindbad akinusurika. Alitengeneza mtumbwi na kuuweka sawa sawa na mkondo wa mto uliomchukua hadi ukingoni. Pale alichukuliwa na watu weusi mpaka mjini Serendib. Alipelekwa mpaka kwa mfalme ambaye baada ya kusikiliza jinsi Sindbad alifika pale, alimpa Sindbad zawadi za thamani ambazo baadhi yake zilikuwa ni zawadi za Khalifa wa Baghdadi, kisha akamwachilia arudi kwao. Akiwa njiani aliweza kuuza bidhaa

zake na kupata mali nyingi. Alirejea Baghdadi na kumpa Mfalme wa Baghdadi zawadi zake.

#### 3.1.1.7 Safari ya Saba

Hii ndiyo safari ya mwisho ya Sindbad. Khalifa wa Baghdadi alimtuma Sindbad kwa Mfalme wa Serendib. Sindbad alifika Serendib salama na akaanza safari ya kurudi nyumbani. Wakiwa safarini, walitekwa nyara, wakanyang'anywa mali yao na kuuzwa kama watumwa. Sindbad alinunuliwa na mfanyi biashara mmoja ambaye alimpatia kazi ya kuwawinda ndovu. Siku moja akiwa mawindoni, alivamiwa na ndovu na mmoja wao akambeba kwa mgongo mpaka mahala palipokuwa na pembe nyingi. Sindbad alimwendea bwanake na kumpeleka mpaka mahali pale. Bwanake alifurahi sana na kumwachilia Sindbad arudi kwao. Sindbad alichukua pembe nyingi kadri awezavyo katika safari yake ya kurudi nyumbani. Aliziuza kisha akajiunga na msafara wa wafanyi biashara kuelekea Baghdadi. Kule Baghdadi, aliweza kuishi raha mustarehe pamoja na familia yake huku wakisherehekea ufanisi mkubwa wa Sindband.

### 3.1.2 Kisa cha Mbilikimo Mwenye Kinundu.

Hadithi hii inahusu mbilikimo mmoja ambaye alikuwa miongoni mwa watu waliomtumbuiza mfalme. Siku moja alikaa mbele ya duka la mshonaji na akaanza kuimba na kuchezacheza. Mshonaji alimchukua yule Mbilikimo hadi nyumbani kwake ili akamfurahishe mkewe. Jioni walipokuwa wakila chajio, mfupa wa samaki ulimkwama mbilikimo kooni na mara akafa. Kwa kuogopa hukumu kali

ambayo wangeipata kutokana na kifo cha mbilikimo, mshonaji na mkewe walimchukua mbilikimo hadi kwa mganga. Walimwegesha ukutani huku wakidai ati ni mgonjwa kisha wakaondoka. Mganga alipoitwa alitoka mbio na bila kujua akampiga mbilikimo teke akambingiria. Akidhani ndiye amemuua, yeye na mkewe walimchukua yule mbilikimo na kumwegesha ukutani nyumbani kwa jirani yao mwislamu. Mwislamu aliporejea nyumbani alidhania kuwa yule Mbilikimo alikuwa ni mwizi na akampiga mno. Akidhani pigo lake limemuua mbilikimo, alimchukua na kumwegesha kando ya duka moja mjini. Mkristo ambaye alikuwa amelewa chakari alipopita karibu na lile duka, alidhani kuwa mbilikimo alikuwa mwizi na akamshambulia ghafla. Mkristo alikamatwa na akahukumiwa kunyongwa kwa mauaji ya Mbilikimo.

Kabla ya mauaji haya kutekelezwa, mwisilamu, kisha mganga na hatimaye mshonaji walijitokeza na wakakiri makosa yao. Hatimaye hakuna mtu alinyongwa maana hawakupatikana na hatia.

### 3.1.3 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Tano

Kisa hiki kinahusu Alnacha ambaye alitumia pesa zake zote kununua mali ambayo alitarajia kuuza ili apate utajiri. Aliponunua yale mali, alikaa kando ya duka moja na kuliweka kapu lililokuwa na mali mbele yake. kwa bahati mbaya, aliligonga lile kapu teke na mali yake yote yakavunjika. Alipewa msaada wa pesa na bibi mkongwe mmoja. Baadaye kidogo, yule bibi alimchukua Alnacha mpaka nyumbani kwa tajiri wake. Akiwa pale, alipigwa na kunyang'anywa pesa zake

zote. Baada ya kujisikia nafuu, Alnacha alilipiza kisasi kwa kumuua bibi mkongwe pamoja na wenzake huku akijaribu kunyakua mali ya yule tajiri. Baada ya kitendo hiki Alnacha alishtakiwa kwa Kadhi ambaye alimfukuza kutoka kule mjini. Hatimaye aliangukia mikononi mwa wanyang'anyi na akapigwa. Ndugu yake alimchukua na kuishi naye.

### 3.1.4 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Sita

Hadithi hii inahusu Shakabak ambaye pia alikuwa ndugu yake kinyozi. Alikuwa mvivu na mwombaji. Siku moja aliendа kuomba kwa tajiri aliyejulikana kwa jina Bamaside. Bamaside alimchukua na kumtunza vizuri na kumgawia baadhi ya mali yake. Baada ya kifo cha Bamaside, mali yake yote yalichukuliwa na sultani ikiwemo mali iliyokuwa haki ya Shakabak. Shakabak aliondoka huko na akijiunga na msafara wa wasafiri waliokuwa wakienda Makka. Kwa bahati mbaya msafara huu ulishambuliwa na kutekwa nyara na Mabedui na wasafiri. Shakabak alifanywa mtumwa na mmoja wa Mabedui. Alimtesa na kumpiga Shakabak na mwishowe akampeleka na kumwacha kati kati ya jangwa ili afie huko. Hatimaye aliokolewa na ndugu yake ambaye alimchukua na kuishi naye.

Hadithi hizi zina masimulizi ya moja kwa moja. Kila hadithi ina sehemu ya mwanzo, kiini na mwisho wake. Utangulizi wake ni wa moja kwa moja na ni mfupi ukilinganishwa na ule wa matini chasili. Hata hivyo, utangulizi huu hauna raghba kwa watoto wanaolengwa. Watoto mara nyingi huvutika na kile wanachokifahamu. Kwa hivyo, watavutiwa na hadithi ambayo utangulizi wake

una mtindo waliouzoea wa 'paukwa pakawa' au 'hadithi hadithi, hadithi njoo.' Mtafsiri angeifanya hadithi hii ivutie kwa kutumia utangulizi kama huu. Ploti za hadithi hizi zimefupishwa zikilinganishwa na zile za matini chasili. Kulingana na Kirmani na Kirmani (2002), hadithi hizi huwa ndefu na baadhi yake zilichukua siku mbili mfululizo au zaidi kusimuliwa. Huu urefu unaweza kumchokesha mtoto asiye na uwezo mkubwa wa kumakinika ndiposa hadithi hizi zimefupishwa. Kilele chake kimesimilishwa kwa njia ambayo itaafiki matarajio ya watoto ambao hupendezwa na hadithi zenye kiishio cha ushindi na chenye kufurahisha. Baada ya safari zake zenye masaibu mengi, Sindbad aliishi raha mustarehe. Katika kisa cha 'Mbilikimo', haki ilitekelezwa. Katika visa vya 'Nduguze Kinyozi', ndugu wote wawili hawakuangamia, waliokolewa na Kinyozi.

## 3.2 Lugha

Sehemu hii inachanganua matumizi ya lugha kuambatana na nadharia ya Elimumitindo kama ufundi wa mtafsiri wa kufanikisha usimilishwaji.

### 3.2.1 Tashbiha.

Huu ni ulinganishi wa moja kwa moja wa vitu au mambo mawili. Kama ilivyodokezwa katika sura ya pili (rejelea uk. 32), mtoto ataielewa tashbiha iwapo anavielewa vitu au mambo yote mawili yanayolinganishwa katika tashbiha. Iwapo ataielewa tashbiha, mtoto ataweza kuwa na picha kamili ya kinachozungumziwa na pia afahamu sifa zinazosisitizwa na tashbiha. Zaidi ya hayo, tashbiha huinua kiwango cha ubunifu wake.

Kuna tashbiha nyingi ambazo zimetumika katika hadithi ya *'Safari saba za Sindbad'*. Baadhi ya tashbiha hizi ni pamoja na; *'kubwa kama shina la mti'* (uk.9) inayoelezea ukubwa wa mguu wa ndege anayeitwa Rok, *'vingi kama nzige'* (uk.13) inayoonyesha idadi ya wale maadui waliowashambulia mabaharia, *'urefu wao wapata mikono miwili'* (uk.14) inayoelezea kipimo cha urefu wa wale maadui, *'refu kama mvumo'* (uk.14), na *'kugumia kwa kitisho sana kama mbwa'* (uk.16) zinazoelezea aina ya mlio uliotolewa na lile jitu, *'ruka kama mshale'* (uk.17) inayoelezea jinsi lile joka lilivyoshambulia, na *'mawe yanang'aa kama kioo'* (uk.32) inayofafanua mng'aro wa yale mawe. Katika *'Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Tano'*, tashbiha *'mzuri kama mwezi'* (uk.53) imetumika kuelezea kiwango cha uzuri wa yule mke.

Nyingi za tashbihi hizi hazipo katika matini chasili lakini mtafsiri ameziongezea katika matini lengwa. Pia amezifanyia marekebisho baadhi ya tashbiha zilizotumika katika matini chasili ili ziweze kueleweka na mtoto. Kwa mfano, tashbiha *'Linalong'aa kama ndimi za moto'* (tafsiri yangu) iliyoko katika matini chasili imerekebishwa ili iwe *'Linalong'aa kama kaa la moto'* (uk.14) katika matini lengwa.

Mwandishi amefaulu katika kutumia baadhi ya tashbiha hizi katika matini lengwa ingawa badhi yake hazieleweki moja kwa moja na mtoto. Kwa mfano *'refu kama mvumo'* (uk.14) ni tashbiha ambayo huenda ikamtatiza mtoto kuielewa maana na huenda asiufahamu mti huu ambao unaitwa mvumo na ambao hupatikana

pwani. Badala ya neno 'mvumo', mwandishi angetumia neno 'mlingoti' . Mwandishi ana jukumu la kurahisisha zile tashbiha ambazo huenda zikawa ngumu kueleweka na mtoto.

### 3.2.2 Tashihisi

Sawa na tashbiha, tashihisi hueleweka na mtoto iwapo mtoto atafahamu vitu vinavyohusishwa. Tashihisi humsisimua mtoto pale ambapo vitu visivyo na uhai hupewa uhai na hata uwezo wa kuyafanya mambo kama binadamu. Mwandishi ametumia mbinu hii kwa njia finyu sana katika matini lengwa.

Baadhi ya tashihisi ambazo zimetumika Katika hadithi ya '*Safari za Sindbad Baharia'* ni pamoja na; '*ukumbi nao ulitujibisha vilio vyetu vya kukata tamaa'* (uk.15) ambapo ukumbi umepewa uhai na hisia za kupokea na kuvijibu vilio vya Sindbad na wenzake, '*nuru ya taa ikimlika wazi wazi kisha mara ikisinzia'* (uk.24) ambapo nuru imepewa uhai wa kimaumbile kiasi kuwa ina uwezo wa kusinzia kumaanisha ule mwangaza ulitokea mara kwa mara huku wakati mwingine ukipotea, '*kifo chanikodolea macho usoni'* (uk.33) ambapo Kifo kimepewa uhai wa kimaumbile kama vile kuwa na macho ikiwa na maana kuwa Sindbad alifahamu wazi kuwa ikiwa hangenusurika, basi angekufa. Katika '*Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Tano'* tashihisi '*hata hiyo dunia haitanena neno jingine'* (uk.52) imetumiwa ambapo dunia imepewa sifa za kunena na kutonena kuonyesha kuwa yule Waziri angetosheka na yale mahari ambayo angelipwa na Alnacha.

Ingawa mtafsiri ametumia tashihisi katika matini lengwa, hakufanikiwa kutumia tashihisi ambazo ni sahili kueleweka na watoto. Uhuishaji katika kazi za watoto wafaa ufanywe kwa njia ambayo itamwezesha mtoto kuielewa na kuifurahia na hata kumchekesha aisomapo tashihisi katika hadithi.

### 3.2.3 Misemo

Misemo ni vikolezo vya kutia utamu katika lugha. Huipamba lugha na pia hukuza msamiati wa lugha hiyo. Misemo ikitumiwa vizuri katika kazi za watoto huwasaidia watoto katika kukuza msamiati wao na pia hujenga taswira akilini mwao. Taswira hizi humsaidia mtoto kuielewa hadithi. Misemo katika kazi za watoto yafaa iwe sahili.

Baadhi ya misemo ambayo imetumika katika kisa cha *'Safari za Sindbad Baharia'* ni pamoja na *'si hai si maiti'* (uk.5) ambapo Sindbad anaelezea jinsi alivyokuwa katika hali mbaya baada ya kupigwa na mawimbi. *'Nikakaa raha mustarehe'* (uk.13) kumaanisha kukaa na kustarehe. *'Ng'oa nanga'* (uk.30) unamaanisha kuondoka. Katika *'Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Tano'*, msemo *'fanya chapu-chapu'* (uk. 59) unamaanisha haraka haraka. Katika *'Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Sita'* msemo *'daima dawamu'* (uk.63) umetumika kumaanisha wakati wote.

Mtafsiri hakutumia misemo mingi katika kazi yake. Hata hivyo, michache aliyoitumia imetumika vizuri na mtoto ataielewa kwa urahisi.

### 3.2.4 Chuku

Chuku ni mbinu ya kukuza sifa za jambo, kitu au tukio fulani kupita kiasi aidha kwa kulipa sifa za kulikuza likaonekana kubwa kuliko kawaida au pia kulifanya liwe ndogo kuliko kawaida. Hutumiwa katika kazi za watoto ili kusisitiza sifa fulani na pia kumpa taswira ya jambo linaloelezewa. Ile taswira humsaidia mtoto kuwa na picha ya kinachozungumziwa hata ikiwa ni jambo la kidhahania. Chuku pia ni mbinu mojawapo ya mbinu zinazotumiwa ili kumsisimua mtoto.

Katika kisa cha *'Safari Saba za Sindbad, Baharia'* kwa mfano, msimulizi katika (uk.9) anasema kuwa majoka waliokuwa katika kisiwa cha majoka -wala watu-walikuwa wa kutisha kiasi cha kuwa hata wale wadogo wangaliweza kumeza tembo mzima pasipo shida. Hii ni chuku kwa sababu tembo ni mnyama mkubwa sana kiasi cha kumezwa na nyoka mdogo tu. Ni chuku kuwa miti ya mikarafuu iliyokuwa katika kisiwa cha Roha ilikuwa mikubwa kiasi kuwa watu mia moja wangeweza kujificha chini ya mti mmoja bila shida, (uk.12). Mbinu ya chuku inadhihirika zaidi pale ndege Rok amesawiriwa kama aliye na nguvu nyingi sana kiasi kuwa anao uwezo wa kuruka angani akiwa amewabeba tembo na kifaru kwa kutumia kucha zake. Ni chuku kuwa yai la ndege Rok haliwezi kuvunjika ila tu pale litakatwa kwa mashoka na watu wengi ndipo livunjike. Katika *'Kisa cha Mbilikimo Mwenye Kinundu'* ni chuku kuwa Mganga, Mwislamu na Mkristo hawakutambua kuwa yule Mbilikimo alikuwa amekufa. Ni jambo lisilo la kawaida kuwa kila mmoja wao alipigana na mzoga bila kutambua na tena haiwezekani kuwa yule maiti kwa wakati huo wote hakuwa akinuka. Mwandishi kwa jumla

amefaulu katika kutumia mbinu hii kwani anaipa kazi yake ujumi na kumsisimua msomaji.

### 3.2.5 Vihisishi

Mwandishi amevitumia vihisishi kwa wingi katika matini lengwa. Vingi vya vihisishi hivi haviko katika matini chasili. Miongoni mwa vihisishi hivi ni '*oh!*' (uk.1) kuonyesha jinsi mtumishi wake Sindbad alivyopigwa na butwaa aliposikia kuwa Hindbad hakumfahamu Sindbad. '*Lo-o! Masalale!*' (uk.16) kuonyesha mshtuko wa mabaharia baada ya kuzingirwa na maadui. '*Toba! Musa Nabii!*' (uk.45) kuonyesha majuto ya mganga. '*Mama We!*' (uk.46) na 'Toba!' (uk.46). Ingawa vingi vya vihisishi hivi vina asili yake katika ndini ya Kiisilamu, matumizi yake yamesheheni katika lugha ya Kiswahili. Mtoto atavifurahia kuvisoma.

## 3.3 Msamiati

Kama ilivyodokezwa katika sura ya pili (rej uk.46), usimilishwaji huipa kazi inayosimilishwa uwazi na uangavu unaowafaa wasomaji. Uangavu huu hutegemea miongoni mwa vipengele vingine kipengele cha msamiati. Msamiati ukiwa mgumu, unamtatanisha mtoto na unatinga uelewa wake na hatimaye anakosa ile hamu ya kukisoma kitabu. Hivyo basi mwandishi ana jukumu la kuurahisisha msamiati wa matini lengwa ili ueleweke wazi na watoto anaowalenga. Mwandishi anastahili kuusimilisha msamiati ili uambatane na lugha pokezi. Kuna baadhi ya misamiati ambayo imetumiwa katika matini chasili ambayo huenda ikamtatiza mtoto kuielewa. Kwa mfano, neno '*reale*' badala ya

'pesa'. Pia misamiati ya mimea na bidhaa kama vile *'karafuu'*, *'midalasini'*, *'sandali' na 'kukumanga'* na msamiati wa marashi kama vile *'udi na ambari'* ni migumu kueleweka.

Mtafsiri ametohoa majina ya miji na visiwa ili kufanya iambatane na sarufi ya lugha pokezi kama ifuatavyo:

| Matini chasili | Matini lengwa |
|---|---|
| El-Basrah | Basra |
| Es-Selahit | Salahat |
| Serendib | Serandib |

Hata baada ya kufanyiwa utohozi, msamiati huu ni mgumu kutamkika na mtoto maana hauambatani vizuri na sarufi ya lugha pokezi. Badala yake, mtafsiri angetumia majina ya miji ya pwani ya Afrika ambayo ni rahisi kueleweka na mtoto.

### 3.4 Usimulizi

Mwandishi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza katika kisa cha *'Hadithi Saba za Sindbad, Baharia'* ambapo Sindband mwenyewe anawahadithia wenzake hadithi kuhusu safari zake. Usimulizi huu kulingana na Wamitila (2003) hujenga uhusiano wa kibinafsi kati ya msimulizi na msomaji. Hali hii humfanya mtoto kupenda kujitambulisha na mhusika ambaye ni msimulizi – mwandishi. Katika kisa cha *'Mbilikimo Mwenye Kinundu'*, *'Nduguye Kinyozi wa Tano'* na *'Nduguye Kinyozi wa Sita'*, usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika. Usimulizi kama huu

unampa nafasi msimulizi kuteua ni mambo yapi ya kusimulia na ni yapi ya kupuuza kufungamana na umuhimu wa mambo hayo.

## 3.5 Wahusika

Hadithi hizi zina wahusika wanyama na wahusika binadamu. Kila hadithi imetumia wahusika tofauti na hadithi nyingine. Sehemu hii imehakiki sifa za wahusika wakuu katika hadithi hizi.

### 3.5.1 Kisa cha Safari Saba za Sindbad Baharia.

Mhusika mkuu katika safari zote saba ni Sindbad. Ni mhusika jasiri. Kila wakati anapojikuta masaibuni, anatumia hekima na ujasiri wake ili kujiokoa. Kwa mfano, alipotekwa nyara na yule mzee wa Baharini, Sindbad alitengeneza mvinyo ambao ulimlevya huyo mzee kisha Sindbad aliweza kumuua na akaweza kutoroka. Alipotumbukizwa katika lile shimo la maiti, Sindbad aliweza kugundua mwanya ambao aliutumia kutorokea. Alitumia ndege Rok na Tai kuokoa maisha yake.

Sindbad ni mkarimu na mwenye huruma. Kila wakati anaporudi kutoka safarini zake za kuchuma mali, anawagawia watu maskini mali yake. Ukarimu wake labda ndio ulimfanya astawi na kuwa tajiri wa kufana. Mtoto anajifunza kuwa jasiri na kuwa mkarimu kupitia kwa mhusika huyu.

### 3.5.2 Kisa cha Mbilikimo Mwenye Kinundu

Mhusika mkuu ni Mbilikimo. Kupitia kifo cha Mbilikimo, sifa ya ukweli inaendelezwa na wahusika Mshonaji, Mganga na Mwislamu pale ambapo kila mmoja wao alisema ukweli kuhusu jinsi alivyohusika na kifo cha Mbilikimo. Ukweli uliwaokoa kutoka kifoni. Mtoto anaweza kujifunza umuhimu wa kuwa mkweli kupitia wahusika hawa.

### 3.5.3 Kisa cha nduguye Kinyozi wa Tano.

Mhusika mkuu ni Alnacha. Ni mvivu sana na anapenda vitu vya bwerere, uk.51. Uvivu wake ulimfanya akae mbele ya duka na kujiliwaza kwa mawazo ya kinjozi badala ya kuuza mali yake. Hatimaye mali yake yalimponyoka akabakia kuwa maskini. Ni mwenye tamaa ya mali. Tamaa ya mali ilifanya apigwe, aumizwe na anyang'anywe pesa zake alipokuwa nyumbani kwa bibi aliyekuwa tajiri na hatimaye kufukuzwa mjini na Kadhi wa ule mji. Kupitia kwa mhusika huyu, mtoto ataweza kujifunza kuwa uvivu na tamaa huangamiza.

### 3.5.4 Kisa cha Nduguye Kinyozi wa Sita.

Mhusika mkuu ni Shakabak. Alikuwa mwombaji. Alizurura mjini akiombaomba. Tabia hii ilimfanya hatimaye aishie kuwa mtumwa. Mtoto ataweza kujifunza kuwa tabia ya kuzururazurura mjini na kuombaomba si tabia nzuri na inaweza kumwangamiza mtu.

Mtafsiri amefaulu kuwasawiri wahusika katika njia ambayo mtoto ataweza kuwaelewa kisifa na kitabia na kujinasibisha na wale wazuri. Hata hivyo, wahusika hawa hawakupewa majina yaliyo rahisi kutamkika na kukumbukika na mtoto. Mtafsiri ameyatohoa tu bila kuzingatia kama utohozi huu unaambatana na sarufi ya lugha pokezi au la. Majina haya yametoholewa kama ifuatavyo;

| Matini Chasili | Matini Lengwa |
|---|---|
| Ainaschar | Alnacha |
| Shakalik | Shakabak |
| Barmekis | Bamaside |
| Khalifeh Harun Er-Rashid | Khalifa |
| Es-Sindibad of the land | Hindbad |
| Es-Sindibad of the sea | Sindbad |

Mtafsiri alihitajika ayasimilishe majina haya ili yaweze kutamkika kwa urahisi. Kwa mfano, Alonacha, Shakabaki, Hindibadi na Sindibadi.

## 3.6 Maudhui

Maudhui ya kazi za watoto yafaa iwafunze maadili ya kijamii. Katika kitabu hiki, maudhui mbalimbali kama vile wema, ukarimu, haki na wivu yameshugulikiwa.

### 3.6.1 Ukarimu

Unaendelezwa na mhusika Sindbad pale ambapo baada ya kurudi kutoka safarini, alihakikisha kuwa aliwapa maskini sehemu ya mali yake. Kutokana na ukarimu wake, Sindbad alifanikiwa kuwa tajiri mkubwa. Ukarimu pia unaendelezwa na mhusika Bamaside ambaye alimpa Shakabak aliyekuwa maskini sehemu ya mali yake.

### 3.6.2 Wema

Kinyozi anaendeleza maudhui haya. Ingawa ndugu zake ndio waliojiingiza katika masaibu kutokana na tabia yao ya uvivu, Kinyozi anawatendea mema. Alimwendea ndugu yake wa tano alipoachwa baada ya kupigwa na wakora, akakaa naye nyumbani kwake na kumuuguza. Pia alimwokoa ndugu yake wa sita alipomwendea kutoka jangwani pale alipokuwa ametupwa na tajiri wake ili afe, akaishi naye na kumtunza kama ndugu yake.

### 3.6.3 Haki

Maudhui ya haki yamejitokeza katika *'Kisa cha Mbilikimo'* ambapo uamuzi wa kesi ulifanywa kwa njia ya haki. Hakuna yeyote aliyenyongwa kwa sababu si wao waliomuua Mbilikimo ila kifo chake kilisababishwa na mfupa uliokwama kooni mwake.

### 3.6.4 Uvivu

Maudhui haya yanaendelezwa na ndugu zake Kinyozi, Alnacha na Shakabak. Uvivu unakemewa na madhara yake yanaonyeshwa wazi pale ambapo hawa ndugu wawili wanaangamia hatimaye. Alnacha anaishia kupoteza kila kitu na kufukuzwa kutoka mjini. Shakabak pia alipoteza mali yake yote na akawa mtumwa.

### 3.7 Umbo La Kitabu

Sehemu hii imeshugulika na mambo ya uchapishaji kuliko uandishi. Pamoja na lugha, umbo la kitabu huchangia katika ujumi wa kazi ya fasihi.

#### 3.7.1 Jalada na Anwani ya Kitabu

Jalada la kitabu hiki limetiwa rangi nyekundu (taz. Kbt. 9). Lina mchoro wa kiumbe anayeonekana kama zimwi na mchoro wa binadamu aliyeketi akiwa ameshika kifaa mikononi mwake. Mchoro wenyewe haueleweki moja kwa moja. Mchoro huu unaweza kumkanganya mtoto maana unatofautiana na yaliyomo katika hadithi zote nne. Anwani ya kitabu ni *'Alfu Lela Ulela'* ambayo imefafanuliwa kuwa ni siku elfu moja na moja. Anwani hii haina uwiano na mchoro wa jalada wala hadithi zenyewe. Watoto hawapendezwi tu na michoro lakini pia wanajaribu kuielewa. Kwa hivyo, iwapo mwandishi ataamua kutumia mchoro katika jalada la kitabu, basi mchoro huo hauna budi kuwa sehemu ya yaliyomo ya kitabu chenyewe.

#### 3.7.2 Michoro ya Matini

Vielezo vikitumika katika matini hutumiwa kufafanua matini hiyo. Kwa hivyo vinafaa viwe na utaratibu maalum. Vielezo ambavyo mwandishi amevitumia katika hadithi za *'Safari Saba za Sindbad, Baharia'* vina uwiano wa moja kwa moja na matini (taz. Vbt. 10 – 14). Hata hivyo, vielezo hivi vimekosa udhabiti. Mhusika mkuu amechorwa kwa njia zinazotofautiana jambo ambalo huenda likamkanganya mtoto katika kutambua mhusika huyu. Kwa mfano, katika mchoro

wa Kbt. 10 na 14, kichwa cha Sinbad ki wazi, hakina kilemba ilhali katika mchoro wa Kbt. 11 na 12, mhusika huyu amevalishwa kilemba. Vile vile mavazi ya Sindbad yanatofautiana kutoka mchoro mmoja hadi mwingine. Katika hadithi ya *'Mbilikimo Mwenye Kinundu'*, mchoraji amefaulu kuambatanisha maelezo ya wahusika wake na mchoro. Ni rahisi kumtambua Mbilikimo, mkewe mshonaji na mshonaji mwenyewe (taz. Kbt. 15). Mchoro unaohusu Alnacha na kapu lake haukujitokeza vizuri. Ingawa kapu lake limejaa vitu vya thamani, mchoro unaonyesha kinyume cha mambo ambapo kapu lile limechorwa kama lililojaa vikochokocho tu visivyoweza kutambulika ama ni vya thamani (taz. Kbt. 16). Labda kama mchoraji angetumia michoro iliyo na rangi, basi ingekuwa rahisi kuvitambua vitu hivyo kama vyenye dhamana. Hata hivyo mchoraji amefanikiwa kuijumuisha michoro hii katika matini lengwa kwa kuongezea michoro ambayo haipo katika matini chasili.

### 3.7.3 Maandishi ya Chapa

Mwandishi ametumia kiwango cha wastani cha maandishi. Maandishi haya pamoja na rangi nzito ya chapa na pia karatasi nzuri zimeifanya kazi hii isomeke vizuri bila utata wowote.

## 3.8 Hitimisho

Sura hii imehakiki usimilishwaji katika kitabu cha *Alfu Lele Ulela.* Kwa kuongozwa na nadharia ya Elimumitindo, sehemu hii imehakiki jinsi lugha imetumika kitamathali na pia jinsi ambavyo maudhui ya matini lengwa yamewasilishwa.

Aidha sifa na tabia za wahusika zimeshugulikiwa. Kadhalika, umbo la kitabu limehakikiwa pamoja na ploti za hadithi hizi.

Mtafsiri amefanikiwa katika kuisimilisha kazi yake kwa niaba ya kusomwa na watoto. Ameweza kutumia sentensi fupi fupi na hata aya fupi fupi ambazo hazimchoshi msomaji kinyume na kazi ya matini chasili. Zaidi ya hayo, ameweza kuitumia mbinu ya ufupishaji. Ameifupisha ploti ya matini chasili bila kuathiri hadithi zenyewe na pia kuitafsiri kwa lugha ambayo ni sahili na rahisi kueleweka na mtoto aliyelengwa. Matukio ya ploti yana mfululizo wa moja kwa moja na maudhui yake ni mwafaka kwa watoto. Hatimaye ameweza kutumia lugha kufuma pamoja vipengele hivi vyote na kuibuka na matini lengwa.

Sura ifuatayo imehakiki usimilishwaji wa riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani* kwa kuzingatia mikakati na mbinu za usimilishwaji zilizoainishwa katika sura ya pili. Vipengele vya lugha, ploti, wahusika, maudhui na umbo la kitabu vimeshugulikiwa.

# SURA YA NNE

## Usimilishwaji wa Riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani*

### 4.0 Utangulizi

Sura hii imehakiki usimilishwaji wa riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (1981) ianayolenga hadhira ya watoto iliyosimilishwa kutoka kwa riwaya iliyolenga hadhira ya watu wazima ya *King Solomon's Mines.*

Kitabu hiki kwa mara ya kwanza kiliandikwa na Haggard (1885) na kutafsiriwa na Johnson kwa lugha ya Kiswahili katika miaka ya thelathini. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), kitabu hiki kilikuwa ni miongoni mwa riwaya za kimagharibi zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kujenga msingi wa riwaya ya Kiswahili. Wataalamu wengi wamekichukulia kitabu hiki kuwa ni tafsiri tu kwa sababu wamejikita tu katika kipengele cha lugha bila kuzingatia marekebisho mengine ambayo yamefanyiwa kitabu hiki. Kutafsiriwa kwa kitabu hiki si ithibati kamili ya kukihalalisha kuwa tafsiri tu. Ingawa utafiti huu unakubaliana na maoni ya wengi kuwa kitabu hiki kimetafsiriwa, kimefanyiwa marekebisho mengine mengi yanayodhihirisha kuwa, bali na kutfsiriwa, pia kimesimilishwa.. Utafiti huu umelichukulia swala la tafsiri kama njia moja inayotumiwa kufanikisha usimilishwaji.

Kitabu hiki kiliandikwa na Haggard (1885) wakati nchi za Ulaya zilikuwa zimezimiliki na kuzitawala nchi za bara la Afrika kama koloni zao. Hadithi hii ilitungwa katika mandhari ya nchi ya Afrika Kusini ambayo ilikuwa miliki ya



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Waingereza. Hadithi hii inahusu Wazungu watatu , Bw. Good, Bw. Henry na Bw. Quatermain ambao walisafiri kuelekea nchi ya Wakukuana kule Afrika Kusini ili kwenda kumtafuta ndugu yake Bw. Henry. Safari hii ilikuwa ndefu na yenye matatizo mengi. Iliwabidi wapande na kushuka milima, wavuke mabonde na wapitie jangwani kabla ya kufika kule. Walikumbana na matatizo mengi njiani kama vile kupatwa na kiu na njaa kwa sababu ya ukosefu wa maji na chakula jangwani. Ng'ombe wao walikufa kwa njaa na kiu. Baadhi ya watumishi wao walikufa pia na wakati mwingine waliumizwa na joto la jangwani na wakazizimwa na baridi ya milimani. Baada ya kufika katika nchi ya Wakukuana, waliweza kukaa huko kwa muda na kushiriki katika sherehe na vita vya Wakukuana. Hatimaye walifanikiwa kumpata ndugu yake Bw. Henry wakiwa safarini kurudi kwao.

Kulingana na Mpesha (1995), kitabu hiki cha *Mashimo ya Mfalme Sulemani* ni miongoni mwa vitabu ambavyo viliweza kufanyiwa marekebisho ili visomwe na watoto shuleni katika kipindi cha wakoloni na kikawavutia wasomaji.

Kwa mujibu wa nadharia ya Elimumitindo, utafiti huu umehakiki jinsi vipengele vya ploti, lugha, maudhui, wahusika na vielezo vimesimilishwa ili kuifaa hadhira ya watoto. Utafiti huu umewalenga watoto wa umri wa kati ya miaka kumi hadi miaka kumi na mitano (taz. uk.1-2) kwa maelezo kuhusu watoto hawa). Kwa mujibu wa Oyoo (2003), watoto wa umri huu huvutiwa na ploti iliyojaa matukio mengi na yenye kusisimua. Tena, watoto hawa huvutiwa na matukio ambayo yatawatambulisha kwenye maeneo na mazingira mapya.

## 4.1 Ploti

Kwa jumla, kitabu hiki kina sura ishirini. Hizi ni sura fupi fupi na zina uwiano wa moja kwa moja. Hadithi hii ina mtiririko mzuri wa matukio. Ploti ya kitabu hiki inaweza kugawanywa katika sehemu nne kuu;

1. Matayarisho kabla ya safari.
2. Safari yenyewe.
3. Nchi ya Wakukuana.
4. Safari ya kurudi nyumbani.

### 4.1.1 Matayarisho Kabla ya Safari.

Sehemu hii inajumuisha sura ya kwanza hadi sura ya tatu. Katika sehemu hii wahusika wakuu watatu ambao ni Bw. Good, Bw. Henry na Bw. Quatermain wanakutana melini wakiwa katika shughuli zao za usafiri. Bw. Good na Bw. Henry wako safarini kwenda kumtafuta ndugu yake Bw. Henry. Bw. Quatermain yumo safarini ya kurejea kwake Durban. Wote wanakutana kisadfa na baada ya maongezi ya muda mrefu, Bw. Good na Bw. Henry wanatambua kuwa, Bw. Quatermain alikuwa amekutana na George (ndugu yake Bw. Henry) akiwa safarini kuelekea kwenye Mashimo ya Sulemani. Pia walipata kutambua kuwa, Bw. Henry alikuwa amepewa ramani ya kumwelekeza jinsi angesafiri mpaka kwenye Mashimo ya Sulemani na Mzungu mmoja, Jose da Silvestre. Fauka ya hayo, waliweza kufahamu jinsi Bw. Quatermain alikuwa na uzoefu na ujuzi wa hali ya juu wa safari kutokana na safari nyingi alizokuwa amezifanya katika biashara yake ya kuwinda ndovu na kuuza pembe. Hali hii iliwapelekea

kumuuliza Bw. Quatermain aandamane nao safarini jambo ambalo hatimaye alilikubali.

Walianza kujiandaa kwa minajili ya kuianza safari yao. Walinunua gari na ng'ombe wa kuliburura, wakatayarisha dawa na chakula cha kuchukua safarini, bunduki na pia risasi na wakawachagua Waafrika watano akiwemo Umbopa kuwa watumishi wao.

### 4.1.2 Safari Yenyewe

Sehemu hii imejumuisha sura ya nne hadi saba. Safari yao inaweza kugawanywa katika awamu nne. Katika awamu ya kwanza, wanaingia msituni baada ya kufika mji wa Sitanda katika nchi ya Matebele na kuwaacha Goza na Tom ili kulichunga gari lao. Wakiwa msituni waliweza kuwawinda ndovu na kuwang'oa pembe ambazo walizificha chini ya ardhi wakiwa na matumaini kuwa wangezichukua na kwenda nazo nyumbani wakijaliwa kurudi kwao. Hata hivyo, walipatwa na masaibu mengi. Ng'ombe wao walikufa kutokana na njaa, magonjwa na majani yenye sumu. Pia walimpoteza mmoja wa wafanyikazi wao, Khiva, baada ya kushambuliwa na ndovu.

Katika awamu ya pili, waliingia katika jangwa lililokuwa kavu na lenye joto jingi. Iliwabidi wasafiri usiku na kupumzika mchana kwa sababu ya jua. Kutembea kwa muda mrefu kuliyafanya maungo yao kuuma. Zaidi ya hayo, walipatwa na kiu sana maana hakukuwa na maji jangwani ingawa mara kwa mara waliweza

kubahatika kupata maji hata kama ni machafu na kuweza kukata kiu chao. Wakati mwingine walifanikiwa kuyapata matikiti ambayo yaliwasaidia kukata kiu.

Awamu ya tatu ya safari yao ilianza kwa kuipanda milima iitwayo *'Maziwa ya Shaba'*. Katika safari hii, walikumbwa na njaa karibu wapoteze matumaini yao ya kuishi tena kwani milimani hakukuwa na wanyama wa kuwindwa. Baridi ya kule milimani iliwazizima kiasi kuwa mmoja wa watumishi wao, Ventvogel, alifariki. Hapa ndipo pia walibahatika kuona maiti ya yule mzungu, Jose da Silvestre, aliyempa Bw. Quatermain ile ramani iliyokuwa ikiwaongoza mpaka sasa. Hatimaye walifanikiwa kumpata mnyama, wakamuua na wakamla ili kuyatuliza matumbo yao. Baada ya kula walipumzika kando ya mto, pale ambapo Infadus, Skraga na askari wengine waliwakuta na kuwachukua mpaka nchi ya Wakukuana.

### 4.1.3 Nchi ya Wakukuana

Sehemu hii imejumuisha sura ya nane hadi kumi na nane. Bw. Quatermain na wenzake walikutana na Mfalme Twala, mfalme wa Wakukuana ambaye ni katili na mwovu. Walikutana na kizee Gagula ambaye ni mwanamke mchawi. Wakiwa huko, walihudhuria baadhi ya sherehe za Wakukuana kama vile *'Ngoma kuu ya kufichua wachawi'* ambapo watu wengi hupoteza maisha yao. Ni katika sherehe hizi ambapo Bw. Quatermain na wenzake walizuilia kutekelezwa kwa mauaji ya Foulata, mwanamwali aliyekuwa mrembo na Umbopa yule mtumishi wao. Baada ya sherehe hizi, Bw. Quatermain na wenzake walishiriki katika vita vikali baina ya

Mfalme Twala na wafuasi wake na Umbopa na wafuasi wake na wakafaulu kumng'oa Mfalme Twala mamlakani. Umbopa alitawazwa kuwa Mfalme wa Wakukuana.

Baadaye, Bw. Quatermain na wenzake walizuru Mashimo ya Sulemani wakiwa wameandamana na Infadus, Foulata na kizee Gagula pamoja na askari wengine. Wakiwa kule ndani, Foulata aliuawa na Gagula ambaye kwa upande mwingine alifinywa na ukuta mpaka akafa. Bw. Quatermain na wenzake walipatwa na masaibu pale ule ukuta uliwafungia ndani na hawakuwa wakijua jinsi ya kuufungua. Baadaye, waliweza kupata mwanya wa kupitia mpaka wakatoka nje ya mashimo yale ya Sulemani pale ambapo waliungana tena na Infadus na wenzake kisha wakarudi kwa Mfalme Ignosi (Umbopa).

### 4.1.4 Safari ya Kurudi Nyumbani.

Sehemu hii imejumuisha sura kumi na tisa hadi ishirini. Bw. Quatermain na wenzake walimuaga Mfalme Ignosi na wakaondoka kurudi kwao. Walifanikiwa kumpata ndugu yake Bw. Henry kule jangwani alipokaa baada ya kuvunjika mguu wake. Walimchukua na wakaenda naye nyumbani.

Hiki ndicho kilele cha hadithi ambapo mtafsiri amefanikiwa kuyatuliza matarajio ya wasomaji. Si hayo tu, kupitia ploti, mwandishi amefaulu katika kuwapitisha wasomaji wake katika hali mbalimbali za hisia kama vile hisia za furaha, hisia za huzuni, hisia za kupoteza matumaini au kuwa na matumaini na hata hisia za

kuogofya kupitia wahusika kama vile Gagula au mandhari kama yale ya Mashimo ya Sulemani. Pia yale matumizi yake ya motifu ya kutafuta inaifanya hii motifu kuwa kiungo muhimu kinachounganisha matukio yakawa hadithi iliyo na mfululizo wa kupendeza.

Hata hivyo mtafsiri hakufaulu katika kuipa hadithi ploti nzuri katika sehemu ya utangulizi. Ametumia maelezo mengi sana mwanzoni mwa kitabu katika sura za kwanza mbili ambayo yanaifanya hadithi ikawie kuanza.. Baadhi ya maelezo haya yangeondolewa bila kuharibu ploti ya hadithi. Kwa mfano, maelezo kuhusu sababu za kukiandika hiki kitabu si muhimu katika ploti hii. Maelezo haya pia yanakanganya msomaji kwa sababu yamebeba mambo mengi sana kwa wakati mmoja. Kuna ile hadithi kuhusu jinsi Bw. Quatermain walikutana na Bw. Good na Bw. Henry na kuna ile barua ambayo ilikuwa imeandikwa na Jose da Silvestre na hadithi yenyewe.

Sehemu hii ya ploti ina wahusika wengi sana ambao wanakanganya. Baadhi yao hawana umuhimu wowote katika sehemu hii kama vile mhusika Foulata na Gagula. Kwa jumla usimilishwaji wa sehemu hii ya ploti haukufanikisha mahitaji ya wasomaji maana watoto kulingana na Hollindale (1974) hufurahia hadithi zenye utangulizi mfupi na unaoeleweka moja kwa moja. Utangulizi huu unapaswa kumjulisha mtoto kile anachokitarajia katika hadithi moja kwa moja. Haya hayajitokezi katika matini lengwa.

## 4.2 Lugha

Kulingana na nadharia ya Elimumitindo, matumizi ya lugha hujitokeza katika vipengele kama vile jazanda, taswira, taharuki, tashihisi, tashbiha, tanakali za sauti na kadhalika. Mwandishi hutumia vipengele hivi ili kuuwasilisha ujumbe wake. Sehemu hii imeshugulikia usimilishwaji wa vipengele hivi.

### 4.2.1 Tashbiha

Tashbiha humsaidia mtoto kuwa na picha ya kile ambacho kinazungumziwa katika matini. Picha inayoundwa kupitia tashbiha humsaidia kuielewa ile dhana sawasawa. Kwa mfano, tashbiha *'eusi kama kaa'* itamsaidia mtoto kutambua kiwango cha *'weusi'* unaozungumziwa. Ni muhimu basi kutumia tashbiha ambazo mtoto ataweza kuzifahamu ili mtoto auelewe ujumbe wa mwandishi.

Mtafsiri ametumia tashbiha nyingi katika matini lengwa. Baadhi yake ni *'akinusa hewa ile yenye moto kama anavyonusa paa mzee anayeshuku hatari'* (uk.44), kuonyesha jinsi Ventvogel (mmoja wa watumishi wa Bw. Quatermain na wenzake) alijaribu kila awezalo kutambua mahali palipokuwa na maji. Tashbiha *'akirukaruka na kupiga kelele kama mtu aliyeshikwa na wazimu'* (uk.47) imetumika kuonyesha furaha isiyo na kifani aliyokuwa nayo Umbopa baada ya kuyapata matikiti ambayo yangewasaidia kukata kiu walichokuwa nacho. Tashbiha *'ukingo wa mlima uliokuwa kama meza'* (uk.54) inamaanisha kuwa, kilele cha mlima ule kilikuwa tambarare. Tashbiha *'njia pana iwandani imetambaa kama nyoka'* (uk.55) inaonyesha jinsi njia ilikuwa imenyooka. Tashbiha 'k*abila hili*

*lilikuja kama kuvuma kwa dhoruba'* (uk.64) inamaanisha kuwa Wakukuana waliingilia ile nchi kwa kishindo kikubwa. *'Wakageuka kama simba watafutao kitu cha kurarua'* (uk.65) ina maana kuwa wakati huo, Wakukuana walikuwa na ari na mori wa kulifanya jambo lolote mradi tu waweze kutimiza haja yao. Tashbiha *'wakawa kama mwitu wa mikuki'* (uk.87) inafafanua idadi ya askari wa Wakukuana. Tashbiha *'akakaza mwili kama mbwa aliyesikia harufu ya nyama porini'* (uk.90) imetumika kuonyesha tabia ya kizee Gagula alipokuwa anatambulisha wachawi. Tashbiha *'damu za watu zinamwagika kama mto wakati wa masika'* (uk.95) inaonyesha jinsi mfalme Twala aliwauwa watu wengi wakati wa utawala wake.

Mwandishi hakufanikiwa kusimilisha tashbiha alizozitumia katika matini lengwa. Kama ilivyodokezwa katika sura ya pili (Taz. uk.22), mwandishi anatakiwa kutumia jicho la mtoto anaposimilisha kazi za watoto ndipo waweze kuzielewa. Mtafsiri hakuyatilia maanani haya alipokuwa anazisimilisha tashbiha alizozitumia katika matini lengwa. Nyingi za tashbiha hizi zimetumia msamiati mgumu wa baharini na ambao si rahisi kueleweka moja kwa moja na mtoto. Baadhi ya msamiati huu ni maneno kama dhoruba, mawimbi ya bahari na ukungu. Badala ya kusema kwa mfano, '... kama *mwitu wa mikuki'* (uk.87) angetumia tashbiha kama '...*kama mwitu wa miti'* na badala ya '...*mwagika kama mto wakati wa masika'* (uk.95) angerahisisha hii tashbiha kwa kusema, '*mwagika kama maji ya mfereji'*.

### 4.2.2 Misemo

Misemo humpa mtoto taswira inayomwezesha kuelewa kinachozungumziwa katika matini mbali na kuongezea ujumi wa lugha. Kwa jumla, mtafsiri ametumia misemo katika matini lengwa. Baadhi ya misemo hii haipo katika matini chasili ilhali mingine ipo lakini ameifanyia marekebisho na kuiingiza katika lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya misemo aliyoitumia ni pamoja na '*kujifunga kibwebwe*' (uk.2) kumaanisha kujitahidi. '*Kung'oa nanga*' (uk.3) ambao una maana ya kuanza safari. 'K*wa macho ya uroho*' (uk.36), unamaanisha kuwa na tamaa. 'A*mekaa kitako*' (uk.39), una maana ya kutulia. '*Mwendo wetu ulikuwa wa kobe tu*' (uk.48), unamaanisha kuwa walitembea pole pole sana. '*Anakata roho*' (uk.51), una maana ya kufariki. '*Tutafanya jitihada*'(uk.113) una maana ya kufanya bidii. '*Kata tamaa*' (uk.168) una maanisha kutokuwa na matumaini ya jambo tena na msemo '*giza totoro*'(uk.154) una maanisha kiza kingi.

Mtafsiri amefaulu katika kuisimilisha misemo hii katika matini lengwa. Ameweza kutumia lugha inayoeleweka na watoto kwa urahisi.

### 4.2.3 Vihisishi

Vihisishi humliwaza mtoto anapoisoma hadithi. Humpa nafasi ya kupumua na humshirikisha katika kuvitamka hivyo vihisishi. Si hivyo tu, vihisishi husisimua hisia za mtoto kulingana na jinsi vimetumiwa katika matini. Huenda mtoto akawa

na hisia za furaha, huzuni, hasira, huruma na zinginezo. Kwa kufanya hivyo, mtoto anaweza kuondoa uchovu wa kuisoma ile hadithi na pia kuondoa ile hali ya ukinaifu wa kusoma maandishi yaliyowazi tu.

Mwandishi ametumia vihisishi kama *'lo!'* (uk.13) ili kuonyesha jinsi Bw. Good alishangazwa na hadithi ile iliyokuwa imeandikwa na marehemu Jose da Silvestre kwani hakuwa amewahi kusikia hadithi nyingine kama hiyo hapo kabla. Kihisishi *'Alhamdulilahi!'* (uk.43) kimetumiwa kuonyesha furaha aliyokuwa nayo Bw. Quatermain baada ya kuwa na hakika kuwa wangeyapata maji ya kukidhi kiu chao hatimaye. Kihisishi *'Lo!'* (uk.46) kimetumika kuonyesha mshangao wa jinsi walivyoyagugumia yale maji baada ya kuyapata. Kihisishi *'Ah!'* (uk.125) kimetumika kama tamko la dharau pale ambapo Ignosi anawadharau askari wa Twala baada ya kuwashinda vitani. Katika ukurasa huo huo, baada ya Bw. Quatermain kuhakikisha kuwa Bw. Good alikuwa salama, anatamka tamko la kumshukuru Mungu *'alhamdulilahi!'*. Tamko lili hili linatamkwa na Bw. Quatermain baada ya wao kunusurika kifo baada ya kuugundua ule mwanya ambao ungewasaidia kutoka ndani mwa Mashimo yale ya Sulemani. Kihisishi *'lo!'* (uk.150) kimetumiwa kuonyesha jinsi Bw. Good alivyokiajabia kile kifuko kilichokuwa na almasi. Foulata katika (uk.151) anatamka *'lo! lo! lo!'* kuonyesha hofu iliyomshika alipoona kuwa mwamba ulikuwa unaanguka. Kihisishi *ah!* (uk.152) kinaonyesha hisia za kuudhika za Bw. Quatermain baada ya kushuhudia kitendo cha Gagula cha kumuua Foulata. Katika ukurasa huo huo, Quatermain alishangaa *'lo!* alipoona jinsi ule mwamba ulivyompondaponda Gagula mpaka

akafa. Bw. Henry anatamka kihisishi *'haya!'* (uk.157) ili kuwapa moyo wenzake waliokuwa wamekata tamaa ili waje walichukue lile jiwe pamoja.

Wakati mwingine mtafsiri ametumia katika matini lengwa visawe vya vihisihi vilivyotumiwa katika matini chasili jambo ambalo limekubalika katika usimilishwaji. Kwa mfano, vihisishi vifuatavyo katika matini chasili vimetumika,

1) *'Heavens! How we did drink!'* (uk. 79)
   (mbingu! Jinsi tulivyokunywa!') (tafsiri yangu)

2) *'Great powers! It is my brother George!'* (uk.292)
   (Nguvu kuu! Ni ndugu yangu George!) (tafsiri yangu)

na ambavyo vimesimilishwa katika matini lengwa kama ifuatavyo,

1) *'Lo! Tulivyokunywa!'* katika uk.46.
2) *'Alhamdulilahi! Ni ndugu yangu George!'* Katika uk.167

Mtafsiri ameweza kuvisimilisha vihisishi katika matini lengwa ili viwafae watoto wanaolengwa. Ingawa asili ya baadhi ya vihisishi hivi ni dini ya Kiislamu, matumizi yake yamesheheni katika lugha sanifu ya Kiswahili na kwa hivyo vihisishi hivi vinaeleweka na watoto.

### 4.2.4 Tanakali Sauti

Kama ilivyo katika matumizi ya vihisishi, tanakali sauti ni muhimu katika kazi za watoto kwani humliwaza mtoto na pia humshirikisha katika matamshi ya tanakali sauti hizi. Kwa mujibu wa Alembi (1991), watoto huwa wasikivu wa sauti na huwa na uwezo wa kutambulisha sauti tofauti tofaufi hata bila kuona asili ya sauti yenyewe.

Baadhi ya tanakali sauti alizozitumia mwandishi ni pamoja na '*woof! woof!*' (uk.28) ambayo ni sauti ya mlio wa ndovu. Katika (uk.51) tanakali sauti '*aa! aa!*' ambayo inaambatana na kilio cha Foulata baada ya kuchomwa kisu na Gagula imetumiwa na inaibua hisia za hofu kwa msomaji. Tanakali sauti '*sh! sh!*' (uk.137) ambayo ni sauti iliyoambatana na kupumua kwa Bw. Good akiwa usingizini imetumika. Katika kurasa 139, 140 na 141, tanakali sauti '*ha! ha! ha!*', '*hee! hee! hee! ha! ha!* inayoambatana na kicheko cha Gagula imetumika. Hii tanakali inaibua hisia za chuki kwa msomaji.

Mtamfsiri amebadilisha baadhi ya tanakali sauti na kuziandika upya. Kwa mfano tanakali sauti '*help! Help!*' na '*hush-h-h!*' katika matini chasili zimebadilishwa kuwa '*aa! aa!*' na 'sh! sh!' katika matini lengwa. Vile vile, ameongezea baadhi ya tanakali zingine ambazo haziko katika matini chasili. Kwa mfano, tanakali sauti '*hee! hee! hee!*' (uk. 141). Kwa jumla, mtafsiri amefaulu kusimilisha tashbiha hizi ingawa hakutumia baadhi yake kama vile 'sh! sh!' kwa njia inayofaa. Tanakali sauti hii imetumika katika matini lengwa ikiwa na maana ya kukoroma ilhali katika hali halisi, tanakali sauti hii hutumiwa kama njia mojawapo ya kuwaashiria watu wamanyamaze.

### 4.2.5 Taswira

Taswira hujitokeza pale ambapo mbinu ya maelezo imetumika vizuri kuwaelezea wahusika, mandhari au matukio tofauti tofauti. Ni mbinu muhimu katika kazi za watoto kwa sababu inaamsha ile hali yao ya fikra ambapo wanaweza kuwa na

picha kamili kuhusu kile kinachoelezewa. Pia ni muhimu kwa watoto kwani huenda ikaibua hisia fulani kwake pale ambapo anaathirika na kuonyesha msimamo wake kuhusu tukio, mazingira au mhusika fulani. Mtafsiri ametumia mbinu ya taswira pale ambapo anawaelezea Mfalme Twala na Mhusika Gagula. Katika uk.74, mwandishi anamwelezea Mfalme Twala kama ifuatavyo,

> ...Alikuwa mkubwa kabisa na sura yake ilichukiza kupita sura zote tulizoziona. Midomo yake ilikuwa minene mno, pua yake imebonyeka, na alikuwa na jicho moja tu lililong'aa. Jicho lingine hana ila tundu tu...

Kulingana na maelezo haya, msomaji anaweza kupata taswira ya mtu ambaye umbo lake ni kama la zimwi ambao husimuliwa katika ngano za hadithi simulizi. Mhusika Gagula ameelezewa kwa njia ifuatayo katika uk.78,

> Alikuwa mwanamke kizee sana sana, na uso wake umekunjika mno kwa uzee hata kuwa kama uso wa mtoto mchanga wenye mikunjo mingi. Kinywa chake kilikuwa kama ufa katika mikunjo hiyo, na chini ya ufa, kidevu chake kilitokeza kama ncha. Alikuwa na pua ndogo na kama macho yake yasingalionekana, uso wake usingalikuwa kama wa uso wa maiti uliokauka kwa kuwekwa juani. Lakini macho yake yaling'aa kama mwenye akili nyingi. Kichwa chake kilikuwa kipara, hana unywele kabisa, na ngozi ya utosini iliyokunjana ikimeta kama ngozi ya nyoka.

Maelezo haya yanampa msomaji taswira ya kiumbe ambaye hapendezi na anachukiza. Hisia kama hizi zina athari zake katika maisha ya mtoto pale ambapo atawachukia wachawi katika jamii na hangependa kamwe kuhusishwa nao wala vitendo vyao maishani.

### 4.2.6 Taharuki

Taharuki ni mbinu muhimu katika kazi za watoto kwa sababu humpa mtoto hamu ya kutaka kuendelea kuisoma hadithi kurasa baada ya kurasa ili aweze kuyafahamu yaliyojiri baadaye. Hadithi hii imejaa matukio yenye kujenga taharuki ya msomaji. Kwa mfano, mtoto angetaka kujua kama akina Bw. Henry walifanikiwa kumpata ndugu yake na iwapo walifanikiwa, walimpata wapi? Je alikuwa yu hai au yu maiti?. Pia mtoto angetaka kujua kama Bw. Henry na wenzake walifanikiwa kulivuka lile jangwa na kama walifanikiwa kuyapata yale mashimo ya Sulemani. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yatamtia mtoto azma ya kutaka kuendelea kukisoma hiki kitabu.

Mtafsiri amefanikiwa kuijenga na kuiendeleza taharuki ya mtoto tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi na hatimaye kumtuliza mtoto pale ambapo hadithi inaishia baada ya Bw. Henry na wenzake kufanikiwa katika kumpata ndugu yake.

### 4.2.7 Ucheshi

Mbinu hii hutumiwa ili kuwafanya wasomaji waburudike. Ni mbinu muhimu katika kazi za watoto kwa kuwa huwafanya watoto waifurahie kazi wanayoisoma. Kwa mujibu wa Weche (2000), ucheshi ndiyo mbinu nzuri zaidi ambayo mwandishi anaweza kuitumia ili kuwafurahisha watoto na kuwafanya wamakinikie hadithi wanayoisoma. Mbinu hii inaweza kujitokeza katika kazi za watoto kupitia kwa michoro, maelezo kuhusu jambo fulani au pia katika nyimbo. Kwa mfano katika uk.63 Bw. Henry anamwambia Bw. Good:

> Tazama Bw. Good, ulipofika nchi hii wenyeji wameona ni tabia yako kuwa hivi, na sasa lazima udumu hivi. Hufai kabisa kuvaa suruali tena. Tokea sasa lazima uvae shati na viatu na miwani yako tu basi.

Kwa hivyo kwa siku nyingi zilizofuatia, Bw. Good hakuvaa suruali bali alikaa bila suruali. Ingawa jambo hili linaonyesha jinsi Wazungu wanamdhalalisha Mwafrika, kwa mtoto, mtu mzima kukaa bila suruali ni jambo ambalo linaweza kuwachekesha.

### 4.2.8 Nyimbo

Wimbo hutumika katika kazi za fasihi kama njia moja ya kuwaburudisha wasomaji. Nyimbo huwapa burudani watoto kwa sababu watoto wanazichukulia kuwa ni matamshi ya muziki na kwa hivyo wanahusika katika kuziimba. Wanaweza kubuni lahani zao wenyewe au wakatumia lahani wanazozifahamu ili kuziimba zile nyimbo. Kwa hivyo, mwandishi wa kazi za watoto anafaa kuzisimilisha nyimbo zilizotumiwa katika matini chasili ili ziwe na wizani ndipo ziweze kuimbika na kuambatanishwa na vitendo kama vile kupiga makofi au pia miondoko fulani na mtoto anayelengwa. Kwa hivyo, nyimbo hukuza ubunifu wa mtoto na huondoa uchovu wa kusoma matini kwa mfululizo.

Katika matini lengwa, Mtafsiri ametumia nyimbo mbili, mmoja katika uk.88 ambao ni wimbo mfupi wa majibizano pale ambapo sauti moja inaongoza na wengine wanajibu kama ifuatavyo,

> Sauti: Nini ajali ya mtu azaliwaye.
> Jibu: Mauti.........!

Wimbo huu ni mfupi na utawapendeza watoto kwani ni wimbo wa majibizano. Wimbo ulioimbwa na Ignosi (uk.132) baada ya kushinda vitani ni mrefu sana kiasi kuwa haumvutii msomaji, umeimbwa na mtu mmoja na maneno yake hayana wizani. Wimbo huwa wimbo kwa sababu ni maneno yanayotamkika kwa sauti ya muziki. Kwa hivyo, maneno haya yanatarajiwa yawe na wizani ndiposa yaweze kuimbika. Mtafsiri hakufaulu katika kuusimilisha huu wimbo. Mtoto hataufurahia kwa sababu ni mrefu mno na unaonekana kama sehemu ya matini. Mwandishi angeufupisha na pia, angeyafanya baadhi ya maneno kuwa na wizani au yarudiwe rudiwe ili yavutie mtoto na yaimbike. Vile vile, angeufanya kuwa wimbo wa mapokezano baina ya mhusika Ignosi na wafuasi wake ambao bila shaka walifurahia ushindi wao, hali ambayo mtoto angeifurahia na kushiriki.

#### 4.2.9 Tasfida

Hii ni mbinu ya kutumia lugha iliyochujwa ili maneno yanayokihiri yasitumike. Katika kila jamii, kuna miiko na makatazo ya kutumia lugha ya wazi hasa kuhusiana na uchafu wa matusi au karaha ya aina fulani. Mwandishi wa kazi za watoto hana budi kutumia lugha yenye adabu kwa sababu fasihi ya watoto kama fasihi kwa jumla ina jukumu la kumfundisha mtoto maadili ya jamii. Pia, mtoto huwa katika hali ya ukuaji kimwili, kisaikolojia na hata kilugha ambapo mara nyingi mtoto hutumia ile lugha ambayo amejifunza kutoka kwa jamii, mazingira na pia fasihi anayoisoma.

Ikiwa lugha ya matusi imetumika katika matini chasili, mtafsiri wa matini lengwa hana budi kuiondoa kwenye matini yake. Katika uk.75 Mfalme Twala anamwita kijana ambaye ngao yake ilianguka *'mbwa',* (uk.93), Mfalme Twala anaiita miili ya waliouawa katika vita *'mbwa'* na (uk.139) Ignosi anamwita *'Gagula mbwa jike'.* Hii ni lugha ambayo inaudhi na haikubaliki katika jamii ya Waswahili na hasa watoto. Mtafsiri wa matini lengwa angeichuja lugha hii kwa kutumia maneno mengine au aiondoe sehemu hiyo kabisa.

## 4.3 Usimulizi

Mwandishi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza ambapo Bw. Quatermain ndiye msimulizi – mwandishi. Amefaulu katika kuteka akili za mtoto na kumfanya aambatane naye katika safari yake pamoja na wenzake. Hali hii inaujenga uhusiano wa karibu baina ya msimulizi na mtoto. Aidha, mtoto anaweza kufuata mtiririko wa hadithi na pia kuielewa, jambo linalojenga hamu ya mtoto ya kutaka kuendelea kuisoma hadithi hii.

## 4.4 Wahusika

Usimilishwaji wa wahusika katika kazi za watoto ni jambo muhimu sana kama ilivyojadiliwa katika sura ya pili (taz. uk.36). Sehemu hii imehakiki usimilishwaji wa baadhi ya wahusika ambao wametumiwa kuendeleza na kufanikisha hadithi hii.

### 4.4.1 Bwana Quatermain

Ni mwindaji hodari. Kazi yake ilikuwa ni kuwawinda ndovu ili kupata pembe zao na kuziuza. Uhodari wake unadhihirika pale alipowaongoza wenzake kuwawinda ndovu wakiwa safarini kwenda kumtafuta ndugu yake Bw. Henry. Ni mtu jasiri. Aliweza kukabiliana na wanyama hatari wa porini alipokuwa akiwinda. Anasema amewahi kuwauwa simba sitini (uk.2). Ujasiri wake pia unadhihirika pale anapowaongoza wenzake kulivuka lile jangwa kubwa lenye hatari nyingi.

### 4.4.2 Mfalme Twala.

Ndiye mfalme wa Wakukuana. Nguvu zake na uwezo mkubwa ambao anao unatokana na yule mchawi Gagula ambaye anabashiri mambo na kumshauri mfalme kuhusu hatua atakayoichukua. Ni mfalme katili ambaye anapenda kumwaga damu. Aliamrisha kuuawa kwa askari ambaye aliiangusha ngao yake kwa bahati mbaya. Pia anashuhudia umwagikaji wa damu ya mamia ya watu wakati wa sherehe ya kuwatambua wachawi. Ana tabia ya kutumia lugha ya matusi hasa pale anapowazungumzia wananchi anaowatawala. Kwa mfano, anasema katika (uk.75):

> Mbwa wewe usiyeangalia, ngao yako
> Ndiyo aliyoanguka........

Vile vile, anatumia lugha ya matusi anapotumia neno 'mbwa' (uk.93) kuirejelea miili ya watu waliokuwa wameuawa.

### 4.4.3 Gagula.

Ni mhusika ambaye ni mwovu na ni mchawi. Ni ajuza ambaye ameishi miaka mingi sana kuliko wenyeji wa nchi ya Wakukuana. Gagula ni msaidizi mkubwa wa mfalme Twala hasa katika kutekeleza maovu, (uk.136). Kwa kutumia nguvu za uchawi, anashirikiana na wanawake wengine ili kuwatambulisha wale ambao watauawa katika sherehe ya *'ngoma kuu ya kufichua wachawi'.* Kupitia nguvu za uchawi, anaweza kubashiri mambo ambayo yatatokea na kisha yanatokea kama alivyobashiri. Alibashiri kuhusu umwagikaji wa damu katika nchi ya Wakukuana, jambo ambalo lilitokea wakati wa vita baina ya Umbopa na Mfalme Twala. Ni mwenye ujuzi mwingi ambao labda unatokana na kule kuishi kwingi kwake. Ndiye pekee anayejua wale watu waliojenga barabara kuu ya Suleimani na anafahamu siri zote za yale Mashimo ya Sulemani kama jinsi ya kuufungua ule mwamba wa chumba cha mauti.

### 4.4.4 Bwana Good.

Ni mhusika aliyeandamana na Bw.Henry na Bw. Qutermain katika safari yao. Ni mwenye huruma. Anaonyesha hisia za huruma wakati Khiva alipojeruhiwa vibaya na kuuawa na tembo. Vivyo hivyo alimhurumia Foulata aliyeuawa na Gagula walipokuwa ndani ya Mashimo ya Sulemani. Hakati tamaa haraka akilinganishwa na wenzake. Wakati Bw. Quatermain na Bw. Henry walipokata tamaa ya kupata njia ya kutoka mle ndani mwa chumba cha mauti, Bw. Good alijitahidi kuendelea kutafutatafuta kama angepata njia yoyote. Mwishowe alifanikiwa na wote wakaweza kutoka nje. Ni mwenye hekima. Anawashauri wenzake wachimbe

shimo, waingie ndani na wajifunike na majani ili kuliepuka joto kubwa la jangwani, (uk.41).

### 4.4.5 Umbopa

Ni mhusika aliyehiniwa urithi wake na mfalme Twala. Aliandamana na akina Bw. Quatermain safarini huku akiwahudumia kama mtumishi wao. Ni mhusika shupavu. Alielewa kuwa ndiye alikuwa mfalme halali wa Wakukuana hivyo basi akafanya azimio la kurudi katika nchi ya Wakukuana, kupigania haki yake na mwishowe aliuchukua uongozi.

Ni mwenye haki. Aliwaahidi Wakukuana kuwa iwapo angeshika hatamu kama mfalme, angepiga marufuku sherehe ambazo zinaambatana na umwagikaji wa damu ya watu wasiokuwa na hatia. Aidha aliwaahidi kuwa hukumu ingetolewa kwa njia ya haki kwa wale ambao wangepatikana na hatia.

Ni mhusika jasiri. Aliweza kuwaongoza wafuasi wake vitani na kuwatia moyo wa kupigana mpaka wakashinda. Ujasiri wake pia unajitokeza pale ambapo anawashauri na kuwapanga askari wake katika vikosi tofauti tofauti na kisha kuwapa maarifa ya jinsi wangelishambulia jeshi la mfalme Twala.

### 4.4.6 Bw. Henry

Huyu ndiye mhusika aliyefunga safari kwenda kumtafuta ndugu yake.

Ni shujaa wa vita. Alijitolea kupigana na mfalme Twala ambaye alikuwa akiogopwa katika nchi nzima ya Wakukuana na akaweza kumshinda na hata

kumuua. Ni mwenye nguvu. Amepewa jina Ndovu kwa sababu ya nguvu alizokuwa nazo. Nguvu zake ziliwasaidia Bw. Good na Bw. Quatermain kuliinua lile jiwe kubwa, (uk.157).

Mtafsiri hakuwafanyia marekebisho mengi wahusika wa matini chasili. Amewapa majukumu kama yale waliyopewa katika matini chasili. Hakupunguza wala kuongeza idadi ya wahusika bali ametumia idadi ile ile ambayo imetumika katika matini chasili. Baadhi ya marekebisho waliyofanyiwa ni kuyasimilisha baadhi ya majina ya wahusika ili yaambatane na sarufi ya lugha pokezi ingawa mengine aliyahamisha tu kama yalivyo kutoka matini chasili hadi katika matini lengwa.

Kwa mujibu wa Mdee (1986), sababu moja ya kuunda majina mapya ni kule kurahisisha uzungumzaji pale ambapo maneno mapya huundwa kutokana na yale yaliyopo. Mwandishi ameyaunda majina kutokana na yale ya matini chasili akiwa na nia ya kurahisisha matamshi yake ili yawafae wasomaji wanaolengwa na pia waweze kuyakumbuka kwa urahisi. Mwandishi ametumia mbinu ya ukopaji wa utohozi pale ambapo amebadili maumbo ya maneno yaliyokopwa ili yakubaliane na mfumo wa lugha pokezi. Kwa mfano,

| <u>wahusika katika matini chasili</u> | <u>wahusika katika matini lengwa</u> |
|---|---|
| Gagaoola | Gagula |
| Macumazahn | Makumazahn |
| Silvestra | Silvestre |
| Scragga | Skraga |
| Infadoos | Infadus |

Baadhi ya majina ya wahusika ambayo hayakufanyiwa marekebisho yoyote ni pamoja na Umbopa, Khiva, Jim, George, Bw.Quatermain, Bw. Good, Bw. Henry, Mfalme Twala na Foulata.

Hata hivyo, mtafsiri hakufanikiwa kuufanya usimilishwaji wa majina haya kwa sababu hata baada ya kuyafanyia marekebisho, bado hayakuambatana na mfumo wa sarufi ya lugha ya Kiswahili labda tu yale ya wahusika Gagula, Mfalme Twala na Foulata. Angeyasimilisha zaidi yale majina ya Waafrika ili yachukue mfumo wa lugha iliyotumika katika matini lengwa ambayo ni Kiswahili. Kwa mfano, majina kama, 'Makumazahn', 'Silvestre', 'Skraga' na 'Infadus' angeyafanya yatamkike kama 'Makumazani', 'Silivesta', 'Sikiraga' na 'Inifadusi'.

Mtafsiri vile vile hakufanikiwa kuwasimilisha wahusika kutokana na ukosefu wake wa udhabiti anapowarejelea wahusika katika matini lengwa. Baadhi ya wahusika wamerejelewa kwa majina tofauti katika baadhi ya kurasa jambo ambalo linamkanganya mtoto. Kwa mfano, mhusika 'Naville' ndiye bado mhusika 'George', 'Bw. Henry' ndiye 'Ndovu', 'Bw. Good' ndiye 'Bougwan', 'Bw. Quatermain' ndiye 'Makumazahn' na 'Umbopa' ndiye 'Ignosi'.

Mtafsiri anamkanganya mtoto zaidi pale ambapo anatumia majina yote mawili ya mhusika na wakati mwingine anatumia jina moja tu kati ya yale mawili kumrejelea mhusika yuyo huyo. Wakati mwingine anaambatanisha jina la mhusika na anwani na wakati mwingine analitumia jina la mhusika yuyo huyo

bila kuliambatisha na anwani yoyote. Kwa mfano, mhusika Bw. Henry wakati mwingine amerejelewa kama Bw. Henry Curtis, mhusika Jose da Silvestre anarejelewa wakati mwingine kama Marehemu Jose au pia Mzee Silvestre, mhusika Gagula ameitwa Kizee Gagula au pia mchawi mwanamke Gagula na Bw. Quatermain amerejelewa kama Bw. Allan au Alan Quatermain. Kule kutofuatilia mtindo mmoja wa kuwarejelea wahusika wake kunaifanya matini lengwa kuwa ngumu kufuatiliza wahusika wake.

Aidha, mwandishi amewatumia wahusika wengi sana katika matini lengwa ambao wanawakanganya wasomaji. Si rahisi kwa msomaji kuwakumbuka baadhi ya wahusika hawa na majukumu yao katika hadithi hata baada ya kuisoma hadithi ile. Kwa mfano, wahusika kama vile Evans, Goza na Tom miongoni mwa wengine. Mwandishi angepunguza idadi ya wahusika hawa kwa kuondoa baadhi yao ambao hata wakiondolewa kwenye hadithi, hadithi bado itakuwa na mtiririko na kiini chake kitabaki vile vile. Kwa jumla, usimilishwaji wa wahusika katika matini lengwa haukujitokeza vizuri.

## 4.5 Maudhui

Kazi za watoto zinatakiwa kuwa na maudhui mepesi ambayo mtoto atayaelewa moja kwa moja. Maudhui haya yanatakiwa kumfundisha mtoto maadili. Katika matini lengwa kuna maudhui mbalimbali ambayo yamejitokeza;

### 4.5.1 Ushujaa

Ushujaa ni maudhui ambayo huwavutia watoto sana. Watoto hupendezwa na maudhui haya kwa sababu wanajitambulisha na mashujaa na ushindi wao. Mashujaa wa kiutamaduni hupewa sifa za uhalisiajabu ambazo huwavutia watoto. Hawa ndio wahusika ambao wanatumika katika matini lengwa ambao wanakumbana na mambo ya ajabu ajabu na kupitia ushujaa wao wanaweza kuibuka washindi. Baadhi ya wahusika hawa ni Bw. Quatermain, Bw. Good, Bw. Henry na Umbopa. Mwandishi ameonyesha namna mbalimbali za jinsi sifa ya ushujaa inajitokeza miongoni mwa wahusika hawa:

#### 4.5.1.1 Ushujaa wa Safari

Ushujaa unajitokeza pale ambapo Bw. Quatermain na wenzake wanaamua kusafiri safari ambayo ilikuwa ya hatari mno na ambayo walijua kuwa aidha wangekufa kabla ya kuikamilisha au wanusurike kifo. Kule kuivumilia njaa, kiu, baridi na mashambulio ya wanyama ni kitendo cha ushujaa pia. Hatimaye waliweza kufanikiwa kuimaliza safari yao. Hiki kitendo cha kuamua kusafiri na kukabiliana na yale yangewajiri njiani ni kitendo chenye kuvutia watoto.

#### 4.5.1.2 Ushujaa wa Kugundua Mambo

Bw. Quatermain na wenzake wanaonyesha ushujaa wa hali ya juu pale ambapo waliweza kuponyoka mauti mle mashimoni mwa Sulemani. Kutokana na itikadi za Wakukuana, hakuna aliyeingia mahali pale na akaishi. Kwanza kabisa ilionekana kama Bw. Quatermain na wenzake hawangeishi tena baada ya kufungiwa na ule

mwamba katika mahali pa mauti na hawakujua jinsi ya kuufungua ili watoke. Hatimaye waliweza kujiokoa kwa njia ya ajabu pale walipogundua mwanya ambao waliufuata kwa shida mpaka wakatoka nje.

#### 4.5.1.3 Ushujaa wa Ulengaji Shabaha

Ulengaji shabaha hodari unajitokeza wakati Bw. Good alimpiga risasi twiga akiwa mbali na kumuua, wakati Bw. Quatermain alimpiga swala risasi kwa mbali na pia pale Bw.Henry alipompiga risasi ng'ombe. Vitendo hivi ni vya kishujaa ambavyo vinaweza kuwavutia watoto hasa wa kiume. Watoto hawa wanapenda michezo ya uwindaji sana ambapo wakati mwingine wanatumia mawe au panda ili kulilenga shabaha windo lao.

### 4.5.2 Maadili

Fasihi ya watoto hutumiwa kama nyenzo ya kuendeleza maadili ya kijamii. Maudhui haya hujenga uadilifu miongoni mwa watoto na hukashifu vitendo vinavyokiuka uadilifu kama vile ukatili, uchoyo na ubinafsi. Maswala ya uadilifu ambayo yamezungumziwa katika kazi hii ni pamoja na:

### 4.5.3 Upendo.

Swala la upendo ni jambo muhimu katika kazi za watoto. Mtoto anapoonyeshwa mapenzi na familia yake, shuleni na hata jamii kwa jumla hujihisi akiwa yu salama. Maudhui ya upendo humfunza mtoto jinsi ya kuishi katika maisha ya undugu kati yake na wanajamii wale wengine.

Maudhui haya yanaendelezwa na wahusika kama vile Bw. Quatermain, Umbopa, Bw. Good, Bw. Henry, Infadus na Foulata katika matini lengwa. Ni kwa sababu ya upendo ambapo Bw. Henry anajitolea kwenda kumtafuta ndugu yake aliyekuwa amepotea. Uhasama uliokuwepo baina yao umesahaulika na wanapokutana tena wanakumbatiana kama ndugu. Bw. Quatermain anaonyesha kitendo cha upendo pale ambapo anakubali kuandamana na wenzake ili awasaidie kwenda kumtafuta ndugu yake Bw. Henry. Bw. Good anatenda kitendo cha upendo anapomwokoa Foulata kutoka mikononi mwa wauwaji. Vitendo hivi vyote vinamwonyesha mtoto kuwa upendo huzaa matunda mema.

### 4.5.4 Fadhila.

Maudhui kama haya humfunza mtoto jinsi ya kutendeana matendo mema miongoni mwa wanajamii. Yanakuza ile hali ya kuleta utangamano baina ya watu katika jamii. Humtoa mtoto katika ule ulimwengu wake ambapo anakiona kila kitu kuwa chake hadi ulimwengu ambapo anafunzwa jinsi ya kushirikiana na wenzake katika jamii. Bw. Quatermain na wenzake walishirikiana na kugawana chakula na maji baina yao walipokuwa safarini na waliishi kama ndugu. Mwandishi anasema, '*...tulikula chakula chetu kwa mwangaza...*' (uk.27) Matumizi ya kiambishi *'tu-'* yanaonyesha wingi, kuwa wote kwa jumla walishiriki. Zaidi ya hayo, walisaidiana mmoja na mwingine. Bw. Quatermain na wenzake walimsaidia Umbopa kumng'oa Mfalme Twala mamlakani ilhali naye Umbopa alikuwa amewasaidia kwa kuwatumikia wakiwa safarini. Bw. Good alimsaidia Foulata pale ambapo alitaka kuuawa naye Foulata kwa upande ule mwingine

akamuuguza Bw. Good aliposhikwa na maradhi. Hivi ni vitendo vya fadhila na mtoto anahimizwa kuyatenda matendo kama haya katika jamii.

### 4.5.5 Umoja

Haya maudhui yanamhimiza mtoto kuwa na mapatano mema na wanajamii. Mwandishi amefaulu kumwonyesha msomaji anayelengwa umuhimu wa umoja katika jamii. Ameonyesha jinsi jambo lolote linalofanywa kwa umoja huwa linafaulu. Msomaji anafundishwa kuwa umoja ni nguvu. Katika uk.157, mwandishi anaonyesha jinsi umoja baina ya Bw. Quatermain na wenzake uliwafaulisha kuliinua lile jiwe kubwa ambapo walipata njia iliyowasaidia kutoka mle ndani mahali pa mauti. Mwandishi ametumia maneno yafuatayo kuonyesha namna waliungana,

> 'Haya! Vuteni! Vuteni! Inalegea!' Nasikia mishipa yake ikidata kwa nguvu. Mara tulisikia sauti ya kukwaruza, mara sote tulianguka nyuma pande la jiwe kubwa likaruka juu.....

Pia umoja wa askari wa Ignosi pamoja na wafuasi wake uliwapa ushindi dhidi ya Mfalme Twala na wafuasi wake. Umoja wa Bw.Quatermain pamoja na wenzake wakiwa safarini ndio uliwawezesha kufaulu kuvuka misitu, jangwa na hata milima na mwishowe kufaulu. Kwa jumla, mwandishi amefaulu katika kumwonyesha msomaji anayelengwa umuhimu wa umoja miongoni mwa wanajamii.

### 4.5.6 Haki

Hii ni hali ya uendeshaji wa mambo kwa kufuata inayostahiki. Palipo na haki pana usawa na amani. Watoto ni binadamu wanaopenda kuona haki ikitekelezwa. Wanaamini kuwa uzuri unafaa kutuzwa na uovu uadhibiwe vilivyo. Hata hivyo, pindi wanavyoendelea kukua, ni wajibu wa jamii kumfunza mtoto jinsi haki inavyotekelezwa. Inamfanya mtoto ajue kuwa, si lazima haki itekelezwe kwa namna ya 'jicho kwa jicho' kama anavyotazamia iwe bali inaweza kutekelezwa kwa njia mbali mbali. Njia moja ya kumfunza mtoto ni kupitia fasihi yao. Mwandishi wa matini lengwa ameonyesha jinsi haki itatekelezwa na Iginosi. Kwa mfano, ikiwa Iginosi angechukua uongozi, basi angekomesha ile sherehe ya kuwafichua wachawi inayoambatana na umwagikaji wa damu. Anasema katika uk.109,

> ...nikiishi kukaa juu ya kiti cha enzi cha babu zangu, kumwaga damu ya bure kutakoma...kila mtu atalala salama katika nyumba yake bila hofu, na haki itazagaa katika nchi yetu yote.

### 4.5.7 Ukatili

Ukatili ni kitendo ambacho ni kinyume na maadili ya jamii. Ni kitendo kiovu na kinaambatana na maovu katika jamii na kwa hivyo kinakemewa. Mwandishi ameonyesha uovu na ukatili pale ambapo hukumu maalum inatolewa kwa Mfalme Twala na Gagula. Baada ya kuwaua watu wengi wasiokuwa na hatia, ambacho ni kitendo cha ukatili, hatimaye Mfalme Twala anauawa na pia Gagula anakufa kifo cha ajabu pale anapopondwapondwa na ule mwamba mpaka

anafariki. Mwandishi amefaulu kutimiza matarajio ya mtoto kuwa uovu uadhibiwe.

## 4.6 Umbo la Kitabu

Umbo la kitabu hujumuisha mambo ya uchapishaji kuliko uandishi. Hata hivyo huwa ni jambo muhimu katika fasihi ya watoto (taz. sura ya pili uk.42-47). Sehemu hii imehakiki jinsi usimilishwaji wa umbo la kitabu umefanywa.

### 4.6.1 Vielezo (michoro)

Kulingana na nadharia ya Elimumitindo, michoro ni njia moja ya kutumia lugha ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa msomaji. Kwa hivyo, michoro inapokuwa imetiwa rangi au la, hutumiwa kutoa ufafanuzi zaidi wa hadithi yenyewe. Kitabu hiki kina mchoro wa jalada na michoro iliyoko katika matini.

#### 4.6.1.1 Mchoro wa Jalada

Mchoro huu umetiwa mchanganyiko wa rangi (taz. kbt. 1). Kwa mujibu wa Cass (1967), rangi ni jambo muhimu katika vitabu vya watoto. Watoto hupendezwa na huvutiwa na kitabu kilicho na michoro iliyotiwa rangi kuliko kile chenye michoro isiyotiwa rangi. Hata hivyo, kitabu hakivutii tu kwa sababu ya rangi, bali rangi ambazo hupendeza macho na zilizo na upatanifu na mchoro wenyewe. Michoro yafaa idhihirike na kutambulika kwa wepesi na watoto.

Ijapokuwa jalada la kitabu hiki lina mchoro uliotiwa rangi, mchoro huu una uluwiluwi unaotokana na mchanganyiko wa rangi zilizotumiwa kiasi kuwa si rahisi kutambua ni nini hasa kilichoko kwenye ule mchoro moja kwa moja. Fauka ya hayo, hapana upatanifu baina ya anwani ya kitabu na mchoro ulioko kwenye jadala la kitabu. Ule ukosefu wa upatanifu unaweza kukatiza azma ya mtoto ya kukisoma kitabu hiki.

#### 4.6.1.2 Michoro ya Matini

Michoro iliyojumuishwa katika matini haikutiwa rangi, (taz. vbt. 2 – 8). Aidha michoro hii haipendezi wala kuvutia macho kwa sababu inaonekana kama inayofifia na haionekani vizuri. Watu waliochorwa tangu mwanzo hadi mwisho wa kitabu wanaonekana kama sanamu na wasio na uhai. Isitoshe, wanaonekana kama watu wa kale mno. Kulingana na Cass (1967), watoto huvutiwa macho na kile ambacho wanakifahamu katika michoro.

Huenda michoro ya matini hii isiwavutie wala kufahamika na watoto kutokana na jinsi ilivyochorwa. Kwa mfano, Wazungu Bw. Good, Bw. Henry na Bw. Quatermain wamechorwa kwa njia tofauti sana na wale Wazungu ambao watoto wa siku hizi wanawafahamu. Kadhalika, maelezo kuhusu Umbopa (uk.25) kuwa alikuwa *'mwekundu'* wala si mweusi sana hayaeleweki kwa sababu mara nyingi watu huambatanishwa na aidha weupe au weusi. Maelezo haya yanakinzana na mchoro ambapo Umbopa amechorwa akiwa mweusi ti! Hakuna hata dalili ya wekundu mwilini mwake (taz. kbt. 2). Vile vile, michoro hii imejitenga na uhalisi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

pale ambapo Waafrika wamechorwa wakiwa nusu uchi (Taz. kbt. 2,3,6) jambo ambalo ni taasubi ya kikoloni.

Kwa jumla, mwandishi ingawa amepatanisha maelezo ya hadithi na michoro, hakufaulu kuisimilisha hii michoro. Pana pengo kubwa sana lililoko baina ya mchoro ulioko katika jalada ambao umetiwa rangi na michoro iliyojumuishwa katika matini ambayo haikutiwa rangi. Pengo hili linakatisha matarajio ya mtoto na linaweza kukatisha azma yake ya kukisoma kitabu hiki. Ili kuzuia haya kutokea, mwandishi angetia rangi ile michoro ili iwe sawa na ule wa jalada.

### 4.6.2 Umbo la Nje la Kitabu.

Kitabu kizuri cha watoto kulingana na Cass (1967) kinatakiwa kuwa na ujalidi na jalada imara. Jalada la kitabu hiki ni dhabiti kwa hivyo hakiwezi kuchakaa haraka. Ujalidi wa kurasa umefanywa kuwa dhabiti kiasi kuwa msomaji ataweza kukisoma kitabu vizuri bila wasiwasi wa kukiharibu.

### 4.6.3 Aina ya chapa.

Maandishi ya chapa aliyoyatumia mchapishaji ni ya wastani. Mtoto anaweza kuyasoma bila kukazika macho. Hata hivyo aina ya karatasi iliyotumiwa kupigia chapa ni ya hali duni. Inafanya maandiko yaonekane kama yasiyong'aa na kama yamechakaa na kwa hivyo kutomvutia mtoto. Fauka ya haya, mchapishaji aliacha pambizo nyembamba sana katika pembe zote za karatasi jambo ambalo linayafanya maandiko yake yaonekane kama yanayosongamana na hivyo basi

kutopendeza. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yanafaa kutiliwa maanani wakati wa usimilishwaji.

## 4.7 Hitimisho

Sehemu hii imeshugulikia usimilishwaji wa kitabu cha *Mashimo ya Mfalme Sulemani.* Kitabu hiki kilisimilishwa na mzungu wakati wa ukoloni ili kiweze kusomwa na watoto shuleni. Vipengele kama vile ploti, lugha, wahusika, maudhui na umbo la kitabu vimejadiliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Elimumitindo. Ploti imejadiliwa kwa kuonyesha jinsi matukio na sura zinafuatana. Kipengele cha lugha kimejadiliwa kupitia tamathali za usemi kama vile tashbihi, tashihisi, taswira, taharuki, tanakali sauti, vihisishi na nyimbo. Aidha tabia na sifa za wahusika zimeshugulikiwa, na michoro pia. Kadhalika, mafanikio na udhaifu wa mtafsiri katika kusimilisha kitabu hiki ni baadhi ya mambo ambayo yameshugulikiwa.

Sura ifuatayo imeshughulikia usimilishwaji wa riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo.* Sehemu hii imehakiki lugha na matumizi yake, ploti ya hadithi, wahusika, maudhui na umbo la kitabu.

# SURA YA TANO

## Usimilishwaji wa Riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo*

### 5.0 Utangulizi

Sura hii, imehakiki jinsi Matundura (2001) ameisimilisha kazi yake inayoilenga hadhira ya watoto. Mtafiti ametumia shairi la *Utendi wa Fumo Liyongo* kutoka katika *Kusanyiko la Mashairi* (Jahadhmy, 1975) kama matini chasili. Shairi hili linauwiano mkubwa na riwaya ya Matundura (khj).

Tenzi ni masimulizi marefu ambayo hubeba maudhui moja kuu. Huwa na ploti ndefu ya moja kwa moja yenye mpangilio wa beti zenye mishororo iliyo na sehemu moja tu. Akiyaungama haya, Nabhany katika utangulizi wa diwani ya *Malenga wa Karne Moja* ya Chiraghdin (1987) anasema kuwa tenzi hutumiwa kwa kusimulia hadithi za mashujaa na ndiyo bahari ya pekee inayoweza kuelezea jambo kwa urefu sana.

Kuna maoni mbalimbali kuhusu asili ya *Utendi wa Liyongo.* Baadhi ya wahakiki wana maoni kuwa Liyongo mwenyewe ndiye aliyeutunga utendi huu. Hawa ni pamoja na Chiraghdin (1987), Knappert (1979), Jahadhmy (1975), Mbele (1986) na Radhiwani (1996). Kulingana na Mbele (1986), utendi huu ulikuwa mrefu sana na ulihifadhiwa katika kumbukizi za jamii kama wimbo ambao kulingana na Knappert (1979), ulikuwa unaimbwa katika sherehe za harusi. Kule kutohifadhiwa kwa utendi huu katika maandishi ndiko kulingana na Mbele (1986)

kulisababisha baadhi ya beti zake kusahaulika na pia kuwepo kwa tafsiri nyingi tofauti za utendi huu. Hii ni kwa sababu waliouhifadhi utendi huu katika maandiko walitegemea fasihi simulizi ya Waswahili wa mwambao wa pwani. Kulingana na Wamitila (2002), utendi huu uliandikwa kwa mara ya kwanza na Mohamadi Kijumwa katika mwaka wa 1913 ambaye alipata hadithi ya Fumo Liyongo kutokana na migani ya jamii ya Wapokomo na jamii zingine za Waswahili wa mwambao wa pwani.

Kwa mujibu wa Jahadhmy (1975), Fumo Liyongo aliishi kisiwani Pate kati ya karne ya kumi na saba na kumi na nane ingawa kama asemavyo Wamitila (2002), tarehe na wakati ambapo Fumo Liyongo aliishi na wakati utendi huu ulitungwa ni jambo linalotatanisha. Mpaka sasa hakuna ithibati ya kihistoria ya kutegemewa kuhusu wakati alioishi Liyongo na pia kuhusu wakati wa kutungwa kwa utendi huu. Wanachokubaliana wahakiki akiwemo Matundura (2001) ni kuwa, Liyongo ni mtu aliyeishi katika kipindi fulani cha kihistoria na alikuwa mshairi maarufu na pia shujaa wa vita aliyesifika sana. Kulingana na Jahadhmy (1975), utendi huu uliimbwa katika sherehe za Waswahili na Wapokomo na uliendelea kuimbwa hata baada ya kifo cha Liyongo. Akikubaliana na haya, Wamitila (2003) anasema kuwa, *Utendi wa Fumo Liyongo* ungali unasimuliwa kama migani katika jamii ya Waswahili na Wapokomo mpaka sasa.

Utendi huu unasimulia jinsi Liyongo alivyokuwa na sifa na uwezo wa kipekee ambao ulimpelekea kusifiwa na kuogopwa sana na watu wa jamii yake na pia

watu wa jamii jirani. Liyongo alikuwa na umbo la kupendeza na watu kutoka mbali walikuja kulitazama lile umbo lake na kuliajabia. Alikuwa shujaa wa vita na sifa za ushujaa wake zilienea mpaka nchi ya Wagalla. Wagalla ndio waliokuwa wamesifika sana katika vita na walikuwa wanaogopwa sana na jamii zingine. Hata hivyo ushujaa wa Liyongo uliwababaisha kiasi kuwa walimwogopa sana akiwemo sultani wa Pate aliyehofia kuwa Liyongo angemng'oa mamlakani, jambo lililomfanya atafute njia za kumwangamiza Liyongo.

Liyongo alipogundua njama hiyo, alitorokea bara kwenye jamii ya Wasanye na Wadahalo. Sultani alipogundua haya alifanya njama na Wasanye na Wadahalo ili wamuue Liyongo. Walitumia hila kuwa Liyongo aupande mkoma mrefu ili awaangulie makoma pale ambapo wangemfuma mishale na kumuua. Liyongo kwa ajili ya hekima yake aliweza kugundua njama hiyo na akakataa kuupanda ule mkoma, badala yake akatumia uta na mishale kuyaangua yale makoma. Alipoambulia patupu, Sultani aliandaa sherehe ya ngoma ya '*Mwao*' na kumwalika Liyongo. Akiwa shereheni, Sultani aliwatuma askari wake waende wamtie nguvuni Liyongo na kumtia gerezani.

Akiwa gerezani, Sultani na wenzake waliamua kumuua Liyongo ili asije akafaulu kumpokonya uongozi. Kabla ya kutekelezwa kwa mauaji yale, Liyongo alitumia hekima kumtuma kijakazi Sada kwenda kumwambia mamake Liyongo atengeneze mkate wa wishwa na ndani yake aweke tupa ambayo angeitumia kukatia minyororo aliyokuwa amefungwa nayo kule gerezani ili atoroke.

Kabla ya Sultani kutekeleza mauaji yake, aliandaa sherehe nyingine ya ngoma ya '*Mwao na Gungu*' kwa niaba ya kumtumbuiza Liyongo kabla hajanyongwa. Wakiwa katika harakati ya kusherehekea, Liyongo alitumia tupa kukata pingu zilizokuwa zimemfunga miguuni na mikononi, akatoroka gerezani na akurudi kule bara. Akiwa kule bara aliuawa na kijana (mtoto wake) aliyemdunga kitovuni mwake kwa kutumia sindano ya shaba. Liyongo alifia kisimani akiwa ameshika uta na mishale tayari kumshambulia adui yake. Watu hawangeenda kuteka maji kisimani kwa sababu walipomwona Liyongo, waliogopa wasishambuliwe naye kwani hawakuwa wamegundua kuwa alikuwa amekufa tayari. Baada ya kuishiwa na maji, watu kijijini walitaabika sana mpaka pale uamuzi ulifanywa wa kumwendea mama yake Liyongo ili aje ambebeleze ndipo atoke kisimani. Mamake alifahamu kuwa Liyongo alikuwa ameaga dunia.

Huu ndio utendi ambao umesimilishwa na Matundura (2001) katika riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* huku akiwalenga watoto. Aidha, utendi huu umesimilishwa katika tamthilia na Mberia (2001) huku akiwalenga watu wazima.

### 5.1 Ploti

Usimilishwaji wa kimsingi sana ambao mwandishi ameufanya ni ule wa kusimilisha utendi kuwa riwaya kwa kulifanyia umbo la ploti marekebisho. Amebadilisha umbo la tenzi lenye mfululizo wa beti zilizo na mishororo kuwa aya fupi fupi zilizo na sentensi fupi fupi huku akiigawanya ploti ya matini lengwa katika sura mbalimbali. Kwa jumla, riwaya hii ina sura kumi na mbili zilizo na

matukio yenye muwala na muumano na yale ya sura nyingine. Kila sura ina anwani mwafaka na maelezo ambayo yanafafanua zaidi kuhusu anwani ya kila sura. Kwa mujibu wa Oyoo (2003) ploti nzuri ni ile yenye kujibu swali 'Kwa nini?'. Mshikamano uliopo katika sura za matini lengwa umeibua ploti ambayo inalijibu swali hili.

Katika sura ya kwanza, '*Kifo cha Fumo*', Mfalme Fumo ambaye amekuwa akitawala anaugua na kufariki kabla ya kumteua mrithi wake. Katika sura ya pili, '*Kuteuliwa kwa Mrithi*', wazee wanamteua Mringwari kama mrithi badala ya Liyongo ambaye alikuwa mtoto wa suria. Uteuzi huu ulisababisha ubishi mkubwa baina ya Liyongo na Mringwari. Katika sura ya tatu, '*Kinyang'anyiro cha Uongozi*', Liyongo anatafuta mbinu za kumng'oa Mfalme Mringwari mamlakani. Mfalme kwa upande mwingine anatafuta njia za kumwangamiza Liyongo. Anatumia hila ya kumtafutia kipusa kutoka katika jamii ya Wagalla ambapo alinuia kuwatumia Wagalla kumuua Liyongo. Katika sura ya nne, '*Liyongo Kumuoa Shida,*' Liyongo alimuoa msichana kwa jina Shida kutoka katika jamii ya Wagalla kisha akaenda kuishi naye kwao (nchi ya Wagalla). Akiwa huko, Mfalme Mringwari anafanya mipango ya kujaribu kumuua Liyongo bila kufanikiwa.

Sura ya tano, '*Jaribio la Kwanza la Kumuua Liyongo*', inaonyesha jinsi mpango wa kumuua Liyongo haukufaulu pale ambapo alikataa kuupanda mti mrefu wa mkoma ili achume makoma. Badala yake alitumia uta na mishale kuyaangusha makoma. Katika sura ya sita, '*Liyongo Kutiwa Mbaroni*', mfalme alitafuta njia

nyingine ya kumwangamiza ambapo Liyongo alishikwa aliporudi Shanga na kutiwa gerezani. Katika sura ya saba, *'Liyongo Kufikishwa Kortini,'* Liyongo alifikishwa kortini na kuhukumiwa kifo. Kabla ya kuuawa, mfalme anamfanyia heshima za mwisho. Katika sura ya nane, *'Ngoma Ya "Gungu Na Mwao"*, mfalme anamwandalia Liyongo ngoma hii. Akiwa shereheni, Liyongo anamtumia mamake ujumbe wa siri. Mamake anapoupokea ujumbe, anatengeneza mkate na kutia tupa ndani kisha akamtuma Sada ampelekee Liyongo kule mbaroni. Liyongo anatumia ile tupa kuikata ile minyororo iliyokuwa imetumiwa kumfunga miguu na mikono na akatoroka gerezani mpaka kule kwa Wagalla ambapo aliungana tena na mtoto na mkewe. Mfalme anashindwa kabisa kumuua Liyongo. Anawaita wazee ili kuuliza ushauri kutoka kwao.

Katika sura ya tisa, *'Mkutano Wa Siri,'* wazee wanamshauri amtumie mtoto wake Liyongo ambaye aliitwa Moni kumuangamiza. Sura ya kumi, *'Mwana Kumdadisi Baba,'* mwandishi anasimulia jinsi mfalme alimwita mtoto wake Liyongo na akamwahidi kumuoza bintiye na pia kumpa mali nyingi ikiwa angedadisi jinsi ya kumwangamiza babake. Baada ya kudadisi na kupata jawabu, mfalme anamwamuru Moni ambaye ni mwanaye Liyongo amuue babake. Sura ya kumi na moja, *'Kifo cha Liyongo,'* inasimulia jinsi Moni alivyomuua babake na kisha akatorokea Shanga kwa Mfalme Mringwari ili aweze kujinyakulia zawadi zake lakini katika sura ya kumi na mbili, *'Moni Kukosa Zawadi'*, Moni hakupewa zawadi na badala yake Mfalme alimfukuzia mbali. Kila sura inaonyesha sababu ya kuwepo kwa sura inayofuatia.

Mwandishi ameweza kuifupisha ploti kwa kuondoa beti ambazo hazisaidii katika ukuaji wa hadithi. Kwa mfano, ameondoa maelezo mengi kuhusu ushujaa wa Liyongo. Kule kufupisha ploti ya matini lengwa kunaondoa uchofu wa mtoto wa kuisoma kwani mtoto hana ule uwezo wa kuisoma hadithi ndefu. (rejelea sura ya pili uk.27 kwa maelezo zaidi)

Mwandishi ameongezea baadhi ya maelezo na matukio mengine ambayo hayapo katika matini chasili. Mwandishi ameongezea maelezo kuhusu kuugua na kufa kwa babake Liyongo katika sura ya kwanza; *'Kifo cha Fumo'*, maelezo kuhusu uteuzi wa mfalme ambaye angerithi ufalme katika sura ya pili; *'Kuteuliwa kwa Mrithi'* na katika sura ya tatu; *'Kinyang'anyiro cha Uongozi'*, ameongezea maelezo kuhusu jinsi Liyongo aliunda chama cha *'Operation Mringwari Out'* alichokitumia kuenezea propaganda za kuharibu sifa za utawala wa Mringwari akiwa na nia ya kumng'oa mamlakani Mringwari. Aidha, ameongezea sura ya kumi na mbili; *'Moni Kukosa Zawadi.'* Mwandishi ameweza kuonyesha vile Moni alitoka ng'o! bila kupewa chochote tena na Mfalme, badala yake anafukuziwa mbali. Mwandishi ameongezea sura hizi ili kuzua mgogoro baina ya Mringwari na Liyongo na kisha kuusuluhisha kufikia mwisho wa hadithi. Kwa kufanya hivi, ameweza kujenga taharuki ya mtoto na kumpa azma ya keendelea kuisoma hii riwaya. Pia, ameipa hadithi kilele kinachoambatana na matarajio ya mtoto pale ambapo uovu wa Moni unaadhibiwa alipokosa kupewa ahadi zake na Mfalme (uk.99).

Kinyume na matini chasili ambapo imetajwa tu kuwa mamake Liyongo aliuimba wimbo wa kumbebeleza mwanaye, mwandishi ameuandika wimbo huu katika matini lengwa (uk.96 – 97) kama ifuatavyo,

> "Liyongo mwanangu gwiji
> Liyongo mwanangu siji
> Mie sinyamazi jii
> Nakuita utoke kisimani."

Huu ni ufanisi wa hali ya juu wa usimilishwaji pale ambapo wimbo kama mbinu ya fasihi simulizi umeingizwa katika riwaya. Mwandishi ameuweka ule wimbo pale kimakusudi ili ampe msomaji nafasi ya kuondoa dukuduku ambalo limejengeka baada ya Liyongo kuuawa na mtoto wake Moni.

Kwa jumla mwandishi amefaulu katika kuisimilisha ploti ya matini chasili. Kupitia usimilishwaji huu, mwandishi ameipa hadithi yake mantiki hasa pale ambapo ameufuma ubeti mmoja na mwingine ili kuzifanya zitiririke katika mkururo wa mawazo na matukio yanayoweza kuziteka akili za mtoto tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Isitoshe, mwandishi amefuma ploti yake kuafiki mtiririko wa vitushi ambao huwavutia watoto yaani utangulizi, kiini na hitimisho. Zaidi ya hayo, hadithi imeishia katika kilele cha juu pale ambapo matarajio ya watoto yametimizwa. Moni anaadhibiwa kwa ajili ya kumsaliti baba yake.

## 5.2. Lugha

Lugha kama chombo cha mawasiliano inaweza kutinga au kuendeleza mawasiliano baina ya mtoto na mwandishi. Lugha ikitumiwa vibaya itatinga

kuwepo kwa mawasiliano na iwapo itatumiwa vizuri itawezesha kuwepo kwa mawasiliano. Kwa mujibu wa Tylor (1994), fasihi ya watoto huwapa fursa watoto kujifunza kuhusu lugha na matumizi yake. Kwa hivyo, inafaa mwandishi atumie lugha yenye ufaafu kwa mtoto na aitumie kwa ufundi huku akifahamu kuwa, mbali na kuwasiliana na mtoto ana jukumu la kumfunza lugha na matumizi yake.

Matundura (2001) ameweza kuirahisisha lugha hii katika kiwango cha kumfaa mtoto. Badala ya lahaja ya Kiamu ambayo imetumika katika matini chasili, ametumia Kiswahili sanifu ambacho ni rahisi kueleweka na mtoto. Mwandishi ameifanya lugha ya matini lengwa inoge zaidi pale anapozitumia tamathali za usemi katika matini lengwa jambo ambalo halijitokezi katika matini chasili. Baadhi ya tamathali alizozitumia ni:

### 5.2.1 Tanakali Sauti (Onomatopea)

Huu ni ujenzi wa maneno kwa kuiga sauti au mlio wa kitu. Wakati mwingine tanakali sauti hutokana na kurudiwarudiwa kwa maneno. Baadhi ya onomatopea alizozitumia mwandishi ni pamoja na '*upepo mwanana ulivuma vuu vuu',* (uk.7), '*kunyamaza jii*', (uk.17) '*damu ilimbubujika bubujububuju,'* (uk.21) na '*alivifunga (vitu) ki ki ki',* (uk.33.) Hizi zimetokana na kuiga sauti. Katika wimbo wa mamake Liyongo, kuna tanakali zinazotokana na kurudiwarudiwa kwa maneno kama vile '*Liyongo mwanangu gwiji, Liyongo mwanangu siji',* (uk.97). Tanakali ni muhimu katika kuijenga taswira akilini mwa mtoto na pia hutumika kulisisitiza jambo.

### 5.2.2 Methali

Methali hutumiwa kutajirisha fani na maudhui, kufunza maadili, kuonya, kutoa kejeli na hata kuongezea utamu wa lugha.

Methali, '*chochote king'aacho si dhahabu*', (uk.32) imetumiwa na mwandishi kumuonya msomaji dhidi ya kukimbilia kile kinachoonekana kizuri bila kwanza kukiweka kwenye mizani kwani huenda kikamletea madhara baadaye. Liyongo alivutiwa na umbo la Shida bila kujua kuwa ndiye angekuwa chanzo cha maangamizi yake. Methali '*kiendacho kwa mganga hakirudi,*' (uk.44) imetumiwa na wazee waliokuwa wametumwa ili wamuue Liyongo. Methali hii inakejeli kitendo cha Mfalme cha kuwahonga wazee ili wamuue Liyongo jambo ambalo walishindwa kulitekeleza. Methali, '*Mbio za sakafuni huishia ukingoni*', (uk.56) inatumiwa na mmoja wa askari waliotumwa na Mfalme wakamkamate Liyongo. Methali hii inaonya msomaji dhidi ya kujiingiza katika mambo ambayo hatimaye hatakuwa na uwezo wa kuyamudu na mwishowe yakamtia matatani kama alivyofanya Liyongo ambaye alitiwa gerezani kwa kuupinga utawala wa Mringwari. '*Msiba wa kujitakia hauna kilio,*' (uk. 56) ni methali ambayo inaonya dhidi ya kujiingiza katika mambo ambayo mwishowe ni balaa tupu. Methali, '*ahadi ni deni*' (uk. 81) ni methali inayofunza juu ya uaminifu kuwa mtu akiweka ahadi na mwingine lazima aitimize. Baada ya Moni kufanya mapatano ya ahadi na Mfalme Mringwari, hakuwa na lingine ila kuyatimiza matakwa ya mfalme.

### 5.2.3 Tashbiha

Huu ni ulinganishi wa moja kwa moja kwa kutumia viunganishi kama vile 'kama'. Hutumiwa na mwandishi kusisitiza sifa fulani na pia kuijenga picha ya aina fulani akilini mwa mtoto.

Baadhi ya tashbiha zilizotumiwa ni pamoja na; Tashbiha '*jogoo walijimbizana kwa kokoiko zao kama washairi wawili wanaojibizana,*' (uk.7) inampa mtoto picha ya mapambazuko. Tashbiha '*mamba alitokea ghafla kama maiti,*' (uk.20) inaonyesha jinsi lile shambulizi la mamba lilitokea ghafla. Tashbiha '*chakula kilikuwa shida kupata kama kaburi la Baniani,*' (uk.24) inaamanisha kuwa kulikuwa na ukame. Tashbiha '*upara mkubwa kama jangwa la sahara*', (uk.38) inaonyesha jinsi sehemu kubwa ya kichwa cha yule askari ilikuwa haijaota unywele hata mmoja. '*Mkoma mrefu kama mlingoti,*' (uk.39) ni tashbiha inayosisitiza urefu wa ule mti wa mkoma. Tashbiha '*askari wengi kama wingu la nzinge,*' (uk.50) inaonyesha idadi ya wale askari. Tashbiha '*tamaa kama fisi*' (uk.69) imetumiwa kuashiria ulafi.

### 5.2.4 Misemo

Kulingana na Senkoro (1982), matumizi ya nahau, misemo na misimu katika fasihi hutegemea uhai wake kwani misemo hii huzaliwa, hukua na wakati mwingine hufa.

Mwandishi ametumia misemo kwa wingi. Baadhi ya misemo hii ni pamoja na; '*Kuaga dunia'*, (uk.13) kumaanisha kufa, '*ukumbi ulijaa pomoni'*, (uk.16) kuonyesha wingi wa watu, '*kufua dafu,'* (uk.21) kwa maana ya kufaulu, '*jino la ukucha'*, (uk.27) kwa maana ya kwa lolote liwalo, '*Tia bidii za mchwa,'* (uk.23) kumaanisha kufanya kazi bila kupumzika, '*akufaaye wakati wa jua nawe ukamfaa wakati wa mvua,'* (uk.78) kumaanisha kusaidiana mtu na mwingine wakati anahitaji msaada, '*kucheza na moto,'* (uk.27) na (uk.91). Neno '*Moto*' mara ya kwanza limetumiwa kumwashiria Mfalme Mringwari na mara ya pili linamwashiria Liyongo na kumaanisha kuwa wote wawili walikuwa hatari, 'ukumbi ulijaa kelele *kama zile za nzi wanaofanya sherehe katika kinyeshi,'* (uk.16) kumaanisha kuwa ukumbi ulijaa minong'onezano ya wazee na '*wazee walijibu kwa pamoja mithili ya nzi wengi kwenye kinyesi,'* (uk.75) kumaanisha kuwa wazee walishirikiana kwa pamoja kumjibu Mfalme.

### 5.2.5 Taswira

Haya ni maelezo ambayo humpa mtoto picha akilini kuhusu kile ambacho kinazungumziwa. Mwandishi ameambatanisha maelezo haya na mbinu ya tabaini ili kuleta msisitizo wa jambo fulani. Kwa mfano katika uk.31 anapoelezea kuhusu mhusika Shida anasema;

> Shida alikuwa mwanamke wa Kigalla mwenye
> Rangi hudhurungi. Si mrefu si mfupi
> mwembamba si mnene...

Mwandishi kupitia maelezo ya jinsi Moni alivyousukumia ule msumari ndani ya kitovu cha babake (uk.92) anampa mtoto taswira ya jinsi mauaji haya yalitekelezwa.

### 5.2.6 Wimbo

Watoto wanafurahia wimbo katika matini kwa sababu wanaweza kuuimba ule wimbo na pia kuuambatanisha na miondoko na matendo kama vile kupiga makofi. Wimbo huwaliwaza watoto na pia huwafanya wakumbuke hadithi waliyoisoma. Mwandishi ameuongezea wimbo ufuatao katika matini lengwa,

Liyongo mwanangu gwiji
Liyongo mwanangu siji
Mie sinyamaji jii

### 5.2.7 Chuku

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), chuku hutokea pale ambapo sifa fulani imekuzwa kupita kiasi. Kukuzwa huku kunaweza kuwa ni kwa udogo au ukubwa. Chuku huliweka jambo linalozungumziwa kwa uwazi zaidi na hukuza sifa fulani.

Kwa mfano, sifa ya ushujaa wa Liyongo inakuzwa pale ambapo mwandishi anayatumia maneno ya chuku (uk.34). Anasema kuwa Liyongo alitembea haraka huku akiliacha nyuma wingu la vumbi. Pia, vitendo vya Liyongo vimekuzwa kuliko kawaida. Kwa mfano, anaangua makoma kwa kutumia uta na mishale, na anapuliza baragumu mpaka inapasuka.

### 5.2.8 Ucheshi

Mwandishi ametumia mbinu ya ucheshi mwishoni mwa hadithi pale ambapo anatundokezea kuwa Liyongo alikufia kisimani akiwa amepiga goti moja na kushika uta na mshale mikononi akiwa tayari kushambulia. Watu kijijini hawakudhubutu kwenda kuyateka maji kisimani kwani walimwogopa Liyongo asije akawafuma mishale. Kwa zaidi ya siku nne, wanakijiji hawakukaribia kisimani kwa sababu Liyongo alibaki vile vile na kumbe Liyongo wakati huu wote alikuwa maiti. Hawakujua mpaka pale walipomwendea mama yake Liyongo aje ambembeleze ili akubali kuondoka kisimani uk.96 na uk. 97. Hatimaye mamake anagundua kuwa siku zote hizo watu walikataa kwenda kuchota maji kisimani, Liyongo alikuwa amekufa.

Kwa jumla mwandishi amefaulu katika kuisimilisha lugha hadi katika kiwango ambapo lugha inayotumika katika matini lengwa ni nyepesi, rahisi kueleweka na yenye ufaafu kwa wasomaji wanaolengwa.

## 5.3 Usimulizi

Mwandishi ametumia nafsi ya tatu ili kuisimulia hadithi yake. Amefaulu katika kumwelezea mtoto mengi kuhusu tabia na mienendo ya wahusika aliowatumia katika kazi yake. Pia, ameweza kuelezea mtoto kuhusu mandhari tofauti tofauti ambamo matukio ya hadithi yamejikita. Kwa mfano, ameyaelezea mandhari ya bara alikotorokea Liyongo na pia mandhari ya pwani alikoishi babake Liyongo. Usimulizi huu umeipa kazi hii uasilia.

### 5.4 Wahusika

Mwandishi amewatumia wahusika kuikuza na kuiendeleza hadithi yake. Sehemu hii imeshugulikia baadhi ya wahusika ambao mwandishi amewatumia. Miongoni mwao ni:

#### 5.4.1 Liyongo.

Mhusika Liyongo ni mwanawe Mbwasho, mkewe mfalme Fumo. Katika matini chasili mhusika huyu amerejelewa kwa jina '*Fumo Liongo*'.

Liyongo ni jasiri na shujaa. Anauchukua msimamo wa kupigania uongozi na hashawishiki wala kutishika kwa jambo lolote kuubandilisha msimamo wake. Alitumia siku mbili kusafiri kutoka Shanga hadi Pate badala ya zile siku nne za kawaida. Aliipuliza baragumu mpaka ikapasuka. Ni mwenye hekima. Anatumia hekima anapohisi kuwa pana tatizo. Anatumia uta na mishale kuyaangusha makoma, anamtumia mamake ujumbe kwa njia ya hekima kupitia kwa shairi lake pasipo na yeyote kuugundua na kuuelewa ule ujumbe. Alitumia hekima kuyaangua makoma. Ni mwenye tamaa. Liyongo hakukoma kuupigania uongozi kwa sababu ya kuongozwa na tamaa ya kutaka kuwa mfalme. Kulingana na sheria ya nchi hiyo, hata ingawa Liyongo ndiye aliyekuwa mkubwa wa Mringwari, hangetawazwa kuwa mfalme kwa sababu alikuwa ni mtoto wa suria. Tamaa yake mwishowe ilimwangamiza.

Liyongo ana udhaifu mkubwa. Anapowekewa mtego wa kumuoa Shida, aliitikia kumuoa moja kwa moja bila kwanza kuyatafakari matokeo yake. Si hayo tu, Liyongo alifichua siri ya kifo chake kwa mtoto wake Moni aliyetumiwa na mfalme Mringwari kumuua. Kutokana na sifa na matendo yake Liyongo na hasa ule udhaifu wake, mtoto anaweza kujifunza jinsi ya kuyatathmini na kuyatafakari mambo kabla ya kuyatenda.

### 5.4.2 Mfalme Mringwari

Ni mwanawe Halali, mke wa kwanza wa mfalme Fumo. Amerejelewa kama '*Sultani*' katika matini chasili.

Ni mfisadi. Alitumia mali ya umma kuhonga vibaraka wamwangamize Liyongo. Hawa ni wazee waliokuwa washauri wake (uk.44), wasimamizi wa kesi (uk59) akiwemo Moni mtoto wake Liyongo (uk.79). Ni mwovu na mwenye hila kwa sababu anatekeleza mauaji ya Liyongo kichinichini. Pia anatoa ahadi za uongo kwa Moni ndiposa Moni aitikie kumuua babake.

Watoto hawangependa kujinasibisha na mhusika mwovu. Kwa hivyo, kupitia matendo ya mhusika huyu, mtoto anajifunza dhidi ya kujiepusha na maovu katika jamii.

### 5.4.3 Moni

Ni mtoto wake Fumo Liyongo. Mhusika Moni anarejelewa kama '*kijana*' katika matini chasili. Huenda mwandishi amempa mhusika huyu jina Moni kama njia

moja ya kutaifisha riwaya yake. Yaani, amempa jina la usasa na ambalo limevuka nje ya mipaka ya mazingira ya pwani.

Ni mwenye tamaa. Alipoahidiwa kuozwa bintiye mfalme na pia kupewa zawadi na mali nyingi alikubali kumsaliti babake mzazi. Ni msaliti. Alimsaliti babake kwa adui yake mfalme Mringwari kwa kumfunulia siri ya kifo cha babake. Ni mndanganyifu. Alimdanganya babake kuwa hakuna mtu aliyekuwa amemtuma ili amdadisi (Uk.83) ilhali mfalme Mringwari alikuwa amemtuma. Kupitia mhusika huyu, watoto wanajifunza kuwa uovu haulipi chochote. Ni muuaji. Alimtoa uhai baba yake kwa kutumia msumari wa shaba.

### 5.4.4 Shida

Ni mkewe Fumo Liyongo. Mhusika huyu hayupo katika matini chasili.

Ni mhusika mjinga ambaye anakubali kutumiwa na maadui wa mumewe ili wamwangamize mumewe. Ni msikivu na mtiifu. Anaposhauriwa na mumewe asirudie tena kushirikiana na maadui za mumewe, Shida hakushirikiana na wale maadui tena (uk.43). Kupitia mhusika huyu mtoto atajifunza jinsi ya kuwa mtiifu.

### 5.4.5 Sada

Huyu ni mhusika ambaye amerejelewa kwa jina *'Saada'* katika matini chasili. Ni kijakazi wa mamake Liyongo. Ni mhusika mtiifu kwani anakubali kumpelekea Liyongo chakula. Alikubali kumpelekea mamake ujumbe wa Liyongo. Ni mwepesi wa kuyakumbuka mambo. Aliweza kulikumbuka lile shairi la Liyongo na kuliimba



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

hata baada ya kurudi nyumbani. Watoto wanaweza kujifunza utiifu kupitia mhusika Sada.

### 5.4.6 Mbwasho

Mhusika Mbwasho amerejelewa kwa jina '*mamake Liyongo*' katika matani chasili. Ni mamake Liyongo.Ni mwanamke jasiri ambaye aliweza kumtengenezea Liyongo mkate na kutia tupa ndani yake ambayo Liyongo aliitumia kukatia minyororo yake iliyokuwa imemfunga. Ujasiri wake pia ulimwezesha kumkaribia Liyongo kule kisimani bila uwoga wa kufumwa mshale na mwanaye jambo ambalo hakuna mtu mwingine alilithubutu. Ni mwimbaji. Aliweza kuutunga na kumwimbia Liyongo wimbo wa kumbembeleza ili akubali kutoka pale kisimani (Uk.97). Pia aliweza kuutambua ujumbe uliokuwapo katika lile shairi/ wimbo wa Liyongo na kuutekeleza.

### 5.4.7 Halali

Mhusika huyu hayupo katika matini chasili. Ni mamake Mringwari. Ni mwivu. Hakurithika na kile alichokuwa nacho. Alimwonea wivu mke mwenza (Mbwasho) kwa sababu ya seti za kochi alizokuwa amenunuliwa na mumewe Fumo. Wivu huu unazua ugomvi baina ya Halali na mumewe Fumo (Uk.12). Mwandishi asema hivi katika uk.12,

> ......Ugomvi wa muda mrefu aliokuwa nao na mumewe
> kwa sababu ya kutonunuliwa seti za kochi kama
> alizokuwa nazo Mbwasho ulikuwa umesuluhishwa

Pia sifa hii inadhihirika pale ambapo alimshauri mwanawe Mringwari aende akamuombe babake amrithishe ufalme ili Liyongo mtoto wake Mbwasho asije akarithishwa (Uk.25).

### 5.4.8 Jaji na Wazee

Hawa ni vibaraka wa Mfalme Mringwari ambao walitumiwa ili kumwangamiza Liyongo. Ni wasaliti. Walikubali kuhongwa na Mfalme ili wamwangamize Liyongo. Majaji waliiamua kesi huku wakimpendelea Mfalme Mringwari ilhali Wazee walijaribu kumuua Liyongo bila kufaulu. Aidha, Wazee walimshauri Mfalme Mringwari amtumie Moni, mtoto wake Liyongo kumuua babake.

Mwandishi amewasimilisha wahusika kwa kuwapa majina wale ambao wamerejelewa kwa majina ya kawaida ili watoto waweze kuwafahamu kwa urahisi. Pia amewapa baadhi yao majina ya majazi ambayo yanaambatana na tabia zao. Mhusika Shida ndiye chanzo cha shida katika maisha ya Liyongo. Mhusika Halali ndiye mke halali wa Fumo. Majina ya majazi humsaidia mtoto kuwakumbuka wahusika na pia kuelewa tabia zao. Aidha ameongezea idadi ya wahusika ili kuikuza na kuendeleza ploti ya hadithi. Vile Vile, mwandishi anawatumia wahusika wa kike na kiume katika matini lengwa. Jambo hili ni muhimu katika kazi za watoto. Kwa mujibu wa Oyoo (2003), watoto hujinasibisha na wahusika waliosabihiana nao kijinsia. Kwa hivyo, uumbaji mzuri wa wahusika ni ule unaojumuisha wahusika wa kike na wa kiume katika matini.

### 5.5 Maudhui

Mwandishi ameyashughulikia maudhui mbalimbali katika kitabu hiki. Mengi ya maudhui haya yanaafiki kiwango cha uelewa wa watoto wanaolengwa. Aidha, maudhui haya yana mafunzo juu ya maadili ya jamii. Baadhi yake ni:

#### 5.5.1 Ushujaa

Maudhui haya yanaendelezwa na mhusika Liyongo. Maudhui ya ushujaa yanawatia watoto changamoto ya kujitahidi maishani. Liyongo anaweza kumwokoa kijana mwenzake kutoka kwenye mdomo wa mamba (uk.20-21), anatumia tupa kuikata minyororo, anaangua makoma kwa kutumia mishale na anatembea kutoka Shanga hadi Pate kwa muda wa siku mbili badala ya zile nne za kawaida huku akiwa amebeba mzigo mzito.

#### 5.5.2 Tamaa.

Kupitia kwa mhusika Moni, mtoto anaweza kujifunza kuwa tamaa ni mbaya na ina hasara yake. Tamaa kubwa ya mali ilimfanya Moni amuue babake (uk.92 – 94) na mwishowe hakuipata hiyo mali. Badala yake alifukuzwa na Mfalme pale ambapo aliishi maisha yake ya baadaye yakiwa ya shida na ukiwa kwani alimpoteza baba yake na hangerudi nyumbani kwao kuishi na mama yake.

#### 5.5.3 Ufisadi

Mfalme Mringwari anayatumia mamlaka yake vibaya kama kiongozi. Ufisadi umemfanya Mfalme akose haki, utu na uadilifu katika kuitumikia jamii yake. Aliwadhulumu na kuwanyanyasa wanyonge kwa kuwatumia vibaya ili atimize

matakwa yake jambo lililokuwa limekatazwa na Mfalme Fumo kabla ya kifo chake (uk.12). Anawahonga wazee na wasimamizi wa kesi ili wamwangamize Liyongo. Ingawa ufisadi ni jambo ambalo limesheheni sana katika jamii zetu na ambalo lina madhara makubwa, mwandishi hakulipa uzito unaofaa ili kumfunza mtoto kuwa ufisadi ni kitendo kibaya. Mfalme Mringwari alifaulu kumwangamiza Liyongo baada ya kutumia njia za ufisadi. Kule kutoyapa maudhui haya uzito wa kutosha kumempelekea kuonekana kama kwamba ufisadi ni jambo njema.

### 5.5.4 Usaliti

Usaliti unaendelezwa na wahusika kama Moni, Shida, wazee na Jaji Mkuu. Mhusika Moni alimsaliti na kumuua babake, Shida alimsaliti mumewe alipofanya njama ya kushirikiana na adui zake ili wamwangamize. Wazee na Jaji mkuu wanatumiwa kama vibaraka wa Mfalme Mrigwari. Wazee wanamsaliti Liyongo kwa kukubali kulipwa pesa ili wamuuwe. Pia wanamsaliti Liyongo pale ambapo walimshauri mfalme amtumie mtoto wake Moni kumwangamiza (uk76). Jaji mkuu pamoja na wasimamizi wa kesi walikubali kuhongwa ili uamuzi wa kesi umpendelee Mringwari (uk.59) kitendo kilichomsaliti Liyongo. Mfalme Mringwari alimsaliti Moni kwa kumhini mali aliyomwahidi. Kupitia wahusika hawa, mwandishi amefaulu kumfunza mtoto kuwa usaliti ni kitendo kiovu na anahitaji ajiepushe nacho.

### 5.5.5 Udhaifu

Liyongo alimtolea mtoto wake Moni siri ya kifo chake kitendo ambacho ni cha udhaifu. Udhaifu huu ulisababisha kifo chake. Mwandishi anawafunza watoto wawe watu wa kuficha siri na wasiwe watu wa kuropokwa mambo, jambo ambalo linaweza kuwaletea madhara makubwa na kuwatia mashakani.

## 5.6 Umbo La Kitabu

Hujumuisha mambo kama vile maandishi, michoro na rangi iliyotiwa katika michoro pamoja na ujalidi wa kitabu.

### 5.6.1. Vielezo (michoro)

Kwa maoni yao Knowles na Malmkjaer (1996), vielezo ni muhimu sana kwani humsaidia msomaji kuuelewa mwingiliano uliopo baina ya hadithi, lugha na ulimwengu jambo ambalo huipa hadithi uhai. Wanaendelea kusema kuwa, vielezo humpa mtoto nafasi ya kuwa na mwingiliano wa moja kwa moja na matini kwa sababu vinasisimua hisia zake. Vielezo pia humfundisha mtoto jinsi ya kuyatumia maneno kuashiria kitu fulani.

#### 5.6.1.1 Mchoro na Anwani ya Jalada

Mchoro wa jalada umetiwa rangi zenye mchanganyiko unaovutia macho (taz. kbt. 17). Mchoro huu una muwala wa moja kwa moja na anwani ya kitabu, '*Mkasa wa Shujaa Liyongo*'. Liyongo anaonekana babe la mtu aliye katika mkasa

fulani. Kielezo hiki kinaonyesha jinsi Liyongo alivyofanikiwa kujiweka huru kule gerezani kama inavyodhihirika katika uk.70,

> Katika chumba alimofungwa, Liyongo aliifichua tupa yake. Alianza kuzikereketa zile pingu zilizokuwa miguuni. Baada ya bidii za mchwa alifanikiwa kuzikata. Ilimchukua kama saa moja kuimaliza kazi hii. Halafu aliulenga mlango na kuupiga teke. Ulilegea kidogo pale ulipofungwa. Aliupiga tena, ukalegea zaidi.

Mchoro huu na anwani ya kitabu zinamvutia msomaji kukisoma kitabu. Zinaijenga taharuki ya mtoto ya kutaka kujua ule mkasa uliompata Liyongo.

#### 5.6.1.2 Vielezo vya Matini

Kwa jumla, vielezo vya matini ni kumi na viwili. Kila mchoro una uwiano na maelezo ya matini. Mwandishi ametumia rangi ya buluu katika vielezo hivi (taz. vbt 18 – 28). Ingawa rangi ya buluu ni miongoni mwa rangi zenye kung'aa na ambazo hupendeza macho ya watoto, matumizi ya rangi hii katika kila picha bila kuichanganya rangi hii na nyingine yamekithiri na kuvifanya vielezo hivi viwe kinaishi kwa mtoto. Michoro kama hii huenda ikawachosha watoto hasa wale ambao wanajali vielezo katika matini. Mchoraji amefaulu kutumia vielezo vyenye uthibiti. Mavazi na umbo la wahusika halibadilikibadiliki na kwa hivyo ni rahisi kwa mtoto kuwatambua wahusika mbali mbali bila kukanganyikiwa. Hata hivyo, baadhi ya vielezo haviambatani na maelezo ya matini. Kwa mfano, kielezo katika uk.10 (taz. kbt. 18) mchoraji hakumsawiri Mfalme Liyongo kama Mfalme. Amemvisha mavazi ya kawaida tu ambayo yanamfanya aonekane kama mzee wa kawaida tu asiye na cheo. Kielezo katika uk.41 (taz. kbt. 22) kinakanganya mtoto kwa sababu mti wa mkoma umechorwa kama mnazi na makoma yametiwa rangi

ya samawati badala ya rangi nyekundu. Kielezo katika uk.52 hakiambatani na maelezo ya matini uk. 51 (taz. kbt. 23) kuwa Liyongo alitiwa ndani mwa chumba cha jela kilichojaa giza na baridi akiwa amefungwa pingu mikononi na miguuni. Kinyume na haya, Liyongo hana pingu mikononi wala miguuni na chumba alimokaa kimejaa mwangaza. Ni muhimu kuwa na usawa baina ya matini na vielezo kwani kama asemavyo Oyoo (2003), vielezo hujaribu kuteka yale maneno yaliyoko kwenye matini.

Hata hivyo mchoraji amefaulu kutumia vielezo kama njia moja ya kuwasiliana na mtoto na kuzidisha ubora wa hadithi unaomfanya msomaji aikumbuke ile hadithi, kuifanya haditi ieleweke na msomaji na kukifanya kitabu chake kimvutie msomaji.

## 5.7. Hitimisho

Kwa mujibu wa nadharia ya kimtindo, sura hii imehakiki jinsi mwandishi alivyoitumia lugha ili kufaulisha usimilishwaji wa kazi yake katika kuwaumba na kuwasawiri wahusika, kuikuza na kuiendeleza ploti ya hadithi na kuyawasilisha maudhui ya hadithi kwa mtoto anayelengwa. Fauka ya hayo, sura hii pia imehakiki jinsi mwandishi ameoanisha matumizi ya lugha na vielezo katika matini lengwa ili kurutubisha ujumi wa hadithi yake.

Mwandishi amefanikiwa kuisimilisha matini chasili ya karne nyingi zilizopita na kuipa sura na mwamko mpya wa kisanaa unayoifanya matini lengwa kukifaa

kipindi hiki cha kihistoria. Ameshirikisha matukio ya kisasa kama mbinu za kuunda chama cha upinzani cha kisiasa cha *'Operation Mringwari Out au OMO'* uk.23. Ufanifu wake umedhihirika zaidi pale ambapo kitabu chake kimeteuliwa na kupendekezwa na wakuza mitaala wa Taasisi ya ukuzaji mitaala (K.I.E) wakishirikiana na Wizara ya Elimu kuwa miongoni mwa vitabu vinavyosomwa na watoto katika shule za msingi.

Sura ifuatayo inalinganisha na kulinganua usimilishwaji wa vitabu vyote vitatu vilivyoteuliwa ili kutathmini ukuaji na mwelekeo wa usimilishwaji katika fasihi ya watoto.

# SURA YA SITA

## Ulinganishi na Ulinganuzi wa Usimilishwaji wa *Alfu Lela Ulela*, *Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo*.

### 6.0 Utangulizi

Utafiti huu umeshugulikia usimilishwaji wa vitabu vya fasihi kutoka jamii tatu, *Mashimo ya Mfalme Sulemani* chenye asili ya fasihi ya Afrika Kusini, *Alfu Lela Ulela* chenye asili ya fasihi ya Uarabuni na *Mkasa wa Shujaa Liyongo* chenye asili ya fasihi ya Waswahili. Aidha, usimilishwaji huu ulifanywa katika vipindi tofauti vya kihistoria. Riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* ilisimilishwa baada ya kipindi cha ukoloni ilhali hivi vingine viwili vilisimilishwa na wakoloni wakati wa kipindi cha ukoloni. Katika kipindi hiki, Wazungu walikuwa mabwana huku Waafrika wakisutwa na kudharauliwa. Hii ndiyo hali inayojitokeza hata katika fasihi yao ya wakati huo ikiwemo fasihi ya watoto.

Sehemu hii imehakiki jinsi usimilishwaji uliendelezwa katika kipindi cha ukoloni na kipindi baada ya ukoloni. Vipengele ambavyo vimeshugulikiwa ni lugha, ploti ya hadithi, wahusika, maudhui na umbo la kitabu.

### 6.1 Ploti

Ploti ya hadithi katika matini lengwa imefupishwa ili kuwafaa watoto ikilinganishwa na ile ya hadithi katika matini chasili. Kulingana na Oyoo (2003),

watoto wa umri wa miaka kumi hadi kumi na mitano huweza kusoma hadithi iliyo na urefu wa maneno elfu mbili. Hili ni jambo ambalo limetiliwa maanani katika usimilishwaji wa vitabu hivi isipokuwa riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani.* Riwaya hii ni ndefu na ingawa ina mtiririko mzuri wa vitushi, huenda ikamchosha msomaji hasa kutokana na ile sehemu ya utangulizi ambayo ina maelezo mengi yanayokanganya na kuifanya hadithi ikawie kuanza. Sehemu hii inaweza kuondolewa bila kuathiri kiini cha hadithi.

Aidha, ploti za hadithi katika vitabu vyote vitatu imejaa matukio yenye kusisimua na kumvutia msomaji. Matukio haya yanajenga taharuki ya mtoto hivyo kumpa azma ya kuisoma ile hadithi tangu mwanzo hadi mwisho. Ploti hizi ni za moja kwa moja na ni sahili kueleweka na mtoto.

## 6.2 Lugha

Lugha na tamathali za lugha zilizotumika katika matini lengwa (vitabu vyote vitatu) ni sahili. Hata hivyo kitabu cha *Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Alfu Lela Ulela* vinadhihirisha athari kubwa za kikoloni katika matumizi ya lugha. Kwa mfano, matumizi ya lugha chafu kama vile Mwafrika kumtukana mwenzake kwa kumwita *'mbwa'* katika *Mashimo ya Mfalme Sulemani* ni dhana iliyo na asili yake katika miiko ya Wazungu. Katika jamii ya Waswahili, matusi ni mwiko. Isitoshe, lugha ya Kiswahili ni lugha ya adabu na hutumia tasfida ili kuficha ukali wa matusi.

Vitabu hivi viwili vinaonyesha athari za mandhari ambapo hadithi hizi zilitungiwa hata katika matumizi ya lugha. Hadithi hizi zina mandhari ya baharini hasa zile za Sindbad katika *Alfu Lela Ulela*. Aidha, tashbiha nyingi zilizotumika katika *Mashimo ya Mfalme Sulemani* zimejikita katika mandhari ya baharini na porini. Usimilishwaji wa lugha na matumizi yake katika vitabu hivi una upungufu kwa maana haukufanywa ili kuambatana na mandhari ya mtoto wa Kiafrika na pia miiko na makatazo ya jamii za Waafrika. Usimilishwaji wa lugha katika vitabu hivi unahitaji kupigwa msasa.

Usimilishwaji uliofanywa katika riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* umedhihirisha hali ya juu ya matumizi ya lugha. Lugha inayotumika hapa ni sahili na inaambatana na mandhari ya mtoto wa Kiafrika. Aidha Mwandishi ametumia lugha nzuri isiyovunja miiko ya jamii.

## 6.3. Maudhui

Mengi ya maudhui yanayojitokeza katika *Mashimo ya Mfalme Sulemani* ni ya kumsuta Mwafrika na kumtukuza Mzungu. Mwafrika amesawiriwa kama anayeendeleza maudhui ya uovu kama vile ukatili, uchawi na mauaji. Aidha anaendeleza maudhui ya tamaa ya uongozi na ujinga. Mzungu kwa upande mwingine anaendeleza maudhui ya ujasiri na ushujaa kiasi kuwa inaonekana kuwa bila Wazungu, Wakukuana hawangeweza kumng'oa Twala mamlakani. Wazungu wanaendeleza maudhui ya haki, ujuzi wa hali ya juu na pia ushindi. Wazungu pia wanaendeleza sifa ya undanganyifu. Wanapogundua kuwa

Waafrika hawakuelewa maana ya kuandama kwa mwezi, wanachukua fursa hii kuwandanganya Waafrika kuwa walikuwa na uwezo wa kufanya miujiza ili kuwe na giza kwa muda mfupi na kisha warejeshe ile hali ya kawaida. Maudhui haya yanaendelezwa na Wazungu kwa niaba ya kujitukuza na kujisifu huku wakimwonyesha Mwafrika kuwa walikuwa na uwezo na ujuzi wa hali ya juu.

Hii ni kasumba ya Mzungu dhidi ya Mwafrika , jambo ambalo limepitwa na wakati na linafaa liondolewe katika kazi za watoto kwani kasumba kama hii mwishowe inawaathiri watoto. Wataendelea kumchukulia Mzungu kuwa kiumbe bora kuliko Mwafrika.

Usimilishwaji uliofanywa na Matundura (2001) umemlejeshea Mwafrika hadhi na sifa zote alizonyimwa na Mzungu. Mwandishi ameweza kumwonyesha mtoto kuwa hata Waafrika ni mashujaa na ni werevu, kupitia kwa mhusika Liyongo na wengine. Ingawa kwa upande mwingine mwandishi amewasawiri wahusika wanaoendeleza maovu katika jamii, hakuwasawiri kwa njia ya kuchukiza kama alivyofanya Mzungu. Amewasawiri kwa njia ambayo mtoto ataweza kujifunza madhara jinsi ya kuepukana na maovu na madhara yake katika jamii.

Maudhui katika kitabu cha *Alfu Lela Ulela* yanamfunza mtoto kuhusu maadili ya kijamii kama vile wema, ukarimu, bidii na jitihada maishani. Hadithi hizi zina dhamira za kidini. Kwa upande mwingine, hadithi hizi zinamfunza mtoto madhara ambayo yanaweza kumpata iwapo hataishi kuambatana na maadili ya jamii yake.

### 6.4 Wahusika

Usimilishwaji wa wahusika katika riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani* unaonyesha upungufu mkubwa. Wahusika Wazungu wamesawiriwa kama walio bora kuliko Waafrika. Wana uwezo wa kustahimili vishindo vikubwa wakilinganishwa na Waafrika. Kwa mfano, wanastahimili kifo wakilinganishwa na Waafrika. Khiva na Ventvogel ambao ni Waafrika walikufa wakiwa safarini. Wakukuana wengi walikufa wakati wa vita ilhali Wazungu hawakufa. Waafrika wamesawiriwa kama watumishi wa Wazungu ilhali Wazungu wamesawiriwa kama mabwana. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yanafaa kuondolewa katika kazi za watoto.

Katika hadithi za *Alfu Lela Ulela* hali ya utumwa inajitokeza ingawa si kwa uwazi sana. Hali hii inajitokeza pale ambapo Sindbad na Shakabak wanauzwa kama mtumwa. Pia Sindbad ana watumishi nyumbani. Hata hivyo, hili ni jambo lililokubalika miongoni mwa Waislamu. Mabwana wanakuwa na uhusiano mwema na watumishi wao kama inavyodhihirika kupitia kwa mhusika Sindbad na Bamaside.

Usimilishwaji wa riwaya ya Matundura (2001) unaonyesha hali ya usasa ambapo vijakazi huajiriwa na hulipwa mshahara. Katika riwaya hii, hakuna ile hali ya watu kuwa bora kuliko wengine.

### 6.5 Umbo la Kitabu

Vitabu vilivyosimilishwa na Wazungu wakati wa ukoloni havina michoro inayopendeza. Vina michoro ambayo haikutiwa rangi. Tena michoro yenyewe inaonekana kama iliyochakaa na kujitenga na uhalisi licha ya kuwa hadithi hizi zina matukio yanayopendeza na kuvutia mtoto. Michoro hii inafaa kuchorwa upya ili ifanyiwe marekebisho yafaayo. Riwaya ya Matundura (2001) ina michoro iliyotiwa rangi na ambayo inapendeza macho.

### 6.5 Hitimisho

Uhakiki wa vitabu hivi vitatu umeonyesha kuwa usimilishwaji ni jambo linalohitaji kutathminiwa upya hasa katika vile vitabu ambavyo vilisimilishwa na wakoloni katika kipindi cha ukoloni. Vitabu hivi vina baadhi ya mambo ambayo yamepitwa na wakati na yanafaa yaondolewe au yasimilishwe upya kwa mtazamo mpya. Baadhi ya mambo haya ni kasumba ya Wazungu dhidi ya Mwafrika ambayo inaendelea kukita mizizi akilini mwa mtoto pole pole na mwishoe mtoto anaishia kuwa mtumwa wa Mzungu kupitia fasihi hii. Aidha, usimilishwaji uliofanywa katika kipindi cha ukoloni ulifanywa kiholela bila kuzingatia mahitaji ya watoto waliolengwa. Kwa mfano, utangulizi wa riwaya ya *Mashimo ya Mfalme Sulemani* ni mrefu mno na una mambo mengi ambayo yanamkanganya msomaji. Kadhalika, urefu wa kitabu haukutiliwa maanani. Haya ni baadhi ya mambo yanayohitaji kupigwa msasa upya.

Aidha, kuna umuhimu wa kuisimilisha fasihi ambayo asili yake ni fasihi ya Kiswahili. Kwa miaka mingi, fasihi ya Wazungu ndiyo imetawala uwanja wa fasihi ya watoto na hivyo kumpa mtoto picha kuwa hii ni fasihi bora ikilinganishwa na fasihi ya Kiswahili iliyoandikwa na Waafrika.

Sura ifuatayo imeshugulikia hitimisho la tasnifu hii. Imejadili kila sura kwa muhtasari na hatimaye kutoa mapendekezo ya baadaye ya utafiti.

# SURA YA SABA

# HITIMISHO

## 7.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari wa mahitimisho ya sura zilizotangulia za tasnifu hii. Aidha, inashughulikia matokeo ya utafiti huu na pia mapendekezo ya utafiti wa baadaye katika kazi za fasihi ya watoto.

## 7.1 Muhtasari

Utafiti huu ulidhamiria kuainisha na kuchanganua mikakati na mbinu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto. Kadhalika, ulidhamiria kuvihakiki vitabu vilivyoteuliwa vya watoto ambavyo vimesimilishwa kwa kutumia mikakati na mbinu hizi za usimilishwaji.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza imeshughulikia mada ya utafiti. Malengo ya utafiti huu yameshughulikiwa sawa na sababu za kuchagua mada ya utafiti.

Sura hii pia imeshughulikia na kubainisha upeo na mipaka ya utafiti huu. Udurusu wa yale yaliyoandikwa kuhusu mada hii ni jambo lililoshughulikiwa pia. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Elimumitindo ambapo misingi ya nadharia hii pamoja na mihimili inayotumika katika kuchanganua kazi zilizoteuliwa imebainishwa katika sura hii.

Sura ya pili imeainisha na kuchanganua mikakati na mbinu muhimu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto. Mikakati na mbinu ambazo zimeshugulikiwa ni pamoja na lugha, ploti, wahusika, maudhui na umbo la kitabu. Lugha kama chombo muhimu cha mawasiliano husimilishwa kwa kuifanya iwe sahili na yenye kueleweka kwa uwazi bila kutatiza msomaji anayekusudiwa. Tamathali za semi zinazotumiwa hufanywa ziambatane na kiwango cha uelewa cha mtoto anayelengwa.

Kadhalika, ploti husimilishwa kwa kuondoa ule mpangilio changamano. Mwandishi anaipanga ploti upya kwa kutumia mpangilio wa matukio wa moja kwa moja na ambao unafululiza kwa njia iliyo rahisi kuifuata. Ploti ambayo ni ndefu sana inafupishwa kwa kuondoa baadhi ya sehemu zake. Aidha, hadithi inafanywa kuwa na matukio ambayo yanamvutia na kuijenga taharuki ya msomaji. Hadithi inahitaji kuwa na utangulizi wa moja kwa moja na kilele chake kiwe chenye kumrithisha msomaji pale ambapo uovu unaadhibiwa ilhali uzuri unatuzwa.

Aidha wahusika wasawiriwe kwa njia ambayo wanaweza kuaminika na wasomaji wanaolengwa. Wahusika wapewe majina sahili kuambatana na muundo wa lugha pokezi na tabia na mienendo yao iwe yenye kukubalika na mtoto. Idadi ya wahusika katika hadithi inaweza kupunguzwa au kuongezwa kuambatana na uelewa wa mtoto anayelengwa.

Umbo la kitabu huchangia katika kuinua hali ya ujumi wa hadithi nzima. Mwandishi anaweza kutumia michoro yenye rangi, maandishi ya chapa yaweze kusomeka bila kukaza macho na karatasi inayotumiwa kupigia chapa iwe inang'aa ili kuyafanya maandishi yaweze kuvutia macho. Ujalidi wa kitabu ufanywe kuwa imara na jalada la kitabu lifanywe imara pia ili kuzuia kuchakaa kwa kile kitabu haraka kutokana na ile hali ya kushikwashikwa na watoto wanapokisoma. Mikakati na mbinu hizi ndizo zinatumiwa kuvihakiki vitabu vilivyoteuliwa. Uhakiki huu unaonyesha mafanikio na udhaifu wa kazi hizi zilizosimilishwa.

Sura ya tatu imehakiki kitabu cha *Alfu Lela Ulela* ambacho kimesimilishwa kutoka kwa ngano za fasihi simulizi zenye asili ya Waarabu na ambazo zilitambiwa watu wazima. Uhakiki huu umechunguza jinsi lugha imefanyiwa marekebisho ili kumfaa anayelengwa. Mwandishi ametumia tamathali za usemi katika matini lengwa. Ametumia baadhi ya tamathali zilizotumiwa katika matini chasili bila kuzifanyia mabadiliko yoyote ila tu kuzitafsiri moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya tamathali zingine za usemi zimefanyiwa marekebisho ili ziweze kuwafaa na kueleweka na wasomaji ilhali ameongezea zingine katika matini lengwa ambazo hazipo katika matini chasili.

Kadhalika, amefupisha ploti za hadithi hizi kwa kuondoa baadhi ya sehemu za matini chasili na kilele cha hadithi kinakuwa ni ushindi dhidi ya uovu.

Wahusika wamepewa majina ya utohozi. Idadi ya wahusika katika kila hadithi imebaki kama ilivyo katika matini chasili sawa na tabia na mienendo ya wahusika hawa. Katika hadithi za '*Sindbad'*, mwandishi ametumia mtindo wa usimulizi wa *nafsi ya kwanza umetumika. Mhusika Sindbadametumiwa kusimulia kuhusu* safari zake. Katika hadithi ya *'mbilikimo mwenye kinundu'* na hadithi za ndugu zake Kinyozi, mwandishi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu.

Maudhui ya hadithi hizi ni sahili kueleweka. Yanaambatana na maadili ya jamii ya Waswahili. Yanamhimiza mtoto kuwa mkweli, kujitenga na uvivu, kuwasaidia maskini na hata kutojilipizia kisasi. Mengi ya maudhui haya yameambatana na mafundisho ya kidini na kwa hivyo yanatimiza mahitaji ya kiroho ya mtoto.

Umbo la kitabu limefanyiwa marekebisho. Jalada la kitabu limetiwa rangi na picha pia, kinyume na matini chasili. Mchoraji ametumia michoro isiyotiwa rangi katika matini. Jalada la kitabu halikufanywa kuwa imara na kwa hivyo linaweza kuchakaa haraka na hata kuraruka haraka.

Mafanikio na upungufu wa mwandishi katika kukisimilisha kitabu hiki ni jambo ambalo limeshughulikiwa kwa kina.

Sura ya nne imeshughulikia usimilishwaji katika kitabu cha *Mashimo ya Mfalme Sulemani* ambacho kimesimilishwa kutoka riwaya ya *King Solomon's Mines.* Vipengele kama vile lugha, ploti, wahusika, maudhui na umbo la kitabu ni baadhi ya mambo ambayo yametiliwa maanani katika usimilishwaji wa kitabu hiki.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Ingawa kitabu hiki kinawavutia watoto kwa sababu ya hadithi yenyewe iliyojaa matukio mengi ya kijasiri na ya ajabu na tena yenye mkururo wa taharuki, mwandishi hakufanikiwa kukisimilisha kitabu hiki kwa njia inayofaa. Labda ni kwa sababu kitabu hiki kilisimilishwa na Mzungu katika kipindi cha enzi ya ukoloni pale ambapo mengi ya mambo yaliyopo katika kitabu hiki yamepitwa na wakati na yanastahili kupigwa msasa.

Ploti ya hadithi ni ya moja kwa moja. Inahusu safari na kwa hivyo, mwandishi amefaulu katika kuonyesha jinsi safari hiyo ilivyoanza, yaliyotokea njiani na hata mwisho wa safari yenyewe. Usimulizi huu wa moja kwa moja ni sahili na unampa msomaji nafasi ya kuifuata ile hadithi tangu mwanzo hadi mwisho. Mwandishi ameipa hadithi yake kiishio kinachompa msomaji nafuu baada ya yule ndugu yake Bw. Henry kupatikana. Watoto wanafurahia hadithi zinazoishia kwa ushindi.

Lugha imesimilishwa kwa kutumia tamathali za usemi. Mwandishi ametumia visawe vya tamathali zilizotumiwa katika matini chasili ili aweze kuzitumia katika matini lengwa. Pia, ameongezea baadhi ya tamathali za usemi ambazo hazipo katika matini chasili . Hata hivyo kuna baadhi ya tamathali hizi ambazo amezitafsiri sisisi na kuzitumia katika matini lengwa hasa tashibiha. Pale ambapo ametumia tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri hizo zinaifanya matini lengwa kuwa ngumu kuielewa kwa sababu ya tofauti za kiutamaduni zinazodhihirika baina ya matini chasili ambayo iliandikiwa Wazungu na matini lengwa ambayo ilinuiwa kusomwa na Mwafrika.

Lugha ni jambo la kimsingi sana katika kazi za watoto kwani watoto wangali wanaendelea kukua kimwili, kisaikolojia, kihisia, kimawazo na kilugha. Mtoto anajifunza jinsi ya kuitumia lugha kutokana na mazingira anayokulia na pia fasihi anayoisoma. Kuna haja basi ya mwandishi kutumia lugha iliyo na heshima. Kwa hivyo, lugha inayovunja miiko ya jamii kama vile lugha ya matusi haistahili kutumiwa katika matini lengwa jambo ambalo mtafsiri hakulizingatia.

Baadhi ya majina ya wahusika yametoholewa kutoka kwa majina ya wahusika wa matini chasili. Mwandishi pia ametumia baadhi ya majina ya wahusika kama yalivyo katika matini chasili. Hakuna mabadiliko makubwa ambayo yamefanyiwa wahusika. Hakuiongeza wala kuipunguza idadi ya wahusika waliotumiwa katika matini chasili. Pia hakubadilisha majukumu waliyopewa wahusika hawa katika matini chasili. Hata hivyo mwandishi hakufanikiwa kuwasimilisha wahusika wake ili kuwapa sura na umbo jipya linaloambatana na mazingira ya wasomaji anaowalenga. Kule kutowapa wahusika hawa majina ya Kiswahili hasa wale wahusika wenye asili ya Kiafrika kunaweza kumfanya mtoto ajitenge na wahusika hawa.

Maudhui yaliyoshugulikiwa yana manufaa kwa wasomaji wanaolengwa. Baadhi ya maudhui ambayo yameainishwa ni pamoja na ushujaa, ukatili, upendo na umoja. Maudhui haya yanamfundisha mtoto maadili ya kijamii ambapo mwandishi amefaulu kuyakuza matendo ya maudhui yanayoambatana na uadilifu

huku akiyakashifu na kuyaadhibu matendo yaliyo kinyume na maadili ya jamii kama vile ukatili.

Umbo la kitabu limeshughulikiwa pia. Maandishi ya chapa ambayo yametumiwa ni makubwa kiasi kuwa yanasomeka vizuri lakini karatasi ambayo imetumiwa kupigia chapa inaonekana kama iliyochakaa na isiyong'aa jambo ambalo linaathiri sura ya matini kwa jumla. Mwandishi ameongezea michoro katika matini lengwa. Michoro hutumiwa kuwasilisha ujumbe maalum na pia ili kuongezea ujumi wa kitabu kwa jumla. Aidha, sura hii imejadili kwa urefu jinsi mtafsiri amefanikiwa kukisimilisha kitabu hiki na pia jinsi hakufanikiwa.

Katika sura ya tano, usimilishwaji wa riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* umeshugulikiwa. Vipengele kama vile ploti, lugha, wahusika, maudhui na umbo la kitabu vimeshughulikiwa. Kitabu hiki cha watoto kimesimilishwa kutoka shairi aina ya utenzi; *Utenzi wa Fumo Liyongo* ambao uliandikiwa watu wazima. Kwa hivyo, mwandishi wa matini lengwa ameifanyia ploti marekebisho pale ambapo amelipangua lile umbo la ploti ya matini chasili na kulipanga upya kwa kulitumia umbo la hadithi. Aidha, ameondoa baadhi ya sehemu za beti za matini chasili ili kuifupisha hadithi ya matini lengwa. Pia, ameongezea baadhi ya sehemu zingine ambazo haziko kabisa katika matini chasili ili kuifanya hadithi kuwa yenye ufaafu kwa msomaji anayelengwa. Kadhalika, mwandishi amezingatia mambo muhimu yanayomvutia mtoto katika kazi za watoto. Amehakikisha hadithi yake imejaa taharuki ambayo humpa mtoto hamu ya kukisoma kitabu. Taharuki hii

imejengwa tangu mwanzo wa hadithi na kuendelezwa hadi mwisho. Taharuki yenyewe inatokana na ule mgogoro uliopo baina ya wahusika. Mwandishi amefanikiwa kuihitimisha hadithi yake kwa njia yenye ufaafu kwa wasomaji wanaolengwa pale ambapo uovu unaadhibiwa.

Lugha iliyotumika katika matini chasili ni lahaja ya kiamu. Mwandishi ameisimilisha lahaja hii kwa kutumia lugha sanifu ya Kiswahili sanifu ambayo ndiyo lugha inayotumika katika maandishi na shughuli zinginezo. Ameitumia lugha kitamathali kwa kutumia tamathali za usemi kama vile tashbiha, methali, tanakali za sauti, misemo na misimu, kupiga chuku, takriri, kinaya na hata taswira. Viungo hivi ni vikolezo vya kuitia lugha utamu na pia huwa na funzo maalum kwa msomaji anayelengwa. Mwandishi ametumia lugha sahili ambayo inaeleweka na wasomaji wanaolengwa.

Usimilishwaji wa wahusika umefanywa pale ambapo mwandishi amewapa majina wale wahusika wa matini lengwa ambao hawakuwa wamepewa majina maalum ya kuwatambulisha katika matini chasili. Watoto hupendezwa na wahusika wenye majina maalum wala si majina ya kijumla. Matundura (2001) amefanikiwa kuvutia wasomaji wake kwa njia hii. Idadi ya wahusika katika matini lengwa imeongezewa ili kuipa hadithi mwanzo mzuri. Mwandishi amewafunua wahusika wake kitabia kupitia matendo yao katika hadithi kuliko kuwaelezea jambo ambalo linawapendeza watoto sana.

Maudhui yamesimilishwa ili yawafae wasomaji wanaolengwa. Mwandishi ameshugulikia maudhui kama vile uchoyo, ufisadi, tamaa na ushujaa. Haya ni maudhui ya kimaadili ambayo yanamfunza msomaji anayelengwa jinsi ya kuwa mwadilifu katika jamii. Vitendo vinavyokiuka maadili ya kijamii kama vile uchoyo, tamaa na ubinafsi vinakashifiwa na kuadhibiwa mwishoni mwa hadithi kama ishara ya kumkanya msomaji dhidi ya kujihusisha na vitendo kama hivi katika jamii. Ingawa mwandishi amevihukumu vitendo hivi vilivyo kinyume na maadili ya jamii, hakufaulu kumhukumu mhusika mfalme Mringwari ambaye anapanga njama ya kumuua Linyongo kitendo ambacho ni kinyume na maadili ya kijamii. Umbo la kitabu limesimilishwa ili kukipa kitabu sura mpya yenye kupendeza macho ya wasomaji wanaolengwa. Mchoraji ametumia michoro iliyotiwa rangi katika kila sura na hata katika jalada la kitabu. Kila mchoro una mwingiliano wa moja kwa moja na matini. Michoro inafafanua zaidi ile hadithi inayohusika kwa minajili ya kuleta uelewa wa hali ya juu wa hadithi yenyewe kwa msomaji anayelengwa. Hata hivyo, mwandishi alitumia rangi moja tu ya samawati katika michoro yake yote jambo ambalo linaifanya ile michoro ikose ule mvuto wa macho. Mchanganyiko wa rangi huipa michoro sura nzuri na yenye kupendeza kuliko kuwa na matumizi ya rangi moja katika michoro iliyo kwenye matini.

Sura ya sita imelinganisha na kulinganua usimilishwaji wa vitabu vilivyoteuliwa, *Alfu Lela Ulela*, *Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo* kwa misingi ya lugha, ploti, wahusika, maudhui na umbo la kitabu.

## 7.2 Matokeo ya utafiti

Kutokana na utafiti huu, inadhihirika kuwa usimilishwaji wa kazi za watoto ni jambo ambalo limekuwepo tangu wakati wa kipindi cha Wakoloni ambao ndio walikuwa wa kwanza kuvisimilisha vitabu vilivyowalenga watu wazima ili visomwe na watoto. Pia inadhihirika kuwa usimilishwaji ni jambo muhimu kwani hurahisisha kazi ambazo hapo awali hazingesomwa wala kueleweka na watoto kwa kuzifanyia marekebisho yanayofaa ili ziweze kusomwa na watoto.

Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa, usimilishwaji si jambo linalofanywa kiholelaholela bali ni jambo la kimsingi na linahitaji kufanywa kwa utaratibu kwa kufuata mbinu na mikakati inayofaa. Mbinu hizi zinajumuisha vipengele kama vile lugha na matumizi yake, ploti ya hadithi, wahusika, maudhui na pia umbo la kitabu. Vile vile, ili usimilishwaji ufaulu, mwandishi anastahili kuwa na ujuzi wa kuwafahamu wasomaji anaowalenga pamoja na mahitaji yao. Watoto hutofautiana kimahitaji na huwa na matarajio yaliyotofautiana kulingana na umri wao.

Kutokana na kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu, imebainika kuwa, lugha ni chombo cha mawasiliano na ambacho ni muhimu sana katika fasihi ya watoto. Lugha humwezesha mwandishi kuwasiliana vilivyo na msomaji. Lugha ambayo imetumika katika matini chasili huenda ikawa ngumu kueleweka na mtoto hivyo mwandishi na msomaji huenda wasiwasiliane. Lugha iliyotumika katika matini

chasili basi haina budi kurahisishwa katika matini lengwa ili mtoto anayelengwa aweze kuisoma na kuielewa ile matini.

Imebainika pia kuwa, mara nyingi ploti ya matini chasili iliyowalenga watu wazima huwa ni ploti changamano na huenda ikamkanganya msomaji anayelengwa katika matini lengwa na pia hadithi ya matini chasili huwa ndefu kiasi cha kumchosha mtoto. Kwa hivyo, usimilishwaji wa ploti ni jambo muhimu. Mwandishi ana uhuru wa kuirahisisha kwa kuipangua na kuipanga upya kwa njia ambayo matukio yatapangwa kwa mpango wa 'la mwanzo lije mwanzo na la mwisho lije mwisho'. Pia mwandishi an uhuru wa kuufupisha ule urefu wa hadithi kwa kuondoa baadhi ya sehemu za hadithi mradi tu kiini cha hadithi kitabaki kuwa vile vile bila kuathiriwa. Mwandishi ana uhuru wa kuingilia matini chasili na kuifanyia marekebisho yanayohusiana na jinsi hadithi imeanzishwa na pia kuhitimishwa. Imebainika kuwa watoto hufurahia hadithi zinazoanza moja kwa moja bila utangulizi mrefu na kilele chake kiwe chenye matokeo ya kuridhisha kama vile uovo uadhibiwe na uzuri utuzwe. Pia ploti yenyewe iwe na mfululizo wa matukio ambayo yataijenga na kuikuza taharuki ya msomaji tangu mwanzo wa kitabu hadi mwisho.

Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa usimilishwaji wa kazi za watoto hauwezi kukamilika bila wahusika kufanyiwa marekebisho yanayofaa. Ikiwezekana, mwandishi anafaa kuwatumia wahusika ambao ni watoto. Iwapo atawatumia wahusika ambao ni watu wazima, basi anafaa kuwasawiri kwa njia ambayo

watakubalika na watoto wanaolengwa. Anaweza kufanya hivyo kwa kuwapa majukumu ambayo watoto wanayafahamu kuwa yametengewa watu wazima katika jamii. Kwa mfano, majukumu kama vile ya uzazi. Pia ni muhimu mwandishi awasimilishe wahusika hawa kwa njia ambayo tabia na mienendo ya wahusika hawa itaaminika na wasomaji wanaolengwa.

Maudhui yanastahili kusimilishwa kwa njia ambayo yatawafunza wasomaji wanaolengwa kuwa watu wenye tabia na mienendo inayokubalika katika jamii. Mienendo na tabia inayofaa na kukubalika katika jamii yastahili ituzwe na ile isiyofaa wala kukubalika iadhibiwe. Utafiti huu umedhihirisha haya kupitia kazi zilizoteuliwa ambapo wahusika wenye mienendo mizuri wanajaliwa mema kama vile Sindbad katika kitabu cha *Alfu Lela Ulela,* ilhali wale wenye mienendo mibaya wanaangamia kama vile mhusika Moni katika kitabu cha *Mkasa wa Shujaa Liyongo* na mfalme Twala katika *Mashimo ya Mfalme Sulemani.*

Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa, usimilishwaji wa umbo la kitabu ni jambo muhimu kwani linaongezea katika ujumi wa matini yenyewe. Pia ,hurembesha kitabu na kikaweza kuvutia macho ya mtoto. Usimilishaji wa umbo unahusisha michoro, maandishi ya chapa na ujalidi wa kitabu. Umbo la kitabu linaweza kuvutia au kutovutia macho ya mtoto kutegemea rangi zilizotumika hasa katika michoro. Usimilishwaji wa umbo la kitabu umedhihirika kuwa ni jambo la muhimu kwani huenda hamu ya mtoto ya kukisoma kitabu ikakatishwa au ikajengwa kupitia jinsi kitabu hicho kinavyoonekana.

Kupitia utafiti huu, imedhihirika kuwa, kazi zilizosimilishwa huenda zikapitwa na wakati na kwa hivyo zinastahili kupitiwa upya iwapo zitaendelea kuwa na mashiko miongoni mwa watoto. Kwa mfano, katika kitabu cha *Mashimo ya Mfalme Sulemani,* kuna baadhi ya mambo ambayo yamepitwa na wakati na hayastahili kuwepo tena katika vitabu vya watoto. Baadhi ya mambo haya ni kama vile kumsawiri Mwafrika kama kiumbe ambaye daima yuko nyuma kiakili, kiuchumi na pia kimaendeleo. Pia kumsawiri Mwafrika kama mtu aliye katili sana kama vile mfalme Twala. Pia, kule kuusawiri utamaduni wa Mwafrika kama ulio na mizizi yake katika mambo ya uchawi. Mambo kama haya yanampa taswira mbaya mtoto kuhusu Mwafrika. Hatimaye mtoto anaathirika kiasi kuwa anamdhamini Mzungu na utamaduni wake huku akiudharau utamaduni wa Mwafrika na Mwafrika mwenyewe.

## 7.3 Kiishio

kutokana na matokeo ya utafiti huu, imebainika kuwa kuna mbinu na mikakati ambayo hutumiwa kuongoza usimilishwaji katika kazi za watoto. Mbinu hizi ni kama vile lugha na matumizi yake, ploti ya hadithi, wahusika katika hadithi, maudhui na umbo la kitabu. Mbinu hizi zimedhihirika kuwa zinaweza kufanikisha au kutinga usimilishwaji na kwa hivyo kuna umuhimu wa mwandishi kuwa mwangalifu jinsi anavyovisimilisha vipengele hivi.

Pia imebainika kuwa, ingawa usimilishwaji huchangia katika kukuza na kupanua fasihi ya watoto, kuna kazi chache mno ambazo zimesimilishwa. Baadhi ya kazi

zingine ambazo zimesimilishwa zimepitwa na wakati na zinahitaji kuangaliwa upya. Vile vile, baadhi ya kazi ambazo zimesimilishwa hazikutilia maanani matakwa ya watoto wanaolengwa na kwa hivyo waandishi walizisimilisha tu kama njia moja ya kuibuka na kitabu cha watoto jambo ambalo limesababisha kuwepo kwa vitabu ambavyo vimesimilishwa kwa njia isiyofaa.

Kwa hivyo, kuna haja ya swala la usimilishwaji kupigwa msasa zaidi iwapo waandishi wanaosimilisha kazi za watoto wataibuka na kazi zilizo na usanifu wa hali ya juu.

## 7.4 Matatizo

Utafiti huu ulikabiliwa na tatizo kuu la ukosefu wa malighafi inayofaa. Swala la usimilishwaji ingawa lina mizizi yake tangu enzi za kipindi cha ukoloni ni swala ambalo halikukuzwa wala kushughulikiwa kwa kipindi kirefu katika usomi. Hii ni kwa sababu, kwa muda mrefu, fasihi ya watoto imekuwa ikidunishwa na kuchukuliwa kuwa fasihi ya kitoto. Kwa hivyo wataalamu wengi hawakuifanyia utafiti. Hakuna maandishi mengi yaliyoandikwa kuhusu swala la usimilishaji katika fasihi ya watoto. Mengi ya maandishi ambayo yametumika katika utafiti huu yametokana na fasihi ya watoto ya Kiingereza ambayo pia ni machache mno, na mengi yake ni yale yameandikwa na wazungu.

Aidha, kuna vitabu vichache mno ambavyo vimefanyiwa usimilishwaji hasa katika lugha ya Kiswahili. Bhaadhi ya vitabu hivi ni: *Elisi Katika Nchi ya Ajabu, Kisiwa*

*Chenye Hazina, Hadithi ya Robinson Kruso, Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo.* Vingi vya vitabu hivi ni vile ambavyo vilisimilishwa na wazungu ili visomwe na watoto shuleni na ambavyo kwa hakika havikuzingatia mbinu na mikakati ya usimilishwaji. Vile vile vitabu hivi vimepitwa na wakati na vinahitaji kuangaliwa upya.

## 7.5 Mapendekezo

Usimilishaji katika fasihi ya watoto ni swala pana mno. Utafiti huu umeshughulikia viwango vitatu tu vya usimilishaji, yaani usimilishwaji wa vitabu vinavyoandikiwa hadhira ya watu wazima kuwa vya watoto, usimilishwaji wa ushairi kuwa riwaya ya watoto na usimilishwaji wa ngano za hadithi simulizi zinazoilenga hadhira ya watu wazima kuwa hadithi za watoto. Utafiti wa baadaye unaweza kushughulikia usimilishwaji katika kiwango cha tamthilia, maaigizo halisi na maigizo ya filamu. Aidha, utafiti huu ulijifunga tu maktabani. Utafiti wa badaye unaweza kujishughulisha na upokezi wa kazi zilizosimilishwa na watoto wanaolengwa kule nyanjani.

## MAREJELEO

Akoilet, E. (1990 "Response and Criticism in Children's Literature in Kenya: The Case Study of Babara Kimenye". Tasnifu Ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Alembi, E. (1991) "Analysis of the Style and Social Significance of the Abanyole Children's Poetry". Tasnifu ya M.A, Chuo KiKuu cha Kenyatta.

_______ (1997) *The Cry of a Goat*. Nairobi: Santex Publishers.

Arbuthnot, H. na Z. Sutherland (1972) *Children's Literature*. USA: Scott, Foresman and Company.

Barker, A. na E. Green (1997) *Storytelling: Art and Technique*. New York: R.R.Bowker Company.

Barnouw, E. (1989) *International Encyclopedia of Communications*. New York: Oxford University Press.

Brenn, E. (mtf.) (1962) *Alfu Lela Ulela*. Nairobi: Longmann Kenya Limited.

Bright, W. (mhr.) (1992) *Internatinal Encyclopedia of Linguistics*. New York: Oxford University Press.

Cass, (1967) *Literature and Young Children*. London: Longman Group Limited.

Chiraghdin, S. (1987) *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman Kenya Limited.

Collinson, R. (1976) "A Sense of Audience", katika Fox, G. (mhr.) (1976) *Writers, Critics and Children*. London: Heinemann Educational Books Limited.

Colwell, E. (1980) *Story Telling*. Britain: The Bodley Head Limited.

Davies, A. (1975) *Literature for Children*. Great Britain: Open University Press.

Fox, G. (mhr.) (1976) *Writers, Critics and Children*. London: Heinemann Educational Books Limited.

Gachukia., E. na S. Akivaga, (1978) *Teaching of African Literature in Schools.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Haggard, H. (1885) *King Solomon's Mines.* London: Penguin Books Limited.

Haviland, V. (1973) *Children and Literature.* London: The Bodley Head Limited.

Holindale, P. (1974) *Choosing Books for Children.* London: Paul Elek Limited.

Holman, C. (1977) *A Handbook to Literature.* USA: The Odyssey Press Inc.

Huck, C. (1979) *Children's Literature in the Elementary School.* New York: Holt Rinehart and Winston.

Hunt, P. (1994) *An Introduction to Children's Literature.* New York: Oxford University Press.

Jahadhmy, A. (1975) *Kusanyiko la Mashairi*: Nairobi: East African Educational Publishers limited.

Johnson, F. (mtf.) (1981) *Mashimo ya Mfalme Sulemani.* Nairobi: Longman Group Limited.

Kahigi, K. (1995) "Lugha Katika Vitabu Vya Watoto", katika Juzuu la *Kiswahili Na. 1.* Dar es Salaam: TUKI

Kawegere, F. (mtf.) (1967) *Shamba la Wanyama.* Nairobi: Phoenix Publishers.

K.I.E, (1992) *K.I.E. Style Manual for Authors and Editors.* Nairobi: K.I.E.

King'ei, K. (2000) *Mwanakupona: Poetess from Lamu.* Nairobi: Sasa Sema Publishers limited.

Kirmani, M. na K. Kirmani (2002) *Oral Literature of the Asians in East Africa.* Nairobi: East Africa Educational Publishers Limited.

Knappert, J. (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literacy History and Anthology.* Nairobi: Heinemann Educational Books Limited.

Knowles, M. na K. Malmakjaer (1996) *Language Control in Children's Literature*. London: Rouhledge.

Leech, G na M. Short (1981) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fiction Prose.* England: Longman Group Limited.

Matti, G. (2005) *Mwongozo wa Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

Matundura, B (2001). *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mbele, J. (1986) "The Liyongo Fumo Epic and the Scholars", katika Juzuu la *Kiswahili Na.53/1* na *53/2*. Dar es Salaam: TUKI.

Mberia, K. (2001) *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

McDowell, M. (1976) "Fiction for Children and Adults : Some Essential Differences." Katika Fox, G. (mhr) (1976). *Writers, Critics and Children*. London: Heinemann Educational Books limited.

Mdee, J. (1986) *Kiswahili: Muundo na Matumizi Yake*. Nairobi: Intercontinental Publishers.

Mkangi, B. (mtf.) (2002) *Kuzielewa Sheria za Watoto ya 2001*. Nairobi: Muungano wa Haki na Ulinzi wa Watoto Nchini Kenya.

Mohamed, S. (1995) *Kunga na Nadharia ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia Hadithi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mpesha, N. (1995) "Children Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its Growth and Development" Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwanzi, H. (1982) "Children's Literature in Kenya: An Analysis of Children's Prose Fiction". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngara, E. (1982) *Stylistic Criticism and the African Novel*. Nairobi: Heinemann Educational Books Limited.

Njogu, K. na R. Chimerah (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Odaga, O. (1985) *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Okhoba, E. (1995) "Style and Meaning of Abimarachi Children's Oral Poetry" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Oyoo, M. (2003) "Theory of Children Literature". A Module. Literature Department. The Catholic University of East Africa.

Ridhiwani, P. (1996) "Shairi la Fumo Liyongo MS 57", katika Juzuu la *Kiswahili Na. 59*. Dar es Salaam: TUKI.

Rotimi, O. (1995) *The Gods are to Blame*. Nairobi: Oxford University Press.

Senkoro, F. (1982) *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Stanely, L. (1937) *Havard Classics: Arabian Nights' Entertainment*. New York: P.F. Collier and Son Corporation.

Tucker, N (1981) *The Child and the Book*. New York: Cambridge University Press.

Tylor, M. (1994) "What Children's Books Tell Us About Teaching Language", katika Styles, M. (mhr.) (1994). *The Prose and the Passion: Children and their Reading*. Great Britain: Redwood Books.

Wamitilla, K. (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.


______________ (2002) *Uhakiki wa Vitabu: Misingi na vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Weche, O. (2000) "Children's Literature An Image Forming Force: Case Study of Ezekiel Alembi's Books". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Watkins, E. (1971) *Chaka the Zulu*. London: Oxford University Press.

Williams, A. na B. Gannon (whr.) (1991) *Romeo and Juliet*. Nairobi: Evans Brothers (Kenya) Limited.

**KIAMBATISHO 1**





KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**KIAMBATISHO 2**



*Umbopa alivyosimama alipovua koti lake kubwa.*

**KIAMBATISHO 3**



Twaona vilele vya milima viitwavyo 'Maziwa ya Shet
inang'aa kama fedha.

**KIAMBATISHO 4**



Mwisho wa pango niliona maiti mwingine amekaa,
chake kimeinamia kifuani.

## KIAMBATISHO 5




*Kizee kichawi Gagula anacheza katika ngoma ya kuwafichu wachawi.*

## KIAMBATISHO 6



*Foulata amejitupa miguuni pa Bwana Good na kuomba amlinde.*

## KIAMBATISHO 7




*Maiti za wafalme wa zamani zimekaa kuzunguka meza, na maiti ya mfalme Twala imekaa juu ya meza imepakata kichwa chake.*

## KIAMBATISHO 8




*Tumetoka katika kijia na kujiona ndani ya shimo refu kwa chini ya Wale Watatu Walio Kimya.*

KIAMBATISHO 9




KIAMBATISHO 10




*Sindbad anaachwa baharini na wenzake*

**KIAMBATISHO 11**



*Sindbad katika bonde la majoka*

**KIAMBATISHO 12**




*Sindbad katika shimo la maiti*

## KIAMBATISHO 13




*Rok wanailenga jiwe jahazi*

## KIAMBATISHO 14



*Tembo anamweka Sindbad juu ya mgongo wake*

## KIAMBATISHO 15




*Kifo cha kijitu chenye kibiongo*

## KIAMBATISHO 16



*Alnacha analipiga kapu lake teke*


KIAMBATISHO 17




KIAMBATISHO 18



KIAMBATISHO 19



KIAMBATISHO 20




**KIAMBATISHO 21**




**KIAMBATISHO 22**




**KIAMBATISHO 23**



**KIAMBATISHO 24**



**KIAMBATISHO 25**



**KIAMBATISHO 26**



**KIAMBATISHO 27**



**KIAMBATISHO 28**

